ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Pili – Tarehe 14 Juni, 2010

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti (Mhe. Haji Omar Kheri):

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 1010/2011.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi, afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi (Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji):

Hotuba ya maoni ya upande wa Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 47

Kupandishwa kwa Gharama ya Kugombea Uchaguzi

Mhe. Ali Abdulla Ali: Aliuliza:-

Hivi karibuni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imetangaza katika vyombo vya Habari kuwa imepandisha viwango vya Fedha za dhamana kwa Wagombea nafasi za Uongozi katika Uchaguzi wa Oktoba 2010 kama ifuatavyo:- Shilingi 3,000,000/= (Mgombea Urais), badala ya Shilingi 1,000,000/=, (Mgombea Uwakilishi na Mbunge), 3,000,000/= na Shilingi 50,000/= (Mgombea Udiwani).

(a) Mhe. Waziri, kigezo gani kimetumiwa kuongeza bei hiyo inayopindukia asilimia mia moja.

(b) Huoni kuwa ukubwa wa ada hiyo utawanyima baadhi ya watu haki yao ya kikatiba na ya kidemokrasia ya kugombea uchaguzi.

(c) Kwa nini ada hiyo isiongezwe kwa kiwango kinachoweza kulipwa na wananchi waliowengi wenye nia ya kugombea uchaguzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu a, b, na c kama hivi ifuatavyo:-

Lakini pia katika marekebisho aliyoyafanya bado nitafanya marekebisho tena.

a). Mhe. Spika ni kweli Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imetangaza mabadiliko kwa viwango vya fedha za dhamana kwa wagombea wa nafasi za Uongozi katika Uchaguzi wa Oktoba 2010 . Kigezo kilichotumika kuongeza bei hiyo ni:-

1. Kwanza ni kuona mtu *serious ness* ya mtu anayetaka kugombea nafasi hizi na isiwe kila mtu anakwenda kuchukua fomu tu bila ya kuonyesha *serious ness* yoyote.

2. Kulingana na uzito wa dhamana za Mgombea husika kwa nafasi anayoomba.

3. Kiwango cha dhamana kilifikiwa baada ya Tume kukaa pamoja na wadau wake vyama vya siasa na kukubaliana viwango vifuatavyo Nafasi ya Rais Shs. 2,000,000/= Muwakilishi Shs. 200,000/= na Diwani shs. 50.000/= hayo ndio marekebisho waliyokubaliana pamoja na wadau..

b). Mhe. Spika , ukubwa wa ada hiyo hautowanyima baadhi ya watu haki yao ya kikatiba na ya kidemekrasia ya kugombea uchaguzi, kwa sababu nafasi hizo ni kila mmoja na ukubwa wa dhamana anazoomba, pia na imeangaliwa uwezo wa mtu kwa nafasi anayoiomba.

c). Mhe. Spika , uamuzi huo umechukuliwa baada ya maombi ya wadau kuliangalia kwa undani na umuhimu wake kwa kila nafasi na ikaonekana upo uwezekano wa kila mwenye azma ya kugombea anaweza kutoa ada hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Angalau hizi mbili za juu zinaweza kufahamika kwamba zina mantiki, lakini hii ya diwani tunawafanya hawa ambao hawana uwezo wasiingie katika safu za uongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Kwanza nashukuru kwamba ameona mashauriano yalivyokuwa mazuri mpaka vikafikia hivyo viwango ambavyo vimetwajwa na hichi cha 50,000/= nacho pia kimefikiwa baada ya majadiliano ya wadau wanaohusika na wadau wanaohusika juu ya suala hili.

Mhe. Spika, nilisema mwanzo kwamba ni kujenga *serious ness* ya kwenda kuchukua fomu ili kuona kwamba huyu mtu anayetaka kwenda kuchukua fomu anaweza kufanya kampeni ya kutosha na kuzungumza na wananchi ili waweze kukubalika na kumpa kura yake na kujitangaza vizuri kwenye sera yake, hilo ni suala muhimu kabisa ambalo linatakiwa liwepo katika masuala haya. Na kama amefanikiwa na akapata asilimia kumi ya kura basi *deposit* yake hurejeshewa sio kwamba inachukuliwa moja kwa moja, lakini ukishindwa ukipata chini ya asilimia kumi *deposit* imekwenda na maji.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Hii fedha iliyowekwa kwa mgombea urais na Muwakilishi tumesema ni moja katika vigezo vilivyochukuliwa ni kuwa *serious ness* kwa mgombea, lakini mtu anapotaka kugombea huwa amejiamini na wengine kimaumbile kama alivyowajaalia mwenyezi Mungu wana uwezo zaidi hata hawa wenye uwezo wa pesa na kujaza hizo fomu. Kwa hivyo kibali cha mtu na *serious ness* inahusiana vipi na yule mwenye uwezo lakini hana fedha asiweze kuingia kwa sababu hana fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, tunapokwenda kugombea katika nafasi bila ya shaka kwa mujibu wa katiba yetu tunakwenda kwa mujibu wa vyama vyetu hii imewekwa kuwa ni kipimo cha kuweza kumwambia mtu kama unakuja huku basi ni vizuri uje kulinda hiki ili kikurejee

mwenyewe baadae. Kwa hivyo hilo sio suala la mtu kuwa na pesa nyingi au vipi, lakini ni lazima kuwe na kipimo cha mtu kuweza kukilinda hicho kitu anachokitaka ili pesa zake azilinde ili zisipotee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa Mhe. Waziri ametwambia kwamba fedha hii imezingatia *serious ness* ya mgombea je, yuko tayari sasa kushauriana na vyama ili hii *serious ness* ianze kwenye mkakati wa chama.

b) Baada ya uchaguzi kumalizika na mgombea akapata asilimia kumi fedha hii hutakiwa irejeshwe baada ya muda gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mchakato wa Chama kila chama kina utaratibu wa mchakato wake kwa hivyo hapo siwezi kuzungumzia chochote.

Suala la kurejeshwa ni baada ya kuwa ameshafanikiwa arejeshewe fedha zaka kama ameshavuka ile asilimia kumi na kama hajarejeshewa anachotakiwa ni kuomba fedha yake arejeshewe.

Nam. 38

Kuachiliwa kwa Watuhumiwa

Mhe. Fatma Abdalla Tamim (Kny: Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi) - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada zinazochukuliwa kupunguza uhalifu nchini, bado kuna tatizo la kuachiliwa kwa watuhumiwa wanapokamatwa na Polisi kwa tuhuma mbali mbali. Jambo hilo linawakera wananchi na linawavunja moyo kushirikiana na Polisi katika harakati za kupambana na uhalifu.

Kwanini wahalifu hao waachiliwe ilhali baadhi yao hukamatwa na ushahidi kamili kama vile silaha za moto.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako,napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 38 kama ifuatavyo:-

Muhalifu anapokamatwa na Polisi kwa tuhuma yoyote ile ni lazima ufanyike uchunguzi wa kina kuhusu tuhuma zinazomkabili. Baada ya upelelezi kukamilika ushahidi uliopatikana lazima uwe wa kutosha kuweza kuthibitisha kosa pasi na kuacha shaka.

Kwa upande mwengine Sheria ya Mwenendo wa Jinai Namba 7/2004 ya Zanzibar kupitia kifungu cha 28 kinawataka Polisi wasikae na mhalifu kwa zaidi ya saa 24 bila ya kumpeleka Mahakamani. Kwa maana hiyo kama Polisi watakuwa hawajapata ushahidi unaoridhisha kuweza kuthibitisha kosa ndani ya saa hizo 24, wanatakiwa kumuachia mhalifu kwa kumpa dhamana ya Polisi ambayo ni kumjazisha bondi ili wao waendelee na uchunguzi wa thuhuma hizo.

Hii haina maana kuwa anapoonekana anatembea mitaani huwa tuhuma au mashtaka dhidi yake yamekwisha, isipokuwa upande wa Polisi wanaendelea na upelelezi bila ya kuvunja sheria ya kukaa na mhalifu. Polisi wanapokamilisha uchunguzi wa ana kujiridhisha kuwa kuna ushahidi wa kutosha wanamfikisha Mahkamani muhalifu huyo ili aweze kushtakiwa.

Ikumbukwe kuwa moja ya mikakati ya Serikali ya kulinda haki za mtuhumiwa katika masuala ya mashtaka, ni kuhakikisha upelelezi wa makosa ya jinai unakamilika kwanza ndio kufungua kesi Mahkamani, isipokuwa kwa kesi maalum. Kama vile kesi ambazo hazina dhamana kwa mujibu wa Sheria (kuua kwa makusudi au kupatikana na silaha, au inapoonekana mhalifu anaweza kutoroka atakapopewa dhamana na Polisi na hakuna uwezekana wa kumpata kirahisi.

Kulazimisha kumfikisha mtuhumiwa Mahkamani bila ya kukamilisha upelelezi wa kosa linalomkabili kutapelekea kesi hiyo kufutwa na mahkama chini ya kifungu cha 209 (2) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Namba 7/2004 kwa kutoanza kusikilizwa ndani ya miezi minne kuendesha kesi bila ya kuwa na ushahidi wa kutosha, upande wa mashtaka unaweza kushindwa kuthibitisha kosa bila ya kuacha shaka na kupelekea Mahakama kumuachia huru mtuhumiwa.

Ikumbukwe kuwa kumfungulia mtu mashtaka bila ya kuridhika kuwa ushahidi uliopo unaweza kumtia hatiani ni kosa la kimadai la mashtaka ya uonevu (malicious prosecution) ambalo maarufu tunaita siku hizi "**kumbambikiza kesi".** Hivyo Polisi na Waendesha Mashtaka wanatakiwa kuwa makini kabla ya kumfungulia mtu mashtaka.

Hivyo basi, haitakuwa busara na ni kinyume cha Sheria kwa Polisi kuendelea kumshikilia mtuhumiwa zaidi ya saa 24. Aidha ni kosa kwa upande wa mashtaka kufungua mashtaka Mahkamani wakati wakijua kuwa hawana

ushahidi wa kutosha dhidi ya mtuhumiwa huyo. Pamoja na maelezo hayo yanayohusu taratibu za kisheria za kufungua mashtaka na dhamana kwa washtakiwa, nakubalina na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba inawezekana watendaji wasio waaminifu ambao wapo katika kila taasisi wanaweza kutumia mwanya huo wa kisheria vibaya. Namuomba Mheshimiwa Mwakilishi na wananchi kwa ujumla yanapotokea matokeo yanayowatia shaka kuwa taratibu zimekiukwa ni vyema wawasilishe malalamiko yao ngazi za juu za uongozi wa Polisi kama vile Makamanda wa Mikoa au Makamishna wa Polisi haraka iwezekanavyo ili kupatiwa ufumbuzi malalamiko yao.

Ni imani yangu kuwa viongozi wa Jeshi la Polisi ni waadilifu na wanafuata Sheria, hivyo ni vyema tuwatumie katika kurekebisha kasoro za kiutendaji zinazojitokeza.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu mama amezungumzia masuala mengi yanayohusiana na sheria na mtuhumiwa.

a) Je, ipo sheria yoyote ambayo inamnyima haki mtuhumiwa kupata dhamana kwa baadhi ya makosa.

b) Hivi sasa maeneo mengi tumeanzisha polisi jamii kwa lengo la kusaidia wenzetu walinzi hawa ili tuweze kwenda sambamba. Je, ikiwa muda mdogo tu anakamatwa mtuhumiwa halafu baadae anaonekana mitaani hii si kuwachonganisha baina ya polisi jamii na huyo mtuhumiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora: Nimesema katika jibu mama kwamba yapo makosa ambayo mtuhumiwa huwa hastahiki kupewa dhamana.

Pili hili suala la muda mdogo kuachiwa hapa Zanzibar nadhani ipo haja sasa ya sisi wananchi kwa jumla kuondoa muhali na kutoa ushahidi, maana bila ya kutoa ushahidi ni kweli utafika wakati watalazimika polisi kumpeleka mtu Mahakamani bila ya upepelezi kukamilika kwa sababu sisi tuna muhali hatuwezi kupeleka ushahidi na kama unapeleka kesi ushahidi haujakamilika kesi ile hufutwa kama nilivyosema mwanzo. Kwa hivyo mimi nafikiri ni jambo la busara tuwe tayari wananchi sote kupeleka ushahidi wakati tatizo linapotokezea ili mtuhumiwa yule kesi yake imalizwe bila ya kukaa muda mrefu.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Endapo tayari mtu kapeleka kesi polisi na tayari ikafunguliwa jalada na ikafikia pahala pa kupelekwa Mahakamani ikapelekwa, lakini alipofungua kesi kapeleka na vielelezo ambavyo vimewekwa katika jalada.

Je, endapo vielelezo vile vikipotea pale polisi ni hatua ipi mtu yule anaweza kuichukua.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora: Katika jibu langu nilisema kwamba wapo watumishi wachache ambao si waadilifu katika kazi yao, kwa hivyo suala hilo linapotokea anatakiwa yeye kutoa taarifa katika ngazi za juu za wahusika wa polisi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa busara za majibu ya Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kuna kesi nyengine hutokea tena zina ushahidi kamili lakini kwa bahati mbaya kesi zile kabla ya kupelekwa Mahakamani utakujaona tu yule mtu ameachiwa na yuko huru wakati ile kesi ilipelekwa na ushahidi kamili, sasa kama polisi watakuwa wanafanya hivi kuwa na taaluma yao ya kusamehe kitu ambacho kina ushahidi kamili.

Je, yule aliyedhulumiwa haki yake fanye nini?.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora: Ushahidi unaotakiwa Mahakamani ni ushahidi usioacha chembe ya shaka, kwa hivyo kwa wewe kwa utaalam wako unaweza kuona kwamba ushahidi ule ni kamili lakini kumbe umeacha shaka kwa hivyo ndio maana anaachiwa.

Nam. 17

Mkakati wa Kuimarisha Kilimo cha Maweni

Mhe. Ashura Abeid Faraji - Aliuliza:

Kwa kuwa kilimo ndiyo tegemeo la wananchi kujikwamua na umaskini.

Wizara ina mkakati gani kwa maeneo ambayo ardhi yake ni mwamba wa jiwe kama vile Micheweni, Mwambe, Vitongoji, Chwaka na Makunduchi.

Mhe. Naibu Waziri Wa Kilimo Mifugo Na Mazingira - Alijibu

Mhe Spika, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika ,kuna mazao maalum yanayomea vizuri katika ukanda ya maweni na Makaani yakiwemo ya Micheweni Mwambe na Vitongoji pamona na Makunduchi. Mazao ya maeneo hayo ni pamoja na Mbaazi, Chooko , Kunde, Mahindi, Mtama, Pilipili hoho , Viazi vikuu na aina za Migomba na mboga mboga . Aidha baadhi ya mazao ya matunda kama embe na jamii ya michungwa pia hulimwa ukanda wa maweni.

Mhe. Spika , Wizara ya Kilimo ina mikakati ya kukuza Kilimo cha Maweni Miongoni mwa mikakati hiyo ni ile ya kutoa huduma ya Elimu kwa Wakulima kupitia Skuli za wakulima, kuzalisha mbegu zinazohitajika kwa mazao ya maweni na kuhifadhi mazingira ya maeneo hayo yasiharibiwe vile vile katika tafiti zinazofanywa katika vituo vya utafiti , mazao ya maweni yanafanyiwa utafiti wa kupata mbegu bora.

Mhe. Spika , Wizara ya Kilimo haizalishi , bali wazalishaji ni wakulima, na wana uhuru wao wa kuchagua anachotaka kulima . Na ndio maana wakulima wengi wameacha kulima mtama na pili pili na badala yake wakaenda kunako kilimo cha maweni ambao wameona kuna soko na maslahi mazuri.

Hata hivyo wizara yangu inaendelea na juhudi za kuzungumza na wakulima pamoja na kulima mwani waendelee na kilimo cha maweni ili waweze kuongeza tija na kipato.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu amezungumza kwamba wakulima wa maweni wanapatiwa huduma na elimu ili wafanikiwe katika uzalishaji na mazao ambayo wameyataja ni mtama, mbaazi na chooko n,k.
Hivi nimuulize mimi ni mkulima wa maweni naishi Mfurumatonga Matemwe Wilaya ya Kaskazini (A)

a) Je, huduma hii ilipatikana kituo gani.

b) Katika uotaji wa elimu ni elimu gani iliyotolewa ya ukulima, elimu ya upandaji au elimu ipi.

c) Hivyo utafiti gani umefanywa katika ukulima wa maweni na wamegundua mbegu gani zaidi ya kuliko iliyokuwepo ni lini na pia kituo gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Kwa sababu suala lake linataka vielelezo vingi na mimi nataka nikiri kwamba sikujiandaa na vielelezo hivyo kwa hivyo nitajibu suala hili kwa maandishi.

Mhe. Subeti Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa sababu na mimi ni mkulima wa maweni katika eneo ambalokuwa limetajwa la Micheweni, atakubaliana na mimi kwamba kuna baadhi ya vilimo ambavyo vinakubali katika sehemu za Micheweni navyo hajavitaja kwa mfano kama viazi vitamu na mbatata zinakubali kwa wingi.

Je, serikali au kupitia Wizara yake alikwenda lini kuwaelimisha wananchi ili waendelee kulima vilimo hivyo. Na katika hiyo elimu inayotolewa ni lini imetolewa Micheweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Nataka nimwambie hatulaumiani hapa kwenye Barazal kakini mara nyingi tunapofanya ziara katika maeneo yetu tabia ya kutukimbia inajitokeza, pale Micheweni kuna darasa ambalo tumeanzisha pale na mimi nimetembelea na tulichoanzisha pale ni suala la kulima viazi vikuu.

Kwali viazi vitamu vinakubali lakini kama tulivyosema wakulima wana hiari yao katika kuchagua sisi kama Wizara ya Kilimo tunatoa taaluma, sasa wakulima wenyewe ndio wanaamu kwamba sisi tutalima viazi vitamu au mbatata lakini kwa eneo ambalo anatoka yeye Micheweni ambako ndio kwetu sote mimi nay eye, kule wakulima mara nyingi wanapendelea kulima mtama na pia kwa sababu kuna kilimo chengine ambacho kinakubali zaidi kama migomba lakini sio wakulima wengi ambao wamejiandaa na kilimo kile.

Mhe. Ali. Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mimi si mkulima wa maweni lakini kwa bahati nzuri nimezaliwa katika ukanda huo wa Mashariki wa pwani kwa sababu ukanda wa Makunduchi mpaka Kiwengwa, Matemwe na Nungwi ni mmoja mpaka Micheweni siku nyengine tunalingana.

Zamani wakati huo sisi ni wadogo ukulima wa maweni ulikuwa na tija sana na ulikuwa unasimamiwa vizuri na manufaa mengi yalipatikana hasa ukiangalia katika mazao mbali mbali aliyoyataja Mhe. Waziri kama Mahindi, mtama, uwele, viazi vitamu hata baadhi ya maeneo muhogo lakini kuna na zao moja kubwa sana la pili pili hoho.

a) Je, Mhe. Waziri atahamasisha wananchi kiasi gani ili wananchi waingie katika zao la pili pili hoho ambalo lina soko kubwa huko nje.

(b) b) Kwa kuwa mazingira yanalindwa ili misitu isikatwe atawafahamisha vipi wananchi watumie njia ipi iliyo bora ili msitu wetu ustirike ili kulinda hifadhi ya mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo moja katika tatizo ambalo tulilonalo ni wakulima wenyewe kuamua kulima kilimo hicho cha pilipili. Kwa hivyo tunaomba kwa kupitia Baraza lako tukufu pamoja na yeye na wakulima wengine tushirikiane ili kuhakikisha kwamba tunawahamasisha wananchi wetu ili kuona wanaingia katika kilimo cha biashara ili wapate kuachana na suala zima la ukataji wa miti, hilo ndio lengo letu.

Nam. 3

Wahitimu Chuo Cha Afya Mbweni

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Jimbo la Ziwani) - Aliuliza:-

(a) Ni wahitimu wangapi wa fani za afya waliomaliza Chuo cha Afya Mbweni mwaka 2009.

(b) Je, wahitimu hao waligawiwa vipi katika sehemu za kazi.

(c) Wizara inachukua hatua zipi kulishughulikia suala la upunguaji mkubwa wa Manesi katika Hospitali za Pemba.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 3 lenye vifungu (a) , (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo;-

Mhe. Spika wahitimu wa fani za afya waliomaliza Chuo cha Afya Mbweni Zanzibar mwaka 2009 ni 241.

Mhe. Spika wahitimu hao walikuwa katika fani zifuatavyo:-

1.	*Diploma in General Nursing and midwifery*	-	*46*
2.	*Diploma in General Nursing and psychiatry*	-	*24*
3.	*Diploma in Environmental Health Science*	-	*40*
4.	*Diploma in Clinical Medicine*	-	*31*
5.	*Diploma Medical Laboratory Sciences*	-	*30*
6.	*Diploma in pharmaceutical Sciences*	-	*25*
7.	*Certificate in Public Health Nursing Grade 'B-*		*45*
	Juma la wahitimu ni :-		**241**

Aidha napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kuwa idadi hiyo ni ya jumla ambayo inajumuisha wanafunzi ambao tayari walikwisha ajiriwa wakati wanajiunga na Chuo hicho (*inservice*). Wanafunzi kutoka taasisi binafsi (*private*) na wanafunzi ambao hawajaajiriwa wakati wanajiunga na Chuo na walitakiwa kuajiriwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii baada ya kumaliza masomo yao.

Wanafunzi ambao walipaswa kuajiiriwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii baada ya kumaliza masomo yao ni 163 kama ifuatavyo:-

1.	*Nurses*	-	*61*
2.	*Health Officers*	-	*22*
3.	*Clinical Officers*	-	*27*
4.	*Laboratory Assistant-*	-	*22*
5.	*Pharmaceutical Assistant*	-	*18*
6.	*Public Health Nurse Grade B*	-	*13*

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi , Zanzibar tayari imeshawaajiri kundi la mwanzo la wahitimu hao lenye jumla ya wahitimu 88 linalojumuisha wauguzi (*Nurses*) wote 61 na maofisa tabibu *(Clinical Officers)* wote 27 na wamegaiwa katika sehemu zao za kazi kama ifuatavyo:-

WAUGUZI:

1.	Hospitali ya Mnazi mmoja	-	30
2.	Hospital ya Kivunge	-	8
3.	Hospital ya Kidongo chekundu	-	3
4.	Hospital Mwembe-ladu	-	2
5.	Hospital Pemba	-	18
			61

Aidha napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kuwa wauguzi wengi wamepelekwa katika Hospital kuu ya Mnazi mmoja kwa vile wauguzi wengi

katika Hospital hiyo wapatao 35 hivi sasa wamekwenda masomoni Tanzania Bara kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kwa upande wa maofisa tabibu *(Clinical Officers)* wote wapo katika Hospital ya Mnazi mmoja wakifanya kazi chini ya uangalizi (*internship*) kwa muda wa mwaka mmoja kama ulivyo utaratibu wa fani hiyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na ustawi wa jamii inaendelea na hatua za kulishughulikia suala la uajiri wa wahitimu wengine waliobakia tutawaajiri.

Aidha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaendelea na jitihada zake za kuongeza idadi ya wafanyakazi wa kada za afya wakiwemo wauguzi katika Hospitali za Pemba kwa kadri ya mahitaji na uwezo unavyoruhusu, upanuaji wa chuo cha Afya Mbweni ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi ni miongoni mwa hatua muhimu za kukubaliana na upungufu wa wafanyakazi wakiwemo wauguzi katika Hospitali za Unguja na Pemba.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Katika kutaja wauguzi walivyogawiwa katika mahospitali alisema Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Kivunge, Hospitali ya Kidongo Chekundu, Hospitali ya Mwembeladu lakini mwisho akasema Hospitali za Pemba 18. Napenda nijue hospitali za Pemba zipo sita je, ziligawiwa vipi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, Pemba tumepeleka wauguzi 18 na juu ya Afisa Mdhamini wa Pemba kuwagaiya wauguzi hao kwa mujibu wa mahitaji ya hospitali za Pemba zote sio sita. Kwa sababu muuguzi haendi kwenye hospitali kuu, muuguzi anakwenda hata kwenye kituo cha afya.

Kinachotokea Mhe. Spika, nakiri kwamba ni kidogo. Hilo nalikubali na juhudi na jitihada tutazifanya kukabiliana na tatizo hilo ala upungufu wa wafanyakazi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nafurahi kuwa Wizara ya Afya imejitahidi kuwasomesha madaktari kwa wingi sana. Lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri kuwa hivi karibuni tulikuwa Pemba ni wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii. Moja katika mambo ambayo tuliyapokea kwa masikitiko sana kwa hospitali za Pemba ni upungufu wa madaktari pamoja na wafanyakazi wa hospitali. (*Makofi*)

Tatizo kubwa linalochangia wizara yenyewe inasema bado haijaajiri kwa sababu inasubiri majibu ya *scheme of service* kutoka serikalini, hivyo hilo. jibu la *scheme of service* wameshapewa wenyewe Wizara ya Afya na kama wameshapewa kwa nini hawalifanyii kazi. Lakini kinachosikitisha hata *orderly* na madereva pia tatizo huko Pemba. Hivyo nani aliyezuia utaratibu wa kuajiri watu mpaka ikafikia kiwango kwamba wananchi wanapata tatizo la huduma mahospitalini kwa sababu ya kuwa *scheme of service* haijatengenezwa kwa hivyo ajira hakuna.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, swali lake zaidi linahusiana na *scheme of service*. Mhe. Spika, kama sitojibu vizuri basi nitamuomba Mhe. Dokta Mwinyi Haji anisaidie, nitajitahidi.

Mhe. Spika, hivi sasa tunachokifanya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunataka kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwanza kuwapatia mahitaji mazuri ya malipo yao. Hili ndio tunalolinya hivi sasa. Baadaye itafuatia ajira ya hao ma-*orderly* na madereva aliozungumza Mhe. Mwakilishi.

Kwa hivyo tunachokifanya sasa hivi serikali ni kuboresha maslahi ya wafanyakazi kwanza wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwapatia malipo mazuri, lini? Mhe. Waziri wa Fedha atasema. Lakini baadaye mambo yakisha kamilika tutaanza kuajiri wengine kama madereva, ma-*orderly* na wengineo.

Mhe. Spika: Sijui kuna majibu ya nyongeza Mhe. Dokta Mwinyihaji?

Mhe. Waziri wa Fedha: Inatosha.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Pemba madaktari ni kidogo katika vituo vya afya na kwa kuwa Mhe. Waziri kasema wahitimu ni 241. Je, Mhe. Waziri katika wahitimu hao 241 Pemba ni wangapi na unguja ni wangapi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, wahitimu hao wote ni 241, tuliowapeleka Pemba ni 18, waliobakia wote tumewapeleka Unguja.

Nam. 13

Barabara ya Mwakaje - Mwachealale

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Barabara ya kutoka Mwakaje kwenda Mwachealale mwaka juzi ilipata mdau wa maendeleo na kuilipa UUB Shs. 18 millioni kwa ajili ya kuitengeneza kwa kifusi. Kwa bahati mbaya kazi iliyofanywa sio nzuri. Kifusi kilichowekwa ni cha unga. Vile vile Calvat na vibomba vipo lakini tangu wakati huo havijawekwa kwenye sehemu zinamostahiki.

(a) Mhe. Waziri kwa kuwa UUB walilipwa ili wafanye kazi hiyo vizuri na waikamilishe, ni jambo gani lililosababisha wasifanye kwa kiwango kizuri na wasikamilishe.

(b) Kwa kuwa kutokana na uduni wa kazi iliyofanyika shida ya wana kijiji wa Mwachealale bado haijaondoka. Wazara ina mpango gani wa kuishughulikia njia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika Kikao cha Baraza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 13 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, nakiri kuwa wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Bara bara iliifanyia matengenezo barabara ya Mwachealale kwa kiwango cha kifusi na kuondosha kero ya usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo.

Aidha napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa asiwe na wasi wasi kwani kifusi kilichotumika katika ujenzi wa barabara hiyo, hakikuwa na kiwango, kwa sababu bara bara zote za kati zimejengwa kwa kutumia kifusi kutoka katika shimo hilo hilo ambalo lilitumika pia kwa barabara ya Mwachealale.

Vile vile napenda kutoa taarifa kuwa barabara inayojengwa kwa kifusi hudumu kwa miaka isiyozidi miwili hivyo hutakiwa kurudiwa tena kwa kufanyiwa matengenezo mengine. Aidha kazi kama hizo huingizwa tena katika mpango wa kazi wa Idara. (*Periodic*).

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi naomba nimuulize kama ifuatavyo:-

Amekiri kwamba njia yetu ya Mwachealale imetengenezwa kwa kiwango cha kifusi. Anasema barabara kama hizo kitaalamu huchukua miaka miwili zimeshamalizika, barabara yangu mimi sasa hivi imeshazidi na amesema ikizidi hapo hutiwa kwenye ratiba ya wizara ili kurekebishwa barabara hiyo.

(a) Je, na hii ya Mwachealale imeshatiwa katika ratiba hiyo.

(b) Katika utengenezaji wa njia hiyo palikuwa na tatizo la kuweka kibomba na vibomba hivyo vimewekwa pembeni ya eneo hilo huu sasa ni mwaka wa pili lakini havijawekwa kwenye njia, je na hivyo vitakuja kuwekwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kufatilia kwa karibu barabara hiyo ambayo ipo katika jimbo lake. Lakini pia nimueleze kwamba tutaingiza barabara hiyo katika matengenezo kwa kupitia mfuko wa barabara. Na hilo eneo la calvat ambalo halijashuhulikiwa basi kwa kushirikiana nae basi tutakwenda kuona kwamba hiyo hali ikoje na tuweze kufanya kazi hiyo kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongeze kujibu swali (b) kidogo tu.

Mhe. Spika, nikiri kwamba barabara ya Mwachealale ilijengwa kwa kifungu na mimi nimeshawahi kuitembelea kwa sababu pia na mimi ni sehemu ya wapiga kura wangu. Sehemu ambayo ina matatizo ni pale Mwachealale mwanzo.

Tatizo kubwa la sehemu ile ni magari ya mchanga yanayopita ni mazito na huharibu njia. Kuhusu calvat tulipeleka mbili moja tuliiweka lakini moja hatukuizika kwa sababu wataalamu wetu wamesema kwamba ile moja iliyowekwa inatosha kabisa kwa shuhuli za pale.

Sasa Mheshimiwa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kuhusu matengenezo mengine tutaangalia kila hali itakaporuhusu na nilipata fununu kuwa Mheshimiwa Mwakilishi alisema kuwa fedha zipo, anazo, sasa kama zipo basi azilete ili tummalizie hiyo shuhuli iliyobakia pale.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

(a) Kwa kuwa wamekiri kwamba barabara za kifusi hudumu si zaidi ya miaka miwili ni kwa nini wataalamu wake huwashauri kujenga barabara kwa kifusi ambazo huharimu fedha nyingi lakini muda wa wa kudumu ni mdogo.

(b) Njia hii kwa sababu imejengwa kwa kifusi na muda wake wa maisha tayari umepita je, atakuwa tayari kutwambia kwamba bajeti hii haitamalizika atafanya kama ile barabara ya Magomeni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ukweli ni kwamba hata sisi wizara tungelipenda barabara zote ziwe za lami hapa Zanzibar, kwa barabara ya kawaida tu ya lami basi inatugharibu kati ya milioni 400 mpaka milioni 800 kilomita moja. Lakini tukijenga kwa kifungu pengine hata milioni 20 au 50 tunaweza tukatia kifusi hata kilomita 5. Kwa hivyo wakati mwengine tunajihami tu lakini barabara hasa ni lami, lakini kutokana na hali ya uchumi wa nchi yetu tunakwenda taratibu, tunategemea baada ya muda Zanzibar nzima itakuwa na lami kwa sababu tunakwenda vizuri.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika masawazishoi ya majibu yake hapa alisema Mwachealale kuna wapiga kura wake kwa hivyo ataangalia sana ili kufanya ukarabati wa ujenzi wa barabara hiyo.

(a) Je, huku kulikokuwa hakuna wapiga kura wake na ambapo kuna wananchi wetu na wao wanahitaji masuala ya barabara kama Mboriborini/Amani, Kipanga/Kwaboko, lini anategemea na kutufikiria angalau kujengewa barabara hizi ili kuondosha makero haya.

(b) Je, kuna mifuko mingapi katika Wizara yake ambayo inahusika na masuala ya barabara ili nielewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, niliposema kwamba Mwachealale kwamba kuna wapiga kura wangu kwamba nafika, basi hata na Amani kuna wapiga kura wangu maana mimi ni M-NEC wa Mkoa wa Mjini Magharib kwa hivyo natembelea maeneo yote, nilikusudia kuwa huko kote nafika na na hiyo hiyo barabara ya Mwachealale. Kwa hivyo ikifika muda na barabara ya mboriborini nako mambo yatakuwa mazuri.

Mfuko wa kutengenezewa barabara ni mmoja na uko chini ya Wizara ya Fedha, lakini watumiaji wakubwa au wa asilimia 100 ni sisi Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Tunashukuru sana kwamba mfuko huu unafanya kazi nzuri, tunapata fedha za kutosha ndio maana tunautaratibu mkubwa wa kuzifanyia ukarabati barabara za mjini, baada ya mwezi mmoja mtaona mabadiliko ya mji wetu wa Unguja.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti (Mhe. Haji Omar Kheir): Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, nikiwa na afya njema na kuniwezesha kutekeleza shughuli hii ya kawaida ya kila mwaka ya kujadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama Kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinavyoelekeza.

Mhe. Spika, aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kuchangia bajeti hii nikiwa mtu wa kwanza, kwa niaba ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda pia, kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyoyaonesha wakati wa kupitia taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011; na hatimae kutoa mchango na maoni kwa kusimamia misingi imara ya ukusanyaji wa kodi za serikali na kuelekeza katika maeneo muhimu wa maendeleo ya nchi yetu sote.

Mhe. Spika, naomba niwatambue rasmi waheshimiwa wajumbe wa kamati hii ambao walipata nafasi ya kushiriki kwenye Kamati yetu kwa mujibu wa kanuni kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Haji Omari Kheri	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali	-	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	-	Mjumbe
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mjumbe
5. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	-	Mjumbe
6. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe
7. Ndg. Mdungi Makame Mdungi	-	Katibu
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu

Mhe. Spika**,** kwa kuwa tunazungumzia suala la Bajeti Kuu ya Serikali ni vizuri tukaendelea kumsifu Dkt. Karume kwa kusimamia misingi imara ya ukusanyaji wa kodi za Serikali na kuzielekeza katika maeneo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Sote tunakumbuka kwenye miaka ya 1990 hadi 2000 hali ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali yalikuwa vipi. Kwa msingi huo tunapomsifu hamtusifu kwa sababu ya ukaribu wetu, lakini tunamsifu kwa sababu ya umahiri wake na uzalendo wa kuipenda nchi yake katika kusimamia rasilimali za nchi hii.

Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ushirikiano makubwa waliotupa wakati wa kuupitia Mpango wa Maendeleo na Bajeti hii tunayoijadili leo hii. Vile vile, naomba niwapongeze tena Watendaji wa Wizara hii kwa kumuandalia hotuba nzuri inayoeleweka vyema na pia kwa Mhe. Waziri binafsi kwa kuiwasilisha hotuba hiyo ndefu mbele ya Baraza hili kwa ustadi mkubwa na bila kuchoka. Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo na

Bajeti hii imebeba matumaini ya kuongeza maisha bora ya wananchi wetu.
Mhe. Spika, matumaini hayo yanatokana na mipango madhubuti iliyomo kwenye Bajeti hiyo pamoja na hatua mbali mbali ambazo serikali inakusudia kuzichukua katika mwaka ujao wa fedha zinazolenga kuleta hali nzuri ya maisha kwa wananchi, chini ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) uliozingatia Malengo ya Milenia *(Millennium Development Goal's – MGDs).*

Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

Mhe. Spika**,** Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar inaipongeza kwa dhati Serikali ya Mapinduzi - Zanzibar kwa mafanikio iliyopata katika mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na changamoto mbali mbali tulizozikabili za ndani na nje ya nchi kwa kutekeleza bajeti iliyojulikana kuwa ni ***Bajeti ya Maendeleo ya Miundombinu kwa kuimarisha Kilimo na Utalii*** kwa ufanisi mkubwa**.** Hatua iliyofikiwa imeonesha dhahiri juhudi na usimamizi mzuri wa viongozi wetu. Aidha, mafanikio haya yamefikiwa baada ya serikali kuzipatia taasisi zake mgao mzuri wa fedha za Matumizi ya Kazi za Maendeleo kiasilimia ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo utoaji wa fedha za matumizi ya maendeleo ulikuwa mdogo katika taasisi za serikali.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Kamati hii inaipongeza serikali kwa kuziingizia fedha Taasisi za Serikali za Pemba moja kwa moja kwenye akauti

zao. Jambo hili pia, limesaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi za taasisi hizo. Kamati yetu imefarajika na hili kwani linazidi kudhihirisha wazi kuwa Serikali ya Mapinduzi – Zanzibar inathamini maoni na michango inayotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili.

Mhe. Spika**,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati hii inaishauri serikali kupitia Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato – Zanzibar kuzidisha mkakati wa kukusanya na kukabidhi mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali vya mapato ili bajeti iweze kutekelezeka. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuchukua juhudi za makusudi na kuhakikisha kuwa Wafanyabiashara wote wanatoa stakabadhi ya malipo kwa wanunuzi wa bidhaa zao. Kwani imegundulika kuwa asilimia kubwa ya Wafanyabiashara hawatoi stakabadhi ya malipo wanapouza bidhaa au wanapotoa huduma mbali mbali kwa Wateja wao. Jambo hili linaashiria kuwa asilimia kubwa ya Wananchi hawaelewi umuhimu wa kuwa na stakabadhi ya malipo.

Hivyo, Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato inashauriwa na Kamati hii kuzidi kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa kudai stakabadhi. Hii ni kutokana na kuwa stakabadhi hutoa uhalali wa kitu kwa mmiliki, pia, humsaidia mfanyabiashara kujua idadi na thamani ya bidhaa alizouza kwa siku husika, humsaidia muuzaji kuweka kumbukumbu, kielelezo kinachoonesha kwamba muuzaji na mnunuaji amechangia pato la Taifa pamoja na sababu nyingi nyenginezo.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Kamati ya Wenyeviti imegundua kuwa baadhi ya wafanyabiashara hawajasajili biashara zao. Hivyo, ni vyema Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato – Zanzibar ikawachukulia hatua wale wote ambao hawajasajili biashara zao kama Sheria za Nchi zinavyoelekeza. Aidha, tunaishauri Mamlaka hii kufanya utafiti wa kina juu ya wlipa kodi ili nchi iweze kujua idadi halisi ya walipa kodi waliopo, na aina za kodi wanazopaswa kulipa kama nchi nyengine zinavyofanya.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mapato ya nchi, kamati yetu inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa wakandarasi wote wakiwemo wakandarasi kutoka nje ya nchi wanasajili shughuli zao kama Sheria Nam. 5/2008 ya Kusajili Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo *(The Architects, Engineers and Quantity Surveyor's Registration Act),* Sheria Nam. 6/2008 ya Sheria ya Kusajili Wakandarasi na Kuanzisha Bodi itakayoratibu shughuli za wakandarasi (*The Contractor Registration Act*) na Sheria Nam. 14/2008 ya Kodi ya Majengo (*The Property Tax Act)* zinavyoelekeza. Aidha, kamati yetu imegundua kuwa baadhi ya makampuni huchukua washauri elekezi (*consultant*) kutoka nje ya Zanzibar, jambo hili hulikosesha mapato nchi yetu pamoja na kuwafanya wataalamu wetu wakose shughuli za kufanya. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar

inao wataalamu wa kushughulikia masuala haya, kamati yetu inashauri kuwa ni vyema washauri hawa wakatoka Zanzibar.

Mhe. Spika, sambamba na hayo Kamati ya Wenyeviti inaishauri Serikali kutunga Kanuni za Sheria nilizozitaja hapo awali, ili ufanisi wa sheria hizo upatikane haraka. Aidha, kamati inashauri kuwa endapo mwananchi anataka kujenga basi aoneshe gharama halisi za jengo, ili serikali iweze kumtoza kodi inayoendana na gharama halisi za jengo.

BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amewasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inayotarajiwa kuimarisha zaidi hali ya uchumi, kwani ametueleza kuwa pato la taifa linatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 6.7 kwa mwaka 2009 hadi asilimia 7.3 kwa mwaka 2010. Aidha, kiwango cha mfumko wa bei kinatarajiwa kushuka kutoka asilimia 8.9 kwa mwaka 2009 hadi asilimia 7.8 kwa mwaka 2010. Bajeti hii imelenga kufanikisha haya kwa kuenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) awamu ya pili, Malengo ya Milenia ya 2015 pamoja na Mageuzi ya Msingi.

Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia njema kwa wananchi wake. Hata hivyo, inaishauri Serikali kuyatekeleza haya kwa vitendo na sio kuyabakisha kwenye vitabu bila ya utekelezaji.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amevieleza viashiria vya uchumi vinavyotarajiwa kukuza uchumi wetu kwa mwaka wa fedha ujao. Miongoni mwa viashiria hivyo ni pamoja na kuongezeka kwa wawekezaji na idadi ya watalii baada ya kupatikana kwa umeme wa uhakika katika Kisiwa cha Pemba. Kutokana na kukamilika kwa uwekaji waya wa umeme wa chini ya bahari wa Tanga – Pemba, pamoja na kupungua kwa athari za msukosuko wa uchumi duniani. Mhe. Spika, kuyafanikisha haya kamati yetu inashauri kuimarishwa ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali kwa maendeleo ya nchi. Kwani imebainika kuwa kuna pengo la ushirikiano wa kutosha baina ya taasisi za serikali na wadau katika mambo ya uwekezaji.

Mhe. Spika, mara kadhaa Idara ya Uhamiaji Zanzibar, pamoja na taratibu zetu za sheria zilizopo inaweza ama kufuta au kutokutoa kibali cha kazi kwa wawekezaji bila ya sababu ya msingi ingawa *ZIPA* na Kamisheni ya Kazi zimeeleza vya kutosha juu ya umuhimu wa wafanyakazi hao kuwepo Zanzibar kama wataalamu. Hivyo, kutokana na kasoro hizo kamati inaiomba idara hii kuwa makini wakati inapofanya maamuzi kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla. Mhe. Spika, juu ya suala hili kamati yetu

inashauri kuwa endapo mtu atawekeza ndani ya nchi, mbali ya nchi yetu kupata mapato, lakini pia, wananchi wetu hupata ajira, kwani sheria zetu zinaelekeza kuwa baadhi ya kazi ni lazima zitekelezwe na wazalendo. Aidha, nchi yetu itajenga mashirikiano mazuri na nchi nyengine, sambamba na kujulikana zaidi duniani.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo kwa mwaka 2009 imechangia asilimia 30.8 katika pato la taifa ikilinganishwa na asilimia 30.7 kwa mwaka 2008 kama hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi alivyobainisha kwenye ukurasa wa 28. Kwa kuzingatia kauli mbiu ya bajeti ya mwaka 2009/2010 ongezeko hili ni dogo sana. Hivyo, Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, inaishauri Serikali kuitengea fedha za kutosha Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, ili kauli mbiu ya Serikali za kuipa kipaumbele sekta ya kilimo ziendane na vitendo. Aidha, kamati inashauri kilimo cha mazao ya viungo kiimarishwe zaidi kwa kuwa soko lake ni zuri pamoja na kuimarishwa mazao ya biashara kama vile, karafuu kama nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilivyoshauri.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametamka kwamba Bajeti ya mwaka 2010/2011 itakuwa ni “Bajeti ya Demokrasia na Maendeleo”. Hivyo basi, kamati yetu inaiomba serikali kutoa msisitizo zaidi katika kuimarisha utawala bora na demokrasia ndani na nje ya nchi.
Mhe. Spika, katika mwaka ujao wa fedha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuchukua juhudi kubwa zaidi katika kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato nchini na kupendekeza baadhi ya hatua inazokusudia kuchukuliwa. Kamati ya Wenyeviti inaunga mkono juhudi zitakazochukuliwa na katika kufanikisha jambo hilo kamati inaiomba serikali kuyafanyia kazi mapendekezo ya kamati hii niliyoyatoa wakati nilipokuwa ninaelezea “Utekelezaji Wa Bajeti Kwa Mwaka Wa Fedha 2009/2010”.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 92 ametueleza kuwa katika mwaka ujao wa fedha Serikali inakusudia kufuatilia matumizi ya misamaha ya kodi. Ili kuhakikisha kuwa misamaha inayotolewa inatumika ilivyokusudiwa, kamati inashauri kuwa ufatiliaji zoezi hilo lianze mara moja na lifanywe kwa kina na kitaalamu kwani kuna hisia kwamba asilimia kubwa ya vitu vinavyotolewa misamaha huwa havitumiki kwa maendeleo ya jamii. Kwa lugha nyengine tunaweza kusema kuwa kuna wasiwasi kuwa fursa ya utumiaji wa misamaha ya kodi hutumiwa vibaya na baadhi ya watendaji. Aidha, kamati yetu inashauri Sera ya Misamaha ya Kodi kwa Wawekezaji Binafsi ifanyiwe mapitio ili irekebishwe kwani, kwa ilivyo sasa sera hiyo inawanufaisha zaidi wawekezaji kuliko Serikali.

Mhe. Spika, tumeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 ukuaji wa uzalishaji viwandani umepanda kutoka asilimia 1.1 kwa mwaka 2008 na kufikia asilimia 2.4 kwa mwaka 2009. Mhe. Spika, bado kasi hii ya ukuaji wa uzalishaji wa viwanda ni ndogo. Hivyo, kamati yetu inaishauri Serikali kuimarisha sekta ya viwanda ili sekta ya uzalishaji ipate uhai zaidi. Sekta hii haina budi kupewa kipaumbele na kuwekewa mikakati ya kuikuza, badala ya kuiacha ikue wenyewe, jambo ambalo litachukua muda mrefu sana. Sera zetu za kiuchumi ni lazima ziweke mazingira mazuri ili kuvutia uwekezaji katika viwanda. Pamoja na kuweka vivutio maalum vya kisera, kuwe na msisitizo maalum wa kuimarisha miundombinu, hasa upatikanaji wa maji na umeme wa uhakika. Aidha, tunaweza kuwashawishi wafanyabiashara wakubwa wa ndani wawekeze katika viwanda. Katika eneo hili kamati inashauri kwa mara nyingine na kwa msisitizo kuwa ni vyema Wafanyabiashara wa Zanzibar wabadilike; wawekeze katika viwanda ili wazalishe na kusafirisha bidhaa nje badala ya kuagiza tu kutoka nchi za nje.

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri amebainisha mipango mbali mbali ya maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Katika kuleta maendeleo ya nchi Serikali inatarajia kutumia Tsh. 251,204 milioni ambapo, Tsh. 39,490 milioni (asilimia 15.7) zinatarajiwa kutolewa na Serikali na Tsh. 211,714 milioni sawa na asilimia 84.3 zinatarajiwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha zinazotarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Tsh. 78,922 milioni ni Ruzuku na Tsh. 132,792 milioni ni mikopo. Mhe. Spika, Kamati yetu haina pingamizi na mipango hiyo. Hata hivyo, inashauri vifaa na misaada tunayopewa na Washirika wa Maendeleo na vile vifaa tunavyonunua kutokana na fedha za ndani vitunzwe ipasavyo, ili kuthamini juhudi za wale wanaotusaidia pamoja na kuzitumia ipasavyo pesa za walipa kodi wa nchi hii. Sambamba na hayo, Serikali tunaishauri kutekeleza kwa vitendo na kwa wakati ahadi (*commitment*) zake katika mambo ambayo tunapata msaada kwa washirika hao.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika ukurasa wa 83 wa hotuba yake ametueleza kuwa Serikali inakusudia kuwasilisha mbele ya Baraza hili Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Rasmi Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*Constituence Development Fund – CDF*) katika mwaka ujao wa fedha. Kamati yetu inaunga mkono suala hili, hata hivyo, inaiomba Serikali kuchukua juhudi za makusudi na kuhakikisha kuwa suala hili linatekelezwa mapema iwezekanavyo kwani limechukua muda mrefu kukamilika. Kwa kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo huharakisha maendeleo ya wananchi majimboni Kamati inashauri kuwa fedha ambazo zimetengwa kwa Miradi ya Wananchi zitumike kwa ajili hiyo, kwa kuanzia.

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ahadi iliyoitoa ya kuwaongezea mishahara wafanyakazi wa serikali na kufanya kima cha chini cha mshahara kufikia Tsh. 100,000/-, ingawa kiwango hiki bado hakikidhi mahitaji halisi ya maisha kwa mwezi. Pamoja na pongezi hizo, kamati hii inaishauri Serikali kuwakumbuka wafanyakazi wake mara kwa mara, na vile vile kuifanyia mapitio mishahara ya Vikosi vya SMZ kwani umepita muda mrefu sasa Serikali haijaongeza mishahara ya watumishi hao wa umma.

MSAADA WA KIBAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza kuwa katika mwaka ujao wa fedha Washirika wa Maendeleo wanakusudia kupunguza msaada wa kibajeti kwa Tanzania kutokana na sababu mbali mbali. Hatua hiyo itaipunguzia misaada ya kibajeti Zanzibar kwa karibu Tsh. 18,000 milioni. Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuandaa mikakati maalum ya kukabiliana na hali hiyo. Jambo hilo linanifanya nithubutu kutamka tena kuwa viongozi wetu ni mahiri na wapo makini katika kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata huduma bora na zinazostahiki.

Mhe. Spika, kwa kuwa Tanzania inajumuisha nchi mbili ya Tanzania Bara na ile ya Tanzania Zanzibar, tunawaomba Washirika wa Maendeleo waendelee kuipatia misaada Zanzibar. Hii ni kutokana na kuwa Zanzibar inasifika katika kutumia vyema fedha za msaada.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha maoni ya kamati, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu, na naomba Waheshimiwa Wajumbe wanivumilie kwa hili, na leo Mhe. Spika, nitatoa mchango katika eneo moja tu.

Mhe. Spika, katika hotuba ya Bajeti iliyosomwa na Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 38 paragraph ya pili (2) mstari wa mwisho imetajwa Barabara ya Pale Kiongele kuwa ni miongoni mwa barabara inayoendelea kufanyiwa matengenezo. Hivyo, naiomba Serikali kupitia Mfuko wa Barabara kuipatia fedha Wizara ya Mawasiliano ili iweze kutekeleza lengo hilo kama ilivyokusudiwa. Ili wananchi wangu wa Shehia ya Pale na Kiongele na wao waondokane na usumbufu wanaoendelea kuupata. Kwa maana hiyo basi, Mhe. Waziri niko tayari kukusikiliza kwa makini wakati wa kufanya majumuisho juu ya Barabara hii na mimi nataka nikualike kama ulivyonialika wewe siku ya uzinduzi wa Barabara ya Mazizini - Fumba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba uniruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini na pia nikushukuru

wewe kwa mara ya pili kwa kuniruhusu kutumia muda mrefu kiasi katika kuwasilisha maoni ya kamati yangu pamoja na ya jimbo langu.

Mhe. Spika, napenda kutamka tena kwa niaba ya Kamati yangu na Jimbo langu kwamba ninaiunga mkono Bajeti hii Kuu ya Serikali ya mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, *alhamdullilahi* – naanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima na kuniwezesha kusimama mbele yako kuelezea machache kuhusiana na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/11.

Mhe. Spika, naomba pia upokee pongezi zangu kwa kuniruhusu kuzungumza katika Baraza lako tukufu, na aidha nataka ruhusa ya kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu kwao, heshima na imani wanayonipa ni changamoto kubwa katika kuzidisha ari ya kuwatumikia kwa unyenyekevu sana.

Mhe. Spika, juzi tarehe 09/06/2010, Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame alisoma hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 20/10/11.

Hii ni Bajeti ya kumi katika awamu ya sita inayoongozwa na CCM, na katika enzi hii ya maridhiano nitajitahidi sana kuepuka vionjo katika uchangiaji, kwa nia ya kutoa picha halisi ya maoni yetu, nawashauri wengine nao wachangie kwa kuonyesha njia ya matumaini kwa chi yetu.

Mhe. Waziri amejitahidi kutushawishi kwamba Bajeti hii na zile zilizopita zimetekeleza ahadi za Ilani ya CCM ya kupunguza umasikini na kuyafanya maisha bora ya Mzanzibari yawe mazuri zaidi kila miaka ilivyopita. Je, kuna ukweli wowote juu ya upatikanaji wa maisha bora kwa Mzanzibari, je, MKUZA umesaidiaje kumuezesha Mzanzibari kuongeza uwezo wake wa kununua na kuweka akiba.

Mhe. Spika, katika hotuba ya bajeti ya mwaka huu, Serikali imetuelezea kwamba nchi yetu imepata mafanikio makubwa. Kwa mfano.

- Kumekuwa na ongezeko la uimarikaji wa miundo mbinu.
- Kuanzishwa kwa Skuli za Wakulima
- Kuanzishwa kwa miundombinu ya mabonde ya umwagiliaji maji.
- Kununuliwa mtambo mpya wa *"Liquid nitrogen*."

- Kutoa vifaa na maboti ya uvuvi ingawa hazikuelezwa ni ngapi na zimetolewa wapi
- Kutembelewa na watalii 134,954.
- Kuwepo hoteli 23 zenye hadhi ya nyota 4 na 5.

Mhe. Spika, katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana tulielezwa kwamba Bajeti ya miundombinu itakayoimarisha Kilimo na Utalii . Ni vyema waziri akaelieza Baraza lako kwa mifano halisi mafanikio ya kilichopatikana. Haitoshi hata kidogo kutoa maelezo ya jumla pekee. Ni vizuri sana kama :

- Akatueleza kwamba uanzishwaji wa Skuli za Wakulima umetoa tofauti gani ya uzalishaji kwa mlinganisho wa miaka mitano nyuma, au
- Uanzishwaji wa miundo mbinu ya mabonde ya umwagiliaji, matrekta 45 na mbegu za aina 100 zimeongeza vipi uzalishaji wa mchele katika nchi yetu na kwa kiasi gani umepunguza uagiziaji wa mchele kutoka nje, na kwa kiasi gani umepunguza mfumuko wa bei.
- Atueleze kwamba utolewaji wa vifaa na maboti ya uvuvi, umeongeza vipi upatikanaji wa samaki, na ulipunguzaje bei ya samaki kwa mlaji, au uliongezaje kipato cha mvuvi na hivyo kuchangia kupunguza umasikini wa kipato kwa wavuvi wetu.

Mhe. Spika, Kwa bahati mbaya sana, jawabu za masuala yetu hayo hayamo katika hotuba hii ya Waziri.maana hata kule kushuka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka 2009 na kufikia 8.9% ikilinganishwa na 20.6% ya mwaka 2008 hakukutokana na juhudi zetu za ndani isipokua imeelezwa na waziri mwenyewe kwamba kumetokana na kushuka bei ya mchele na kushuka kwa bei ya mafuta duniani na kamwe siyo uzalishaji wetu wa ndani.

Mhe. Spika, pamoja na kukubalika sababu hizo katika nadharia ya kiuchumi, lakini kwa muktadha wa ustawi wa nchi husika sababu hizo za kupungua kwa mfumuko wa bei ni tete (*fragile*) kwani hazitokani na juhudi za uimarikaji wa uchumi wetu. Ingalikuwa ni jambo la kujivunia sana, kama upunguaji wa bei za vyakula ungesababishwa na uongezekaji wa uzalishaji wa chakula ndani na hivyo kupunguza uagiziaji wa chakula kutoka nje, na upunguaji wa bei ya mafuta ungechangiwa na uzalishaji na uchimbaji wa mafuta ndani, na hivyo kupunguza uagizaji na bei ya mafuta ya nje.

Mhe. Spika, bahati mbaya ni kwamba mipango katika bajeti hii tunayoijadili ya kurekebisha kasoro hizo imekosekana. Katika Bajeti ya mwaka huu kumetajwa misamaha ya nafuu ya uwekezaji katika kilimo jee mkulima wa ndizi ya Gando na yule wa tungule wa Matemwe watafaidikaje na misamaha hiyo.

Juzi nilitembelea Soko Kuu la Mwanakwerekwe na kugundua asilimia zaidi ya 70 ya bidhaa zinazouzwa hazitokani na uzalishaji wa wakulima wa Zanzibar. Leo wakulima wa nje ya Zanzibar ndio wanaofaidika na soko la mahoteli ya Utalii Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe.Waziri, anazungumzia suala la urari wa biashara katika Zanzibar na nchi za nje ambapo analalamika juu kupungua usafirishaji bidhaa nje kwa 1.5% ya usafirishaji wa mwaka jana, uliosababishwa na upungufu wa usafirishaji wa mazao ya asili ya karafuu na mwani.

Kambi ya Upinzani imekatishwa tamaa zaidi kwa kukosekana kwa mipango ya kibajeti katika kuimarisha uzalishaji wa karafuu na mwani ambayo ndiyo mazao yetu ya asili ya kutupatia fedha za kigeni. Huaje zao kuu la kitaifa ambalo ndiyo tegemeo letu la kusaidia kupata fedha za kigeni litengewe Sh. milioni 80 Serikali haikuweka mipango yeyote ya muda mfupi au ya muda mrefu kurekebisha hali hii ya mazoa yetu ya biashara.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka jana, Serikali ilipanga kutumia Sh. Milioni 60 tu kuendeleza zao hili nazo hazikupatika zote maana ni sh.50 milioni tu ndizo zilitolewa kwa mradi huu. Hakuna maelezo yeyote juu ya kuendeleza zao la mwani, na badala yake katika bajeti hii, Serikali imetenga Shs. milioni 650 kwa mradi wa mboga mboga, kama inavyoonekana katika kiambatanisho N0.2 ukurasa 86/87 Kitabu cha pili. Nasikitika kusema kwamba hii ni dhihaka katika mipango ya uchumi ambayo kamwe haiwezi kutukwamua . Mboga hizi zinauzwa wapi na ni vipi mboga hizi zinasaidia kupunguza urari wa biashara za nje?

Mhe Spika, sote tunaelewa kwamba pamoja na kuifanya sekta ya kitalii kua ni sekta kiongozi , lakini azimio la Maputo la nchi za *SADC* limezitaka serikali za Afrika kutoa kipa umbele kwa sekta ya kilimo na kuagiza ipangiwe bajeti isiyopungua asilimia 10 kwa mwaka. Kwa miaka mitano iliyopita sekta ya kilimo haijawahi kupewa zaidi ya asilimia 6. Ukichanganya na hali ya mfumuko wa bei za miaka husika na ongezeko la watu ambalo linakua kwa asilimai 3.1 kwa mwaka, bajeti ndogo ya kilimo inayotengwa, haiwezi kusaidia uzalishaji wa chakula au kuimarisha zao la karafuu na kututoa katika dimbwi la umasikini. Mhe. Spika mwaka huu kilimo kimepangiwa asilimia 6.15 tu.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani imepokea kwa faraja habari njema kwamba huduma ya Sekta ya Fedha imekuwa ikikua kwa hatua ya matumaini, lakini linalotia mashaka ni kwamba kati ya mikopo yenye thamani ya Shs. 85 bilioni ilitolewa kutoka mabenki mbali mbali, iliyotolewa kwa ajili ya shughuli za kilimo ni asilimia moja tu, na hapakutolewa taarifa kama kuna asilimia yeyote iliyokwenda kwenye sekta ya uvuvi.

Nani ataamini kwa sera hizi kweli tuna dhamira ya kujiokoa kiuchumi huku tukielewa kwamba kwa Zanzibar, kama vile walivyo wenzetu Bara na migodi ya dhahabu, kwetu sisi Bahari ndiyo mgodi pekee wa kuutegemea kutuletea mabadiliko ya uchumi wetu na kutuondoa katika hali tuliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, ni vyema tukajifunza kwa nchi ndogo ya kisiwa cha Singapore, ambayo ni ndogo karibu mara 2 ya kisiwa cha Pemba, ambacho hakina madini wala mafuta, kina wakaazi zaidi ya milioni 5, kilichokuwa na muungano wa nchi ya Malaysia, ambao ulikatika baada ya kuona matumizi ya "*Soverenity*" moja haikuwa na mchango katika uchumi wao . Pamoja na udogo wa kisiwa cha Singapore kwa maamuzi yao ya kisera ya kuekeza kwenye uzalishaji viwandani na elimu, leo ni miongoni mwa nchi tajiri duniani ikiwa ni nchi ya tisa duniani kwa akiba kubwa ya fedha za kigeni. Sisi Zanzibar hadi leo hatujafanya maamuzi ya wapi tuelekee. Je, ni viwanda, uvuvi,utalii au kilimo cha mboga?

BAJETI NA JINSIA

Mhe. Spika, udhaifu mkubwa wa bajeti hii tunayochangia, haikuzingatia hali ya mwanamke wa Kizanzibari na maandalizi yake hayakulenga kumuondolea mzigo wa unyonge na umaskini uliokithiri.

Bila ya kuchukua hatua madhubuti za kibajeti zinazomuimarisha mwanamke wa Kizanzibari kushiriki katika uzalishaji na kufaidi matunda ya uzalishaji huo, na kupata upendeleo unaostahiki katika kumiliki mali, kumiliki ardhi, fursa za elimu ya juu, fursa za matibabu, fursa za ajira , vyeo na fursa za maamuzi, bado hali ya maisha ya familia za wazanzibari zitakumbwa na unyonge na umaskini.

Mhe. Spika, tafiti zinaonesha kwamba bajeti isiyompendelea mwanamke inapunguza uzalishaji wa kilimo, inapunguza uzalishaji wa jumla katika nchi na hudumaza maendeleo katika nchi.

Tafiti zinaonesha pia kwamba bajeti zisizomlenga mwanamke, hupunguza kiwango cha elimu cha watoto, huduma za afya ya mama na mtoto, hupunguza pato la taifa katika nchi na hudumaza maendeleo katika nchi.

Tafiti pia zinaonesha bajeti zisizomlenga mwanamke hupunguza nafasi za wanawake katika vyuo vikuu, hupunguza fursa za ajira kwa mwanamke, hupunguza *'wage bill'* kwa wanawake na faida nyengine, ambapo hudumaza pato la taifa na hivyo kudumaza maendeleo katika nchi.

Mhe. Spika, katika kuondokana na mafumo mbovu usiozingatia hali ya mwanamke wa Kizanzibari katika bajeti ya nchi, na kwa kuzingatia kwamba tafiti zinazoonesha wanawake wa Zanzibar wanafanya 70% ya wakulima na

wanachangia 70% ya mapato yanayotokana na kilimo, Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

- Sheria na mifumo ya kitaasisi ibadilishwe ili kutoa fursa ya kutosha kwa wanawake wa Kizanzibari.
- Upendeleo wa kibajeti uwekwe ili kuwajengea wanawake wa Kizanzibari uwezo wa kiuchumi na kielimu na kiafya.
- Paanzishwe madawati ya kijinsia katika sekta zote na Wilaya zote Unguja/Pemba.
- Paanzishwe kikundi kazi cha kushughulika na kusimamia uzingatiaji wa kijinsia kibajeti katika mipango, sera na sheria.
- Paongezwe ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi.
- Paanzishwe kitengo cha kutathmini na ufuatiliaji wa masuala ya kijinsia cha Wizara, Mikoa na Wilaya.
- Kisheria, kurekebisha mienendo ya kijamii ambayo inachochea ukandamizaji wa wanawake.

Mhe. Spika, naamini kama serikali itafuata ushauri huu wanawake wa Zanzibar watakuwa ni sehemu ya mazingatio ya bajeti na nchi yetu itapiga hatua ya haraka katika maendeleo.

Bajeti na Washirika wa Maendeleo

Mhe. Spika, serikali imekuwa ikipanga bajeti yake kwa matarajio ya kupata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hili si jambo baya kwa uchumi wa nchi zinazoendelea, lakini kinacholeta masuala ni upatikanaji halisi wa fedha hizo usokuwa mkubwa kama ilivyotarajiwa na hivyo huathiri sana utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo. Mwaka jana wahisani wametupatia kasoro ya asilimia 50% ya matarajio yetu.

Jee ni matarajio gani aliyonayo waziri kwamba pamoja na udhaifu huo, bado Mhe. Waziri katika mwaka unaofuata hupanga matumizi ya fedha nyingi zaidi kutoka washirika wa maendeleo ambazo huwa hazipatikani hata nusu yake? Kwa mfano:

Mwaka	**Tulichotarajia**	**Tulichopata**	**Asilimia**
2008/09	bilioni 173.75	bilioni 61.527	32
2009/10	bilioni199.188	bilioni 92.917	46.48
2010/20	bilioni208.407	Matariajio	?

Kama huo ndiyo mwenendo wa upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka nje ni vyema utayarishaji wetu wa bajeti ukapunguza utegemezi huo na hivyo kupanga kwa tahadhari. Hali halisi ya bajeti hii ni kwamba tumeweka matumaini makubwa zaidi kuliko hali halisi ya upatikanaji wake na hivyo tutazorotesha mpango wetu wote wa mapato kwa miradi hiyo na itakwama njiani. Ushahidi ni uamuzi wa wahisani wetu kupunguza msaada wa kibajeti Tanzania kwa kiwango cha shilingi 297 bilioni na kutulazimisha kutafuta mikopo ya ndani kutoka mabenki ya biashara. Inashangaza kwamba mwaka 2010, sisi tumejiwekea kupata shilingi 208.407 bilioni kutoka nje sawa na asilimia 46.6 ya bajeti nzima. Huku si kujidanganya Mhe. Spika?

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu sana la kiuchumi ambalo ilani na sera zinazofuatwa zimetufelisha ni suala la upatikanaji wa ajira kwa watu wetu.
Mhe. Waziri katika ukurasa 35, wa bajeti yake anatueleza kwamba, ajira iliyo rasmi ina wafanyakazi 47,551, kati ya hao 31,378 wako katika sekta ya umma na wengine 10,230 wako katika sekta binafsi, hii inafanya 41,608 ya wafanyakazi wote. Kama hesabu hii ni sahihi basi kuna tofauti ya 5,943 ambao hawajulikani wanafanya kazi wapi. Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kwamba wafanyakazi hawa 5,943 ni wafanyakazi hewa katika serikali ambao hawajulikani wanafanya kazi wapi na pengine kupokea mishahara hewa.

Mhe. Spika, pamoja na wafanyakazi hao 47,551 ambao wameajiriwa rasmi, takwimu zinataja kwamba nguvu kazi ya Zanzibar ina wananchi wasiopungua 500,000. Kwa hesabu hizo wafanyakazi 47,551 katika laki tano ni chini ya 10% tu, na hivyo 90% ya waliobaki ni waganga njaa na wanaoishi maisha ya omba omba, ili kuche nikahangaike jiko lifuke. Mhe. Spika wengine wanaishi maisha ya ndege wanapoamka sipo wanapolala.

Mhe Spika, baya zaidi katika suala hilo la ajira ni kuona hata nafasi chache zilioko kwenye sekta ya utalii, ambayo imeelezwa na waziri kwamba ni sekta kiongozi, wageni tumewaachia kujaza nafasi hizi, huku Wazanzibari wakifaidi athari ya mmong'onyoko wa mazingira ya ardhi, bahari na mmong'onyoko wa utamaduni wetu na maadili mema. Mpango wa kukuza ajira kwa vijana kwa mwaka mzima ulitengewa shilingi 30,000,000/ fedha halisi walizotiliwa ni shilingi 10, 000,000/ tu. Jee, haya ndiyo mafanikio ya ilani tulioambiwa na Mhe. Waziri?

Matokeo ya kukosa ajira ni hali ngumu ya maisha iliyofanya kuomba kuwa ni moja kati ya ajira. Maana yule anayeomba naye huombwa na hivyo hapa kwetu waombaji hukimbiana wenyewe kwa wenyewe. Wengi ya hawa ni vijana waliokosa matumaini na hivyo kujiingiza katika vitendo vya biashara ya madawa ya kulevya na ukahaba. Hawa ni watoto wa wakwezi na wakulima na

babu zao ndio waliofanya mabadiliko ya utawala hapo 1964 kwa matumaini kwamba kizazi hiki kipate maisha bora.

Mara nyingi hotuba za kibajeti hutumia kuongezeka pato la taifa la kila mwananchi kueleza kuongezeka pato la mwananchi. Kwa mujibu wa maelezo ya waziri katika kitabu chake, pato la mwananchi wa Zanzibar limeongezeka kutoka shilingi 748,057 hadi shilingi 878,403. Kama kweli kuna ongezeko hili basi hali ya maisha ya mzanzibari mitaani isingekua ya kuombaomba, ni viashiria gani anavyotumia Mhe. Waziri kupata ongezeko la pato la taifa kila mwaka huku Mzanzibari akionekana kufukarika.

Mhe. Spika fahari si ya matumizi ya wastani kwa mzanzibari (*Comsumer price Index*) iliyopo katika kitabu cha kwanza ukurasa wa 21, inaonesha kwamba katika kila shilingi 100 anazozichuma mwananchi shilingi 57.4 hutumia kwa chakula na hutumia shilingi 15.16 kununua umeme au kuni ili akipike. Kwa hivyo, kwa kila shilingi mia kuna jumla ya shilingi 73 za uchumi wa mnyonge wa barabarani na yule wa afisini hutumia kwa mahitaji ya kula na nishati ili afike kesho. Shilingi 23 tu zilizobaki ndizo analazimika anunue nguo, apate matibabu, apande dalala na akodi chumba na gharama za kusomeshea mtoto.

Mhe. Spika, hali ya maisha ya wazanzibari ilionekana kupozwa kwa maneno matamu ya waziri kwamba, hangeongeza kodi ya bidhaa au huduma yeyote kwa wazanzibari. Maneno haya matamu yameyayuka siku ya pili tu pale Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano aliposoma Bajeti yake na kuamua kupandisha bei ya bidhaa mbali mbali ikiwemo soda. Kambi ya upinzani tunashangaa! Huaje serikali mbili za chama kimojoa Bara na Visiwani wakose kushauriana katika masuala ya kodi kama haya yanayoathiri maisha ya wananchi wa pande zote mbili.

Mhe Spika, baada ya makelele mengi ya *TUCTA* hadi kufika kiwango cha wafanyakazi kutishiwa ili waache kugoma hapo mwezi wa Mei 2010, Serikali ya Muungano imeona ijikoshe kidogo na kuamua kuongeza mshahara wa kima cha chini. Sote tunaelewa kwamba maisha ya Zanzibar kiajira na kimatumizi ni magumu zaidi ya yale ya Bara. Hivyo hoja ya kuongeza mshahara kwa wafanyakazi ni ya msingi. Mhe. Spika katika sura hiyo tungetegemea bajeti hii ione haja ya kuongeza mshahara wa kima cha chini cha wafanyakazi wa serikali na hata wale wa sekta binafsi angalau kufikia 150,000/- kwa mwezi.

Ukosefu wa Nishati

Mhe. Spika, katika maelezo ya Mhe. Waziri uk. 38 – 42 kuhusiana na nishati na mikakati yake ameigawa mafungu matatu, mikakati ya muda mfupi ya kati na ya muda mrefu.

- Mpango wa muda mfupi ni kutengeza maharibiko ya umeme wa chini ya bahari kutoka Dar Es Salaam hadi Fumba .
- Mpango wa muda wa kati ni upatikanji wa umeme wa akiba kwa kununua majenereta 32 mapya
- Mpango wa muda mrefu ni kutandika wa wa chini ya bahari mpya kutoka Dar hadi Fumba.

Kambi ya Upinzani imefadhaishwa na mikakati hiyo ya serikali kwa sababu inaonekana haijaona umuhimu wa kutafuta umeme mbadala uliozalishwa ndani. Hakuna jambo baya katika nchi kuliko kutegemea nishati kwa asilimia mia, hii ni hatari sana kiuchumi na kisiasa. Baya zaidi ni kwamba umeme huu kutoka *TANESCO* tunanunua, tunanunua kwa bei ya juu sana, wakati wenzetu Bara wanaununua kwa shilingi 27 kwa *unit* moja, sisi Wazanzibari tunatakiwa tuuziwe shilingi 78 kwa *unit* moja baada ya TANESCO kutupandishia kwa zaidi ya asilimia 168 kwa *unit* moja.

Tunahitaji mipango ya muda mrefu ili kuhakikisha kuwa tuna umeme wa kutosha unatosheleza mahitaji ya Zanzibar ya leo na ile ya miaka ijayo. Hadi sasa serikali haionekani kwamba imejiandaa kwa hilo na hili nalo litaviza maendeleo yetu ya kiuchumi tunakokwenda.

Mhe. Spika, serikali ilionekana kukubaliana na maamuzi ya Baraza lako na uamuzi huo kuungwa mkono sana na wananchi wa Zanzibar juu ya utafutaji na uchimbaji wa nishati ya mafuta na gesi kama rasilmali ya Zanzibar. Kambi ya upinzani imepata mshangao kwamba katika bajeti hii hakuonekani mipango yoyote ya kibajeti kuhusiana na kutengwa fedha kwa ajili ya kuendeleza shughuli hiyo. Jee, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetishwa, imerudi nyuma na kuwaacha Wazanzibari kwenye mataa, maana nishati hii ni muhimu katika kukwamua uchumi wetu.
Mhe. Spika, nimepokea kwa furaha habari kwamba, sasa Zanzibar nayo itakuwa na taasisi moja tu ya ukusanyaji wa mapato ambayo ni *Zanzibar Revenue Board* ambayo itachukua majukumu ya *TRA.* Hili ni hitaji la Wazanzibari kwa muda mrefu na hapana shaka itaongeza ufanisi katika utawala wa kodi (*Tax regime*) hapa Zanzibar. Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri, kwa kuzingatia hali ya uchumi wa Zanzibar ingekua jambo la maana kama serikali ingepunguza kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) hadi kufikia 15%. Hii ingevutia uwekezaji ambao ungechochea ukusanyaji mkubwa zaidi wa kodi na mapato.

Mahusiano ya Kifedha na Serikali ya Muungano

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani imefurahi kuona kwamba, serikali imeyazingatia yale yote yaliyokuwa yakisemwa kuhusiana na haki za Zanzibar zinazokosekana kwenye uhusiano wa fedha na wenzetu wa Bara, ila bado suala la utaratibu wa kupata mikopo kutoka nje hauko wazi, inaonekana bado kuna vikwazo visivyokuwa vya lazima. Masuala yanayohusu uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi bado umewekewa masharti kwamba lazima SMZ ipitie Serikali ya Jamhuri ya Muuano wa Tanzania. Njia rahisi ni kwamba SMZ iende *BOT* kupeleka maombi yake bila kupitia SMT maana masuala ya mipango ya kibajeti na maendeleo ya kukuza uchumi wa Zanzibar si masuala ya Muungano. Masharti ya kukopa *BOT* yanayotolewa kwa SMZ hayana budi yawe ni masharti kati ya SMZ na Benki, *BOT*.

Mhe. Spika, moja kati ya malalamiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara wa Zanzibar ni kutozwa kodi mara mbili. Pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri, lakini maelezo kwamba *TRA* itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wa *TRA* wanaotumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani za bidhaa ni jambo ambalo limetutia wasiwasi. Jee, maelezo haya yamekuja kwa nia njema au ni kwa sababu tokea Januari mwaka huu protokoli ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki imeanza?

Kumekua na mabishano ya muda mrefu kwa suala hili la Zanzibar kulipwa asilimia 4.5 ya misaada na mikopo ya kusaidia bajeti za serikali. Kambi ya upinzani inaamini kwamba kiwango hiki kiliamuliwa ili kuziba kelele za muda mrefu, lakini hakikua kwa maelewano baada ya kujengewa hoja kitaalam. Zanzibar inaamini kwamba ingestahiki kupata asilimia kubwa zaidi ya hapa. Wakati waziri katika kitabu chake ukurasa wa 78 analieleza baraza lako kwamba, suala hili litafikishwa kwa viongozi si zaidi ya tarehe 24/06/2010, kuna tetesi kwamba ati wenzetu wanaliundia Tume kulishughulikia.

Kuhusu kima halisi ni kwamba Zanzibar mwaka jana kimepata shilingi 50 bilioni tu, kama ndiyo stahiki yake. Lakini kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa fedha wa Muungano Ibara Na 22. inaeleza kwamba fungu la *Budget Support* na Misaada na Mikopo ya Kibajeti zilipatikana jumla ya trilioni 2, bilioni 379,559milioni ambayo asilimia 4.5 ya kima hiki ni shilingi 107 bilioni na wala sio bilioni 50 tulizopewa. Mhe, Waziri hana budi kulieleza Baraza hili kuhusiana na utata huu.

Mhe. Spika, kuhusiana na mfuko wa pamoja wa Fedha, wengi ya Wazanzibari wanamini kwamba mfumo uliopo unaunufaisha zaidi upande wa SMT ambapo mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vianzio vya Muungano huendeshea shughuli zisizo za Muungano kwa upande wa Tanganyika kwa miaka kadhaa.

Kutokuwepo kwa utayari wa kulijadili suala hili ni sababu tosha ya kujenga imani hiyo. Juhudi nyingi zimefanywa na hata ripoti yenye ya mapendekezo ya kulimaliza suala hili zimeshafikishwa serikalini, bado wenzetu wanaliahirisha ili waendelee kuvuna uhondo nyuma ya mgongo wa Muungano. Kuna habari kwamba nalo hili linaundiwa Tume.

Mhe. Spika, kuhusiana na utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu ni kwamba:
Kambi ya upinzani inaomba kueleza kwamba, mapato yetu yanaweza kuongezeka maradufu kama tungewekeza katika sekta za uzalishaji ili tupate bidhaa na tutumie na kuuza na kutumia vyema fursa ya soko kubwa la Afrika Mashariki. Sambamba na hilo, jitihada ifanywe ili Zanzibar ipate fursa maalum katika shughuli za biashara na kodi katika nchi za Afrika Mashariki(*Special Economic zone*) katika Afrika Mashariki. Hatuna budi kukumbusha kwamba, ili tuweze kukabili ushindani wa ajira katika soko hili mipango yetu ya elimu ilenge kutoa elimu yenye kiwango cha juu.

Kwa upande wa matumizi ya kawaida kambi ya upinzani inapenda kutoa ushauri ufuatao:

- Tupunguze matumizi katika maeneo yasiyo ya lazima na kuzipeleka katika sekta za uzalishaji. Tuepuke kutumia fedha zetu chache katika miradi au maeneo yaliyokua ya lazima. Matumizi haya ndiyo yanatulazimisha tuwe na bajeti yenye nakisi isiyokua ya lazima. Kwa mfano, huaje Afisi ya Mkurugenzi wa Vitambulisho katika kifungu chake cha takrima, ikatengewa shilingi 243,000,000 kwa mwaka, matumizi ya takrima ni matumizi ya chai, soda na orojo afisini tu, katika siku 360 za mwaka ukitoa Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu zimebakia siku 243.

Kwa maana nyengine ni kwamba, Afisi ya Vitambulisho kwa matumizi ya soda, chai na urojo inatumia shilingi milioni moja kwa siku (1,000,000). Wakati Afisi hii inatengewa fedha nyingi kiasi hicho za kuharibu, Idara ya Sekandari ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa matumizi yake yote kwa Pemba na Unguja imetengewa shilingi 160,000,000 tu. Au huwaje kwa Idara ya Kinga ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Pemba na Unguja kwa shughuli zake zote, ikatengewa shilingi 150,000,000 tu kwa mwaka mzima, huku Afisi ya Vitambulisho kwa matumizi ya urojo tu ikatengewa shilingi 243,000,000 kwa mwaka.
Mhe. Spika, matumizi ya aina hii kwa kweli ni kasoro kubwa katika bajeti yetu.

Mfano mwengine ni Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kutengewa karibu shilingi 25 bilioni, wakati Kamisheni ya Utalii ambayo

ina jukumu la kuutangaza utalii wetu Zanzibar ya nchi umetengewa shilingi 737 milioni kasoro ya bilioni moja.

- Mhe. Spika, hakuna hata mradi mmoja wa sekta ya uvuvi ulioekezwa wakati tumeeleza kwamba bahari ndiyo mgodi wetu wa Zanzibar. Mkurugenzi wa uvuvi alikuja hapa Barazani ametueleza kwamba hatujaweza kutumia hata zile maili 12 za ukanda wa bahari achilia maili 200 za kanda kuu.

Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

Mhe. Spika, jukumu la Baraza la kutunga sheria ni pamoja na kusimamia serikali (*oversight role*). Serikali nyingi hutamani katika nchi zao kuweko na Bunge au Baraza dhaifu ili lisiweze kusimamiwa ipasavyo. Moja katika mbinu zinazotumiwa na serikali hizo ni kunyima Mabunge/Mabaraza uwezo wa kifedha wa kutekeleza majukumu yao ya kiusimamizi.
Mhe. Spika, katika kuondokana na kabari hiyo, Bunge na Baraza hulazimisha serikali kuanzisha mfuko wa kibunge (*Parliamentary Fund*) unaoweka fedha kutoka kwenye hazina ya nchi kwa asilimia ya mapato yanayopatikana na pia kupitia wafadhili mbali mbali.

Mhe. Spika, Mabunge/Mabaraza mengi katika nchi za Afrika duniani zimeanzisha mfuko wa aina hii, na kwa hakika kasi ya usimamizi wa serikali umepata ufanisi wa heshima. Kwa bahati mbaya sana Baraza hili tukufu halijaanzisha mfuko wa aina hii, Bunge la Jamhuri wao wameanzisha zamani sasa na kweli sasa limekuwa Bunge lenye meno.
Mhe. Spika, kukosekana kwa mfuko huu hapa Zanzibar unalidhalilisha Baraza hili, unalidunisha Baraza hili, unazorotesha heshima ya mamlaka ya Baraza hili kwa umma na pia linadogosha enzi ya kiti chako.
Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Baraza lako, inaitaka serikali kuanzisha mfuko huu wa Baraza la Wawakilishi, ambao utiaji wake wa fedha utakua kwa utaratibu kama ambavyo Mabunge na Mabaraza mengine yanafanya katika nchi zao.

Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu 2010

Mhe. Spika, huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu kwa mujibu wa Katiba iliopo, utaotanguliwa na kura ya maoni hapo tarehe 31/07/2010. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wa Zanzibar katika kura ya maoni watafanya maamuzi yao kuelekea umoja, mshikamano, amani na maendeleo ya kweli ya visiwa vyetu. Ni matumaini yangu kuwa Tume ya Uchaguzi safari hii wataendesha chaguzi zote mbili za kura ya maoni na ya Uchaguzi Mkuu kwa uadilifu na uwazi, ili kuelekeza nchi yetu pahala penye utulivu na ustawi. Bila amani hakuna

maendeleo, na ni ukweli usioshaka kwamba serikali iliyopatikana kwa vurugu haiwezi kujenga umoj na kama hakuna umoja hakuna manendeleo.

Mhe. Spika, tokea maridhiano ya kisiasa yalipofikiwa baada ya Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt Aman Abeid Karume kuonana na kukubaliana na Katibu Mkuu wa *CUF*- Maalim Seif Sharif, upepo wa utulivu wa kisiasa na mshikamano kwa wananchi na viongozi umeshamiri. Hatua hii ni ya kupongezwa na kuiombea idumu daima milele.

Pamoja na kwamba kila mmoja na chama chake na itikadi yake, lakini kuna jambo moja kubwa na muhimu linalotuunganisha, nalo ni Uzanzibari wetu na mategemeo ya kuishi salama katika nchi yetu. Masikitiko yetu makubwa ni kwamba bado kuna wananchi wengi wenye haki ya kikatiba ya kushiriki katika kura ya maoni na uchaguzi mkuu hawakuandikishwa bila sababu za msingi.

Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunivumilia katika kuwasilisha maoni hayo ya upande wa upinzani na pia namshukuru sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary Kiongozi wa Upinzani kwa miongozo na ushauri alionipa katika kutayarisha na kuwasilisha maoni haya. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza. Kama nilivyoomba mwanzo basi nawaomba waichangie hotuba hii kwa kuonesha njia.

Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Said Ali Mbarouk, Waziri Kivuli, Baraza halina meno, sijui kama ni kibogoyo hayajaota kabisa. Tunaendelea. Sasa ni uchangia wa jumla na tuanze kumsikiliza Mhe. Mkongwe Nassoro Juma na baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Mkongwe Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) na Mtume wake (*S.A.W*) aliyetujaalia kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na salama.

Mhe. Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu mdogo.

Pia nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yeye mwenyewe binafsi pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake. Hotuba yake Mhe. Waziri ilikuwa kubwa na pia wajumbe tulistahamili na kuvumilia.

Mhe. Spika, katika hotuba ya Mhe. Waziri alizungumzia mambo mbali mbali yakiwemo ya uchumi, elimu, kilimo na kadhalika, lakini mimi naanza na hiki kilimo.

Kwanza nazipongeza skuli za maandilizi za wakulima zilizoko vijijini. Mhe. Spika, hivi sasa tayari zimeandaliwa skuli za maandalizi za wakulima zilizoko katika vijiji. Kusema kweli skuli hizi zinatoa matarajio makubwa sana ambayo wenyewe Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira walitegemea yafanikiwe.

Mhe. Spika, skuli hizi zinazalisha mboga mboga na vilimo vya aina mbali mbali. Lakini pia kwa hatua hii waliyoifanya wizara bado haijakidhi haja. Kwa sababu hivi sasa kuna wakulima wengi sana hata hao wa mboga mboga wanashindwa na pahala pa kulimia. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri aongeze juhudi ya kuweka maeneo ili wananchi wengi waweze kupata nafasi ya kulima.

Vile vile nije katika kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Spika, kilimo cha umwagiliaji maji wengi kusema kweli wanafaidika, lakini na wengi hawafaidiki. Kuna baadhi ya wananchi hiki kilimo cha umwagiliaji hata kukijua hawakijui, hata kukiona hawajakiona, kuna wilaya nyengine pia kilimo hiki hakijafika. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri kwa sababu kuna wakulima wengi wanaotaka kulima na hasa wanawake pa kulimia hawana, basi atutafutie pahala ili na sisi wanawake twende tukalime na hizi mbegu walizozizungumza hata juu zinaota na mabondeni pia zinaota.

Mwaka jana alizisema hapa Mhe. Waziri, niliposema mabondeni kwenye unyevu unyevu nilichekwa. Sasa mbegu zile kusema kweli Mhe. Spika, hatujaziona sisi. Kwa hivyo, tunamuomba mwaka huu mbegu hizo za unyevu unyevu za juu azilete huko vijijini ili wanawake na wao wapate kulima.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika Sekta ya Afya kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kamati yetu tulitembelea Hospitali ya Mnazi Mmoja sehemu ya maabara, tulitembea kwa hali na mali, lakini tulifika katika chumba kimoja cha maabara ambacho kazi yake ni kuchunguzwa maradhi.

Mhe. Spika, chumba hicho kwanza madirisha yake ni ya vioo, mlango wake wa vioo na wafanyakazi wake wengi ni wanawake. Halafu vile vipoza hewa kwa bahati mbaya vyote viliharibika na hata kile ambacho Mhe. Waziri anatusifia hapa kipimo cha kupimia kichwa siku ile pia kiliharibika. Sasa wafanyakazi wale kusema kweli walikaa kama wako katika tanuri la mbata, joto ni lao kwa sababu zile mashine wakiziwasha peke yake zinatoka joto huwezi hata kuchungulia kwa lile vuke lake la joto. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali ikiwa vile vipoza hewa havijatengenezwa basi vitengenezwe. Kwa

sababu wale kina mama waliomo mule wanaatilika, au kama vimeshatengenezwa basi hiyo ni faraja kwetu.

Tukija katika Chuo cha Afya Mbweni kwanza tunapongeza kwa sababu kule yamejengwa mabanda mawili ya wanafunzi. Lakini pia Mhe. Spika, tatizo lilioko kule ni uzio, basi tunaomba kuwekwe uzio. Kwa sababu kuna mabweni mengine ya wanawake na wanaweza kuingiliwa na majambazi usiku wakahujumiwa.

Vile vile katika chuo hicho tatizo kubwa lilioko ni gadava. Tuseme unamsomesha mwanafunzi kama mfano wa mwanadamu unapomweka jikoni kupika kama hujamfundisha kuwa mchele unafanywa hivi, unatiwa nazi, unafanywa hivi, hatajua. Sasa huku chuoni tunatoa madaktari wazuri, tuna wanafunzi wazuri, nafikiri mwenyewe Mhe. Waziri asubuhi alipojibu maswali anasema kuwa wanatolewa madaktari pale wamemaliza diploma ya juu, diploma gani sijui, lakini sasa hizi diploma zinakuwa hazina mafunzo mazuri.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri ahangaike juu chini alitafute gadava. Mimi gadava kulieleza vyote sielewi, lakini mwenyewe Mhe. Waziri analijua. Gadava liwekwe pale chuoni ili wale wanafunzi waweze kujisomea wakihitimu wapate kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, gadava kwa hapa Tanzania liko Hospitali ya Muhimbili. Sasa kama wanalitaka, wachukuliwe wanafunzi wapelekwe kule ili wakajifunze. Lakini gharama inakuwa kubwa mno linawashinda. Sasa basi, tuhangaike tutafute letu hapa hapa.

Nikiendelea sasa nije katika Sekta ya Barabara. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na pia watu wanasema, “hayawi hayawi huwa”. Hivi sasa kwetu Bumbwini tunayaona mabuldoza yapo, yameletwa inafika wiki ya pili hii kuhusu ujenzi wa barabara. Lakini Mhe. Spika, sijui kama tunazibwa midomo tu, kwa sababu tangu siku yaliyofika hayajang’oa hata ule mgomba na hii ni wiki ya pili. Sasa migari ile imekaa tu, kwa nini haipitishwi kwenye minazi, migomba ikakatwa katwa ili tukajua kuwa kweli sasa hivi barabara ipo lakini madude hayo Mhe. Spika, yamekaa hii inafika wiki ya pili, madude tunapita tunayatazama sijui maana yake kama ndio tunazibwa midomo tuseme ni kweli, au ndio vipi.

Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali ikiwa ni kweli tumekusudia jambo basi tulione, sio midude imekuja tuiweke itazamwe kama harusi, si vizuri.

Vile vile Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Rais Amani Abeid Karume kwa ile juhudi aliyoifanya ya kuachiwa wasia na baba yake akaweza kuchukua juhudi ya kukamilisha jumla namba 10 la Michenzani.

Mhe. Spika, jumba lile lilikuwa na nyumba nyingi za watu na wengine walikuwa wanasikitika pembeni hatupewi, hatupewi. Lakini Mwenyezi Mungu kaionesha kheri na busara kamtia moyo na imani karudisha lile deni la watu. Kwa hili mimi nampongeza Mhe. Rais kwa uungwana wake kwa jinsi alivyofanya mambo ya busara.

Mhe. Spika, pia nizungumzie kuhusu habari ya maji. Mhe. Spika, zamani tulikuwa na tatizo la maji lakini kwa hivi sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu maji yameenea hasa ulipokuja huu mradi wa AKRA. Mhe. Spika, kila unapopita utaona mabomba ya mabuluu yametandazwa, ile ni mfano mwema na wengine wameshachimba misingi wameshazika mabomba. Sasa kwa vile tunaona Mwenyezi Mungu atatujaalia lile tatizo maji tunaweza kuliondoa.

Mhe. Spika, mimi sina mengi isipokuwa ninatoa nia yangu. Nakuomba radhi Mhe. Spika, unisamehe natangaza nia yangu mimi kipindi hiki sitogombea. Kwa hayo machache Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie, naiunga mkono bajeti hii mia juu ya mia.

Mhe. Spika: Mimi nilikuwa naelewa tu kwamba kuna nia za kugombea, kumbe na kutogombea pia ipo. Tunashukuru sana. *(Kicheko)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha leo hii kuwa nihai na kuweza kupata pumzi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi. Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa kazi nzito sana ya vitabu hivi viwili pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake wote, wametuletea kitabu kizuri, chenye maadili mazuri, chenye hatua za utekelezaji.

Mhe. Spika, pamoja na hayo ningekuomba kidogo kuna kitu ambacho sikukiona kwenye kitabu hiki na mimi nataka nichangie na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope na wao walikuwa wameisikiliza sana hotuba hii, lakini sasa wamekuta na wao wamenisaidia maarifa na mimi leo nimepata nafasi. Mhe. Spika, naomba uniruhusu kidogo niweze kukisema pengine Mhe. Waziri kitamsaidia.

Mhe. Spika, hapo nyuma tarehe kidogo nimezisahau lakini kumbukumbu kwenye *hansard* ipo. Mhe. Spika, wananchi, wawakilishi wao, mawaziri wao na hata Mhe. Rais alitamka tamko hilo, nitalieleza jinsi gani Mhe. Rais alitamka tamko hilo. Mhe. Spika, ni suala la mafuta halimo kwenye hotuba hii.

Mhe. Spika, tulitamka hapa kwa pamoja kabisa pande zote mbili na tukasema mia kwa mia kuwa hili suala liwemo liruhusiwe wananchi wenyewe wa Zanzibar kuweza kuchimba mafuta haya.

Lakini Mhe. Spika, katika vitabu hivi viwili sijaona mikakati ya kuonesha jinsi gani tutaweza kuinua uchumi wetu, jinsi gani wananchi wetu tutaweza kuwatajirisha kutokana na neno la mafuta halikuwemo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alieleza hapo na Mhe. Waziri Kivuli alieleza, lakini mimi nalieleza kwa upana kabisa kwa kuwa ninao muda. Mhe. Spika, hili suala linatusikitisha sana na hasa tukiangalia uchumi wetu wa Zanzibar uko duni sana. Kuna mambo ambayo lazima tunatakiwa tuyatazame yamo ndani miongoni mwetu sisi wenyewe wananchi wa Zanzibar ambayo yanaweza kutuinua basi ndio mambo tunayoyachenga.

Mhe. Spika, mimi nilitegemea kwenye hotuba hii suala la mafuta litapewa kipaumbele kabisa. Nimejitahidi kuangalia vitabu vyote sikuliona, nikachukua miwani kuangalia sikuliona, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope nao waliliangalia hawakuliona. Sasa Mhe. Spika, kwa kweli hili suala tunamuomba Mhe. Waziri ni sababu gani iliyopelekea hata lisitiwe humu.

Mhe. Spika, hii ni moja katika ilani kwa sababu kufanikisha uchumi ndio ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunavyoitangaza. Lakini suala hili kuwa halikutiwa humu sijui kuna tatizo gani. Namuomba Mhe. Waziri aje kutueleza kwa kina kabisa ili turidhike pamoja na wananchi wetu. Pia ili hotuba yake iwe katika *schedule* nzuri kabisa ni vizuri atueleze kwa fasaha sababu iliyopelekea kwa suala hili. Inategemea pengine mpigaji kompyuta kasahau kulitia humu inakuja hiyo, pengine katika ile kuchapisha mashine kufika kifungu kile kimejirusha inakuja hiyo siwezi kukataa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupe fasaha yake nzuri kwa nini suala hili halikuwemo.

Mhe. Spika, maana ya kumshirikisha Mhe. Rais Dk. Amani Abeid Karume ni kwa sababu siku ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar alitamka mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba kunukuu: “Pamoja na hayo kuwa mafuta haya kidogo basi waachiwe Wazanzibari wenyewe”.

Lakini pia haikuonesha dhahiri sauti yake humu, humu mna mambo ambayo Mhe. Rais mwenyewe aliyatamka na aliyafanya. Mhe. Spika, nimsifu sana Mhe. Rais kutuzindulia umeme Pemba juzi *Alhamdulillahi.* Hili ni jambo moja kubwa sana kwa sababu miaka mingi sana Pemba enzi zangu mimi nilipokuwa nikenda tangu mdogo mpaka juzi kushuhudia mwenyewe king'ora kinalia kuashiria umeme unawaka. Hili ni jambo la kushukuru sana.

Mhe. Spika, pamoja na kunivumilia nakushukuru sana sasa naingia katika kuchangia. Mhe. Spika, nipo katika ukurasa wa 23 kifungu cha 38 kuhusu Hospitali ya Rufaa Mnazimmoja. Mhe. Spika, mara nyingi sana naisema rufaa hii ya Hospitali ya Mnazimmoja. Hili jambo silisemi rufaa na nasema kwa huzuni kabisa. Kwa sababu tusitumie neno wakati ndani yake kubovu, tutumie lugha iendane na yale mazingira yenyewe yalivyo. Tunakubaliana nayo kuwa ni hospitali ya rufaa lakini tuingie ndani sasa tuiangalie ni rufaa kweli? Kuna mapungufu makubwa sana ambayo ni muhimu ya kuijenga hospitali iwe na jina la rufaa.

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa hivi vifaa vilivyopatikana, *CT Scan* tulikuwa tuna tabu nayo sana kuipata hapa, lakini *Alhamdulillahi* tunaipata sasa hivi. Hivi juzi tumeambiwa kuna vifaa vyengine vimeshaletwa vya kuchunguzia maradhi ya *goitre* kujua kama una sumu au huna sumu. Naambiwa hapa kitakuwa bei ya chini sana wakati ukenda kuchunguzwa Tanzania Bara sasa hivi ni shilingi 60,000/=. Hilo moja nalishukuru sana. Tuna mwelekeo huo lakini tunakwenda kidogo kidogo sijui kwa sababu gani.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kivuli alisema kuna sehemu nyengine yanakuwa mafungu makubwa, lakini sehemu nyengine tunakuwa hatuzitazami. Siku moja nilizungumza suala mpaka waandishi wa habari wakanifuata, wakaniuliza mheshimiwa kwa nini unasema kuwa sehemu ya kichaa cha mbwa zimeongezwa pesa nyingi milioni mia moja na zaidi, nini fikra zako. Sasa nikisema fikra zangu ndio, ile mwaka hadi mwaka, kuna siku na siku. Hospitali kila siku wagonjwa wanapelekwa lifti mbovu, wazee wanapata tabu, kuna wengine *heavy weight.*

Audhubillahi min dhalika leo mimi nianguke hapa watanibeba watu wataweza? Hawawezi Mhe. Spika, hili suala tulitazame kila leo lifti zinaharibika halafu tunasema rufaa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, twende kwenye chumba cha wagonjwa mahututi, hebu tuangalie ile *ICU* yenyewe ilivyo haiendani na mazingira yanayotakiwa iwe. Mhe. Spika, kuna vitu vingi sana vibovu mle, aircondition hamna kabisa mna yale ma-*propeller*, si tunatia *virus* mle, maana yake yule mgonjwa yuko *serious*

tunamzidishia na matatizo mengine. Haiwi uko mzima inakuletea *flu* seuze yule mgonjwa aliyekuwa *serious*.

Sasa utakuta hamna vile vitu na tunasema ile ni hospitali ya rufaa. Kuna vitu vya kompyuta jina lake nimelisahau ambavyo vinaangalia jinsi gani yule mgonjwa anaendelezwa kupata kutweta. Vitu hivyo zamani vilikuwepo kwenye idara yao ndogo pale wanaangalia jinsi gani ya ule mwenendo wa *pressure*, mzunguko wa damu na kila kitu, lakini leo vyote vile vimekufa hatuoni hilo. Vimebakia vikompyuta vidogo tu mpaka atoke hapa yule muuguzi aende kule akafuatie, akirudi kule anakuta ameshabadilika yule mgonjwa ameshazimia au ameshakufa zamani. Wakati akitazama hapa anajua nini cha kuweza kukimbilia kumsaidia yule mgonjwa japo na Mwenyezi Mungu yupo lakini na sisi tumeambiwa tutafute sababu yake.

Mhe. Spika, halafu isitoshe la uchungu zaidi wataalam wanatukimbia. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa alizungumza neno halafu akasema mengine atanisaidia Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ni kweli. Kwa sababu utakuta leo daktari *senior* kabisa, ana madigrii yake mshahara unalingana na nesi. Mhe. Spika, uchungu atakaa hapa kweli na hii ndio tunaiita rufaa, hawezi kukaa.

Mhe. Spika, hivi karibuni nilimpeleka mgonjwa Dar es Salaam hata kusema hapa aibu na hili naomba nisiliseme. Kumbe wenzetu kule wanapelekeana *message* jinsi ambavyo mshahara anaopewa daktari aliyetoka *fresh* huko Ulaya na kuja pale anaoneshwa mtu, mara hii kaingia daktari fulani ana *PhD* analipwa mshahara laki mbili na nusu. *Message* nimeiona Mhe. Spika, kwa jicho langu hili, nimeoneshwa tazama kitu hicho. Kwa kweli Mhe. Spika, tunaingia aibu kabisa. Tulisema kuwa kila siku tuwe kwenye marekebisho tu, marekebisho haya sasa sijui mpaka lini na hawa wanaondoka.

Mhe. Spika, nina kigezo cha madaktari si chini ya watatu kwa ushahidi hasa wameshatukimbia. Wengine sasa hivi wamekwenda kuchukua mimwenge hapa, mtu mzima atafanya nini atakaa hapa. Ni *specialist* wa mifupa kabisa kishakwenda kuchukua mabegani hapa, hayupo yupo Lugalo kenda kuchukua pesa chungu nzima. Isitoshe Mhe. Spika, wengine sasa hivi tunawapeleka kule Dar es Salaam wanasoma, anatazamwa huyu Juma kabakisha miaka mingapi, mwaka mmoja, anapelekewa fomu ile akiangalia mshahara wake harudi.

Sasa hii hali Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri hebu tuiangalieni jamani. Hospitali yetu ya rufaa tunateketea ma-*specialist* wanaondoka, hawa waliobakia chonde chonde basi tuwakamateni. Kuna mambo mengine hebu tufanye kitu cha haraka haraka cha marekebisho na ndio maana Mhe. Waziri

atalijibia Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Waziri tulitazame hili.

Mhe. Spika, ukenda kwenye mawodi ndio hospitali ya rufaa hiyo kunanuka, hata ile *detol* ya kusafishia kutoa harufu hakuna. Mhe. Spika, tunasema hiki kitu kwa uhakika na kwa kweli inasikitisha. Magodoro ndio yameoza. Hebu tutazame katika mafungu yaliyokuwa si ya muhimu tuyapeleke huko ili twende katika lile lengo hasa la kuonesha kama kweli hii hospitali yetu inaitwa jina hilo la rufaa liende na wakati ambao ni mzuri sana.

Mhe. Spika, naondoka huko naingia ukurasa wa 27. Mhe. Spika, mama yangu ameeeleza suala la kilimo, sisi waheshimiwa wengine tunajikita hasa katika kilimo. Lakini Mhe. Spika, ukiangalia bado serikali hili neno la kilimo imelirembea kabisa ni sawa sawa na kulirembea sehemu ya afya. Nikisema sekta nzima ya afya ni pamoja na hiyo hospitali yenyewe. Sasa hii kilimo Mhe. Spika, ni kweli kila siku tutakaa na umaskini pale pale, lakini nashangaa kwenye data tunaambiwa zinakua. Sasa mimi najiuliza zinakua vipi.

Ukenda *field* huko chini utakuta hakuna vitu ambavyo vya kuonesha ukuaji ule wenyewe. Lakini kwenye kitabu unaambiwa mwaka fulani hadi fulani asilimia fulani imekua, sasa mimi hujiuliza ukuaji huo ukoje. Hebu Mhe. Waziri tufahamishe ukuaji huo unakuwa vipi, wakati sisi tunakwenda kule tunaona *physical* kabisa yale matendo yenyewe. Sasa mimi najiuliza ukuaji kwa hizo tungule tatu labda ndio unaofanya uchumi wetu kukua.

Mhe. Spika, ukisema leo Kinduni tatu, Donge tatu, sita hizo ina maana ndio ukuaji wenyewe basi tunakubaliana na hilo, lakini kama si hivyo sikubaliani na suala hilo la ukuaji. Kwa sababu bado wananchi wanahitaji pamoja na kuwa hizi shule nyingi za taaluma zimeongezeka lakini akiondoka pale hana kitu kutakua nini hapa. Anasomeshwa anaoneshwa jinsi ya upandaji wa ule mche na ardhi fulani inakubalika kwa tunda fulani. Lakini akiondoka pale kesha yule, kama ana vitabu vyake kavitia kwenye *briefcase* mchezo umekwisha, haya kimekua nini pale.

Lakini baada ya taaluma serikali ni lazima kwa makusudi kabisa itenge fungu ambalo linaloonesha kuwa mwanafunzi akiondoka pale anaondoka na mbegu, majembe, mbolea, halikadhalika na mambo mengine. Hapo ndipo tutasema sasa kinakua kwa sababu akiondoka pale anakwenda kufanya kazi moja kwa moja. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tuliangalie suala hili kuwa bado kilimo hatujakipa hasa nguvu tunakizungumza tu kwenye makaratasi.

Mhe. Spika, mama alizungumza hapa suala la mpunga wa umwagiliaji maji. Kama kweli tungekuwa tumekamatana vizuri, tumelichukulia suala vizuri, basi

mimi ningesema hata hii mifumko ya bei isingekuwepo. Lakini linakuja fumko la bei kwa sababu mchele wenyewe uko wapi, hatuna. Leo wananchi wanalia wanakwambia tumechelewa kupanda wengine kwa sababu trekta hakuna. Nimekwenda juzi nimeona utakuta upande mmoja umezaliwa, upande mwengine hakuna kilichozaliwa, tayari mtu analia nguvu zake zimeshapotea.

Sasa leo serikali mtu kama yule sijui tutamtazama vipi. Mhe. Spika, ndio maana nikasema kuwa hebu tukae kikweli kweli tuiinue hasa hii sekta ya kilimo. Tena wataalam wanao wazuri sana tu, lakini wataalam wenyewe wanakwambia mimi kazi yangu kusomesha sio kutafuta nyenzo, kazi yake imekwisha, ni kweli amemaliza pale. Tunakwenda kummaliza yule mkulima anaingia ndani anakwenda kulala karatasi inasema kimekua.

Mhe. Spika, nije kifungu cha 47 nizungumzie masuala ya viwanda. Mhe. Spika, ni kweli tulitembelea na Kamati yangu ya Fedha na Uchumi kuna sehemu tumeona kweli inazalishwa, lakini kuna sehemu nyengine ya kusikitisha, mwekezaji ameweka mitambo yake tayari kwa kufanya kazi. Lakini la kushangaza zaidi *immigration* inazuia, tumekua wapi hapa. Lakini kitu kinachonisikitisha ndani ya kitabu tunaelezwa jinsi ya ukuaji wenyewe, ile asilimia ambayo wale waliokuwa wenzetu nafikiri wanatiwa humu kuonesha kuwa ndio hii asilimia kubwa ya ukuaji wake.

Lakini ukenda kule moja kwa moja unakuta unalia machozi. Kwa sababu kuna viwanda ambavyo tulioneshwa kama vyengine tumefichwa na *ZIPA* watakuwa wameficha wao. Lakini vile walivyotuonesha Mhe. Spika, vinasikitisha. Amezuiliwa *TX* hakuna sababu yoyote, akiuliza *ZIPA* sababu gani hajibiwi, tumeuliza sisi sababu gani hatujibiwi. Halafu leo tunasema sekta ya viwanda imekua. Wanakula hasara wenzetu kabisa.

Kuna kiwanda kimoja ambacho kinatakiwa kauli ya Wizara ya Fedha na Uchumi tu, itoe kauli ile ili kiwanda kile kirejee ili *ZIPA* impe mwekezaji mwengine kianze kufanya kazi. Lakini mpaka leo vijana wanaiba *aluminium* kama hawana akili vizuri, hasara jamani. Tumekwenda kutazama *scrapper* tupu matangi ya mafuta yaliyobakia lakini kwenye kitabu tunasema uchumi unakua.

Mhe. Spika, sasa hili nalo nimuombe Mhe. Waziri aliangalie kwa makini sana, kwa nini *immigration* inazuia utendaji wa serikali kupata mapato yake. Kwa sababu hivyo viwanda si vya kitoto, kuna kiwanda kule kuhusu masuala ya maji *TX* wake kaondoshwa kwa kuwa nini labda kaoa Zanzibar au vipi siwezi kujua.

Mhe. Spika, ukija huyu mwengine Mhindi hajaoa Zanzibar lakini kasimamishwa. Sasa sijui kamati zao zinakuwaje. Mhe. Spika, naomba

nimuulize Mhe. Waziri katika kukubali kuupitisha mradi *immigration* hawamo kwenye kamati. Kama wamo kwenye kamati kwa nini sasa wanafika pahala wanazunguka wale wenzao wanakamati wanakubali halafu wao wanasema sisi hatukubali kutoa kibali. Sasa Mhe. Spika, hebu tuliangalie hili kwa kweli hii hali inasikitisha.

Mhe. Spika, nikija ukurasa wa 30 katika hali nzuri ya hewa ndio hiyo hiyo ninayoizungumzia, tunazungumzia hali ya hewa lakini utakuta hapa mfumko wa bei kwa kweli unasikitisha. Mhe. Spika, juzi nilichukua pembe nikenda nikalila nyumbani, nikalitazama kweli hili pembe. Maana yake si masihara binadamu anaweza akaamka asubuhi akawa hata ile sauti hana kwa jinsi linavyokwaruza, sijui utie nazi ngapi hata likolee lile.

Mhe. Spika, huwa najiuliza huko kwao nje huwa linapanda bei kweli, liko katika *standard quality* ya bei ya juu huko nje. Tutazame Mhe. Spika, likija huku Zanzibar tunalishwa kwa bei ya juu. Hii hali inasikitisha sana bado vyakula vinapanda bei siku hadi siku. Hebu tuliangalie hili suala na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie ili uweze kufanikisha vizuri.
Mhe. Spika, ukurasa wa 38 ujenzi wa barabara. Niunge mkono kwa dhati kabisa kutokana na huu utekelezaji wa ilani imetekelezeka vizuri hususan kutokana na barabara na mimi imenipita pale kati ya Fujoni na Kiombamvua kuelekea Bumbwini. Mhe. Spika, naunga mkono barabara hii, lakini pamoja na kuunga mkono barabara hii naomba kama alivyosema mama yangu basi tuoneshwe.

Wenzetu kule njia ya Wilaya ya Kati walioneshwa kwa vitendo, walivamia tu wakaanza kuburuga, sasa na sisi tuoneshwe dalili ile, hapo ndio tutajua kama kweli sasa hivi tunataka kutengenezewa barabara yetu. Lakini mpaka leo bado tuna kitendawili kikubwa sana kuhusu suala hilo.

Mhe. Spika, siku nyingi sana tumepiga kelele na mzee wangu Mhe. Said Khelef Ali hapa, leo mama ndio kaanza mwanzo kusema yeye hapa, tumepiga kelele mpaka tumechoka tumeona ile barabara. Lakini sasa hivi imeshapimwa, mabuldoza yameshapelekwa, inawezekana mabuldoza yakawekwa na hatimaye yakaharibika pale pale hakuna hata kimoja kinachofanyika. Kwa hivyo, naomba na hili tulitilie mkazo ili tuweze kwenda vizuri kabisa.

Mhe. Spika, nikija ukurasa wa 50 kifungu cha 94 kuhusu suala la AK na JK. Hapa nashukuru sana naunga mkono lakini naomba tuongeze kasi. Siku moja Mhe. Waziri Kiongozi alituita akatuelimisha na kazi tukenda vizuri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi akemee tena hivi sasa ili kasi izidi kuendelea kwa sababu imezorota. Baada ya kutia mdomo wako ukaelimisha na ukatoa ukakamavu kasi ilizidi lakini sasa hawa watendaji wako *slow down*.

Tunamuomba Mhe. Waziri Kiongozi awachechemue tena ili tuweze kufanikisha. Siku zinakwenda na sisi tumekusudia ndio sehemu moja ya kujisaidia tukapata kurejeshwa tena kwenye majimbo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 51 miradi ya wananchi, hapa vile vile namshukuru Mhe. Waziri kwa utekelezaji wake pamoja na wafuasi wake wanakwenda vizuri sana, lakini masharti kidogo wameweka magumu, tunaomba walegeze masharti. Kuna wananchi wengine wana uwezo wa kufikisha katika kozi tatu mpaka nne katika miradi ya shule, lakini kuna wananchi wengine hawana uwezo huo pamoja na wawakilishi wao kwa sababu mfuko wenyewe ndio kwanza unaanzwa leo kuzungumzwa hapa. Wenzetu wameshaanza kuona neema hiyo, lakini sisi ndio kwanza tunaizungumza hatujui mjaliwae.

Lakini tunachozungumza Mhe. Spika, hebu hii awamu iliyobakia tuliyopeleka miradi waliofika ile *foundation* wasaidiwe kiasi ambacho waoneshe, pengine huko *asaakheri* anaweza kutokezea mfadhili akawasaidia juu. Sasa haya masharti ya kusema kuwa lazima ifike kozi hiyo Mhe. Spika, hapa tutafika pabaya. Ningeomba na hili tuweze kulifikisha pahala pazuri sana.

Mhe. Spika, ukurasa wa 54 kifungu cha 103 hili suala la marekebisho ya mishahara kila siku tunalizungumza. Mhe. Spika, hebu tuondoe urasimu katika suala hili. Mhe. Ame Mati Wadi alilizungumza hapa na ndio maana ikawa waziri mwengine akisimama akisikia suala kama hili atakurejeshea wewe. Sasa hizi kasoro ambazo kama zimo kwenye wizara yake Mhe. Waziri, basi namuomba hebu tuondolee ili tufike pahala na sisi angalau wananchi wetu waweze kujisikia na mshahara wao. Kwa sababu wengine mishahara iko chini, maisha yako juu, ongezeko la bei za vyakula ndio kama nilivyosema vinazidi kupanda.

Mhe. Spika, ukurasa wa 74 kuhusu habari ya Muungano hata mimi napongeza sana. Lakini hapa kidogo juzi nilipata wasi wasi mmoja katika kikao kile nafikiri kimefanyika Bwawani kama nimekosea Mhe. Spika, utanisaidia. Mhe. Spika, kuna jambo ambalo ni muhimu sana kwa Zanzibar hili suala la *IMO*. Sijui kwa sababu gani tunakosa kuwa wanachama sisi Zanzibar na sijapata lugha ya mantiki hasa. Kwa sababu sasa hivi Zanzibar inaleta makampuni ya kuajiri vijana wetu masuala ya ubaharia.

Kwa mfano, tunayo *Donauns* hapa lakini *certificate* inatoka Zanzibar, ajira inatoka Tanzania Bara, kampuni iko Zanzibar, najiuliza. Lakini pia tuna msajili wa meli hapa. Sasa hili suala Mhe. Spika, sijui ilikuwaje. Namuomba Mhe. Waziri Kiongozi tulitazame suala hili kwa sababu lina mantiki kubwa kwa Zanzibar nalo tunakosa mapato. Kule Bara wanachukua mapato mengi sana, sasa hivi ile kampuni ime-*register* wafanyakazi kama sikosei si chini ya elfu

nne wako ndani ya meli. Elfu nne hiyo wamepelekwa kule Dar es Salaam kuchukua cheti sijui kiasi gani, kama laki mbili au laki tatu.

Sasa tuangalie pato limetukimbia hilo. Hebu tuangalie hii *IMO* hatuna historia nayo Zanzibar? Mimi nasikia kama kwa mbali tunayo kwa sababu sisi Zanzibar ndio wa mwanzo kuwa mabaharia na kuweza kuitetea hiyo kwa wenzetu. Mhe. Spika, tulisema hiki chuo cha *IDMO* kama hivi kidogo imenitoka kwa sababu mdomo wangu umeshakuwa mzito na mate hamna maji.

Sasa hiyo Mhe. Spika, hebu tuiangalie vizuri na hayo ni kero kubwa. Kwa sababu leo tunataka kuondoa umaskini kwa vijana wetu, zinakuja kampuni hapa zinataka kuajiri vijana wetu tunashindwa. Halafu isitoshe mimi siku moja nilizungumza na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi lakini nilijiuliza huyu hata akikubali kile chuo *certificate* yake itafika wapi, Chumbe haivuki, haikubaliki, watashushwa tu vijana wetu.

Sasa hebu tukae tayari serikali tuangalie eneo hili tulipe uzito, zana wanazo wale *Donauns* za kufundishia tena *international* kabisa zinakubalika. Tutoe fursa hiyo tuwakubalie chuo chao angalau basi tupate wale walimu basi waje hapa, ni kitu *simple* hiyo. Wakija hapa waungane na hawa hapa basi watutolee mitihani na waweze kufanya vijana wetu lakini lile pato sehemu ibakie hapa. Mhe. Spika, hili nalo ni kero kubwa kwa sababu sasa hivi hao vijana fedha yao yote wanaitia Benki ya Watu wa Zanzibar, hawawekezi huko nchi walizokuwepo wanawekeza hapa kwao, ni moja ya faida nzuri.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri walitilie nguvu hili. Katika hayo majadiliano wanayokaa pamoja na hili tulipe kipaumbele. Tunayo sheria ya kuweza kujiunga *IMO* jamani hebu tuingieni kwenye vitabu. Mimi ningeruhusika leo basi ningekuja na tabu kubwa ningekuonesheni sheria hii hapa Zanzibar inayo ruhusa ya kuingia kwenye *IMO* lakini bahati mbaya sikujitayarisha.

Mhe. Spika, hayo ni mambo ambayo nimeona kwa leo hii niyaeleze kwa fasaha kabisa na kama muda unao, basi niko tayari sijesha ili niweze kuendelea. Lakini nataka niheshimu wakati wako Mhe. Spika, ili na wengine waje kuchangia. Kwa hivyo, hizo ni kero ambazo naomba Mhe. Waziri atusaidie hili suala.

Suala la mwisho katika ukurasa wa 78, suala la 4.5. Mhe. Spika, sisi ni serikali hebu wenzetu waliangalie vizuri hili na kama ni serikali mheshimiwa 4.5 haikidhi haja, tungekuwa tunazipata vizuri hizi fedha mheshimiwa, hata hizi sijui kama tunapewa sawa sawa 4.5 nadhani haziendi asilimia ambayo inatakiwa, unapewa vile vile kasoro. Lakini kuna mambo mengine na sisi

tujiangalie ni serikali 4.5 ni sawa sawa na Mkoa wa Kaskazini tu. Kwa hivyo, hili nalo tuliangalie, kuna sheria zinazorekebishika na warekebishaji ndio sisi mheshimiwa. Sasa na hili suala tukae tuliangalie ili liweze kutusaidia, haikidhi haja hii 4.5 mheshimiwa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi leo kunipa fursa hii ya kuchangia machache kuhusu bajeti hii ya serikali ya mwaka 2010/11. kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Allah kwa kutuweka hai na tukawa wazima, tukapata kauli ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Pili napenda nichukuwe fursa hii kwa sababu ni kikao chetu cha mwisho cha bajeti katika kipindi hiki cha miaka mitano, niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Ziwani, wale waliopata fursa ya kunichagua na wale ambao hawakupata fursa ya kunichagua, lakini tulikuwa pamoja katika kipindi chote na niliweza kupeleka utumishi wangu kwao. Namuomba Mwenyezi Mungu atuweke tena ili katika kipindi kijacho tuwe pamoja.

La tatu Mhe. Spika, napenda nikushukuru wewe kwa kutuongoza vizuri katika Baraza na kuonesha uvumilivu wako pale ambapo mahitaji yalihitajika.

Nikianza mchango wangu, kwa leo napenda nitowe shukurani zangu kwa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake refu ambapo nilifikiria angekunywa maji katikati, lakini *stamina* yake ilikuwa kubwa hata *glass* ya maji hakuwahi kunywa na masaa mawili na nusu aliyakata.

Mhe. Spika, maneno mengi yametajwa katika hotuba ile, lakini kuna maneno huwa yanarudiwa sana likiwemo MKUZA, MKUKUTA na MKURUBITA. Maneno haya hayaingii maskioni mwa watu ikiwa hayakupata tonge ya rizki. Waarabu wanaita *lukmat l-aaysh.* Hii tonge ya rizki ndio inayopiganiwa na watu. Wewe sema maneno yako yote, lakini anachokitazama mwananchi ataongeza kiasi gani katika tumbo lake basi, hayo maneno yako atakuachia wewe mwenyewe.

Kwa hivyo, mimi napenda kumwambia sana Mhe. Waziri kwamba katika hotuba yake kawanyima sana wananchi tonge ya rizki, kwa sababu hakueleza kiunaga ubaga, vipi mwananchi atanufaika na bajeti hii. Tukija nukta ya mwanzo, pato la nchi. Kwa kweli kuna mambo mengi makubwa katika suala

zima la kero za Muungano. Tumeunda kamati ile kwa sheria kamili ya bunge *JFC* ya kushughulikia kero za Muungano katika masuala ya uchumi yaani fedha, lakini hakuna lililokuwa katika kipindi chote hichi cha miaka mitano niliyokuwepo mimi. Nasikitika sana kusema kwamba karibu ya serikali nzima imeshindwa kutatua kero za Muungano katika kipindi hiki kwa masuala ya kiuchumi. Hili suala Mhe. Waziri lichukulie kwa hali yote ya uzito na uje utueleze katika hotuba yako ya kusawazisha, vipi mnamkakati gani kulingana na haya.

Kwanza ndani yake kuna namna ya ugawanaji na ukusanyaji wa mapato, kuna suala la marekebisho ya asilimia nne na nusu, kuna suala la kujiunga na Jumuiya za nje zinazosaidia. Nili-*point out* katika kamati, nilisema kwamba mimi nilishuhudia kipindi ambacho kinaeleza jinsi gani zile nchi zilizojiunga na *OIC* na nchi changa zinavyosaidiwa, wala sio suala la Uislamu kwa sababu Uganda kuna asilimia ndogo sana ya Waislamu. Lakini kuna suala zima la maamuzi, nani ni muamuzi kwamba Zanzibar wajiunge na *OIC* au wasijiunge.

La pili, kuna masuala mengine, kwa mfano miradi ya *TASAF*, ukifanya mahesabu hata asilimia 4.5 haifiki na ukiuliza unaambiwa inagaiwa kimkoa. Sasa kimkoa vipi, ina manaa na sisi Zanzibar tumeshakua mkoa au vipi. Kwa sababu ikiwa ni asilimia 4.5, basi angalau basi iende sambamba ile ile, lakini hakuna.

Mhe. Waziri Kivuli kataja mambo mengi ambayo mimi sina haja ya kuyarudia, nayaunga mkono yote na ninaomba serikali iyachukulie kwa umakini wake, kwa sababu amefanyakazi ya kutosha. Kama tunataka kujenga uchumi, hatuwezi kuondoa kitu kimoja tukaweka chengine, isipokuwa tutaongezea juu ya kile kitu chengine. Suala la zao la karafuu halizungumzwi kwa kina chake katika bajeti ya serikali na ambalo bado linatoa mchango katika mapato ya serikali.

Mhe. Spika, hata utalii. Pengine hiyo mikarafuu ni sehemu moja ya watalii wanaokuja kutazama. Sasa ikiwa lile zao lenyewe la karafuu utaliondoa katika msisitizo na uzito wa serikali, tutachangia nini sisi. Fedha zinazotolewa kuimarisha zao la karafuu hazilingani kabisa na hali halisi ilivyo kwa zao hili. Kwa hivyo, ni kwa nini chanzo kikuu cha mapato kiweze kubezwa kiasi hicho. Mwaka jana na mwaka huu tumetumia muda mrefu sana katika Baraza hili na mahojiano na majadiliano makali makali, wataalamu walitoka Norway walikuja hapa tukazungumza suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta, tukapitisha azimio na Mhe. Rais akalitangaza katika sherehe za Mapinduzi Januari pale Gombani, lakini bajeti hii haikusema chochote, ndio tumekwama. Ni afadhali kuwa mkweli kwa wananchi, kwa sababu ndio wanaotuchagua.

Kama sisi viongozi na ilani yetu ya CCM imeshindwa kwa suala la mafuta basi tuwaambie wananchi wao wenyewe watajua la kufanya. Tunazo kura za maoni zinakuja, tunaanza hii moja tu, lakini na nyengine inakuja wananchi watasema. Tangazeni kwamba sisi tumeshindwa, tumekwama pahala fulani, lakini sio vizuri kunyamaza kimya, hata kama wengine tunahitaji kuteuliwa kuwa marais, lakini haizuwii wananchi kupata habari, tusiwanyime wananchi kupata habari ya jambo lilivyo kwa maslahi ya binafsi. Tunahitaji Mhe. Waziri uje utueleze tumefika wapi hata ikawa hata shilingi moja haikupangwa kwa ajili ya uendelezaji wa suala hili hata kutajwa.

Mhe. Spika, kuna kitu wataalamu wanakiita *wage bill* yaani kile kima cha pato la taifa kinacholipia mishahara. Katika bajeti ya mara hii mimi nimeangalia tena yale ya makadirio sio mapato halisi, basi kima cha kulipia watu mishahara kinafikia karibu asilimia 50 ya makadirio ya mapato ya ndani. Sasa kuna mambo mawili ya mafunzo katika hali hii. Sisi tunasema kwamba mishahara ya Zanzibar ni duni sana, nitakuja kuizungumza maelezo yake baadae. Ukilinganisha na Tanzania na East Africa nzima, basi mishahara ya Zanzibar ni duni, lakini ule mkusanyiko wa mishahara unafanya karibu asilimia 50 ya mapato ya nchi, hii ina maana bado nchi haijakuwa na uwezo wa kutayarisha mapato yake ya kutosha.

Mhe. Spika, wakati Afrika ya Kusini wafanyakazi wanagoma serikali iliwaambia sisi hatuwezi kutumia zaidi ya asilimia 20 ya mapato yetu kulipia mishahara. Naomba kuwanukuu, "*we will not allow wage bill to go beyond 20 percent over our income".* Kule ni Afrika ya Kusini na watu wanapewa mishahara mikubwa kuliko hapa pengine mara mbili au tatu au tano, lakini ile mishahara bado haijafika asilimia 20 ya pato la taifa, wale wafanyakazi wanadai zaidi. Sisi hapa tumeshafika karibu asilimia 50 na mishahara yetu hii, laki moja ya mshahara wa ngazi ya chini ni Shs. 3,000/= kwa siku. Sasa Shs.3,000/= kwa siku hata unapoalikwa semina, ile *package* ya chai yote inazidi Shs.3,000/=. Sasa Shs. 3,000/= kwa siku ndio tunampa mtu sisi kwa ngazi ya chini. Lakini mishahara ukiijumlisha iko zaidi karibu asilimia 50, inaonesha kwamba hata kama tutagawa kwa asilimia ngapi, pato la taifa bado halijatosheleza kwa kiwango fulani matumizi ya nchi.

Sasa serikali ituambie, kama inataka kuchaguliwa tena ina mikakati gani itakapofika mwaka 2011/12 iongeze pato hili kwa mara mbili, ina mikakati gani kama inataka kurudi tena madarakani. Haitaki basi ituachie sisi CUF, kwa sababu serikali maana yake ni kuwaongoza watu kwa maslahi yao, sasa wewe kazi yako ni kuongeza mapato ili wananchi wakafaidika, basi tuelezeni baada ya miaka minne ya kushuhulikia hii mnashindwa kufikisha hapo. Basi tueleze Mhe. Waziri je, una mkakati gani kwa mwaka huu kuongeza mapato mara

mbili, la unashindwa basi wananchi wenyewe wataamua mwaka 2010/11 watampa nani.

Mhe. Spika, bajeti hii iliitwa bajeti ya demokrasia na maendeleo. Mimi nimebakisha neno moja, moja naomba niliondowe. Mimi nimeiita ni bajeti ya demokrasia na masikitiko. Kwa nini Mhe. Spika, nikasema hivyo. La mwanzo ni kwamba hakuna nyongeza yoyote ya mshahara aliyopewa mwananchi wa Zanzibar, sasa ataendelea au atasikitika. Ikiwa kwa mwaka huu Mhe. Waziri hakumuongezea hata shilingi, ataendelea au atasikitika. Kwa hivyo, mimi nimeiita bajeti ya demokrasia na masikitiko.

Mhe. Spika, kuhusu wastaafu. Unapomwambia mstaafu nakutoa kwenye Shs.15,000/= nakupeleka kwenye Shs.25,000/=. Hebu tueleze Mhe. Waziri unakusudia kumwambia vipi yule mstaafu. Mimi nafikiria kwamba mstaafu kwa kumuondolea kero, kwa uwezo mdogo ulionao Zanzibar, basi angepewa kile kile kima cha chini cha mshahara wanaopewa wafanyakazi, hakuna njia nyengine. Angalau angepewa kima cha chini wanachopewa wafanyakazi, kwa sababu yale maendeleo tunayojivunia sisi na yale mambo ambayo tunajivunia sisi basi waliyafanya wao ndio sisi tukayakuta.

Mhe. Spika, hii ni sawa sawa na jela. Jela siku zote ipiganie iwe ni pahala pazuri, kwa sababu mmoja wetu atafika pale pale. Au siku hizi tunaita ulemavu na ulemavu upiganie kwa sababu binadamu hajamaliza kuumbwa, unaweza siku moja ukawa na wewe ni mlemavu na wewe ulisema wasipewe haki yoyote. Kwa hivyo, na hawa wastaafu na sisi tunakwenda huko huko, inawezekana leo mimi ni mwakilishi lakini sijui mambo yatakuwa vipi nikarudi ualimu, halafu nikapewa kile kiinua mgongo cha mwalimu. Kwa hviyo, ni lazima tuwe na mikakati ya kuwasaidia wazee wastaafu, maana wanapiga kelele sana kwa sababu wametumiwa kwa muda wote huo na wala hawapati kitu. Shs. 15,000/= mpaka Shs.25,000/=.

Mhe. Spika, kama kwenye jimbo kuna wastaafu kama kumi au kumi na tano basi naamini mwakilishi anaweza akawapa pesa hizo, wala serikalini wasiende. Kwa hivyo, waseme tu serikali kuwa sisi tumeshindwa, basi hichi tunachokipata humu sisi tutawapa wazee wanaostaafu kwa kiwango hicho cha 25,000/= tunamiliki kuwapa, tutajikosesha siku moja tu. Lakini haiwezekani kusikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawapa wastaafu kutoka 15,000/= mpaka 25,000/= sio rahisi kulifahamu.

Mhe. Spika, nikiendelea. Mimi sitaki kuzungumza wizara kwa wizara kwa sababu muda wao utakuwepo. Lakini nilikuwa nasema kwamba wizara za uzalishaji hazijapewa hasa kipaumbele, kwa sababu tunapozungumza hapa

tunazungumza uchumi. Wizara za uzalishaji hazijapewa kipaumbele kinachostahiki katika bajeti hii.

Kwa mfano Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kusema kwamba wakiingiza *machinery* ndio kodi itapunguzwa. Kwa kweli mwenye kuingiza *machinery* ni nani, ni mkulima wa kawaida au ni kampuni. Kama ma-*harvesters* na mambo mengine ni nani atakayeingiza ni mkulima gani wa tungule atakayeingiza *harvester*. Sasa tuangalie upya ni vipaumbele gani vilivyopo, vingepunguzwa na ingekuwa serikali ime-*subsidize* utumiaji wa trekta kwa eka, wakasema asilimia 20 itachukua serikali, pale tungesema kuwa kila mkulima angalau kaonekana. Lakini kupunguza ushuru tu hakusaidia kitu.

Mhe. Spika, alizungumza Mhe. Waziri kivuli suala hili, uwiano kati ya bajeti ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano hasa katika shughuli za kodi. Tulifikiria kwamba mambo ya serikali ni *confidential otherwise* iwe wenzetu hawaamini kwamba hii ni serikali. Ikiwa wenzetu Tanzania Bara hawaamini kama hii ni serikali basi mambo yao kweli ni *confidential.* Lakini kama wanaamini kwamba na hii SMZ ni serikali basi ilikuwa Waziri wa Fedha wa hapa na wa kule wakutane wajuwe kabla ya bajeti kitu gani kinatokezea. Lakini ikiwa hakuna hiki, basi itabidi tuangalie upya mtazamo wa wenzetu wanaamini kwamba hii SMZ ni serikali au pengine wanaichukulia tu ni serikali ya mtaa basi wao wanaweza wakapanga mambo yao kama yanavyokwenda, ndio tunarudi kule katika kero za Muungano.

Mhe. Spika, jengine katika bajeti hii ambalo lina mashaka kidogo, Mhe. Waziri hakutuonesha ni kwa kiwango gani bajeti hii itatuongezea ajira katika kipindi hiki. Suala hili la ajira ni muhimu sana na bajeti ilikuwa ni lazima ilizungumze kwamba katika kipindi hiki tutaingiza viwanda vitatu na vitatoa ajira kiasi fulani na mambo kadhaa wa kadhaa.

Mhe. Spika, leo asubuhi tumeikutia hali hiyo, wanafunzi wa mwaka 2009 wa Chuo cha Sayansi ya Afya wa Mbweni, wamemaliza lakini hawana ajira wako nje na wengine wanasoma. Mhe. Waziri kasema kati ya 241 wameajiriwa 80 mpaka sasa hivi, sasa haileti picha nzuri kwamba sisi tuna vyuo vyetu hapa vikuu, kwa hivyo ile tuichukulie kwamba ni *output* yetu, kwa hivyo Mhe. Waziri angekuja akasema katika kipindi hiki cha mwaka huu *output* yetu kutoka katika vyuo vyetu vilivyokuwa hapa, ni watu kama 500 au 600 lakini serikali imeshakuwa na uwezo wa kuajiri watu 700, kwa hivyo wengine 100 tutawaagiza kutoka nje. Lakini ikiwa hatuzungumzi ule uwezo wa ajira tulionao na bado *output* zipo hakuna ajira, ina maana uwezo mdogo wa serikali. Kwa hivyo, uwezo mdogo wa serikali ina maana huu ni mwaka wa uchaguzi wananchi wataamua.

Mhe. Spika, kuna jambo ambalo ni muhimu sana katika bajeti, wananchi wanahitaji kuona kwamba kuna uwiano wa kimaendeleo, kwanza baina ya Unguja na Pemba na ya pili baina ya mkoa na mkoa. Haya ni mambo muhimu katika upangaji wa bajeti. Lakini haionekani kufanyika hivyo. Tunashukuru sana na ni suala la kupongeza kwamba Pemba kuna mkonga na Unguja upo na mwengine mpya unakuja wa umeme. Kwa hivyo, kila mmoja ana mkonga wake. Sasa mfano huu ungechukuliwa na katika maeneo mengine ingesaidia sana katika kupunguza ule ukali wa mabishano baina ya Unguja na Pemba. Kwa sababu ukizungumza suala hili unaonekana wewe uko kinyume. Hapana, kila binadamu ana hamu ya kuona kwamba yeye anapata jambo kama alilonalo mwenzake. Hiyo ndio *nature* ya binadamu.

Sasa Mhe. Waziri na sekta nyengine zingefuata mpango huu. Mhe. Spika, angalia Mhe. Waziri alivyojibu leo, mfano huo huo. Kasema kwamba katika watu 241 watu 18 tu manesi ndio waliopelekwa Pemba. Sasa hiyo kweli kuna uwiano hapo katika ile *deplaning* ya kuona kwamba ajira ya huku na ya huku, kweli kuna *proportionality* ya *population* mimi siikatai hiyo, lakini nayo kuna *proportionality* ya *estimate* yenyewe ya mambo. Kwa hivyo, tungependa mambo yende hivyo.

Mhe. Spika, tuje kwenye sekta ya uzalishaji wa viwanda. Kwa kweli bado serikali haijachukua mkazo katika sekta hii. Alizungumza mwenzetu mmoja hapa kwamba kuna viwanda vinataka kuanzishwa, lakini kuna vikwazo vya makusudi vinawekwa. Sasa nasema ile *responsibility* sio ya Wizara ile ya Utalii, Biashara na Uwekezaji peke yake. Linapofika suala la mapato, kwa sababu kiwanda kama hakikuanzishwa na kuendelezwa basi serikali inakosa mapato, serikali ikikosa mapato wananchi wanakua hawafaidiki na ile. Kwa hivyo, inapofika hatua hiyo inakuwa ni *intervention* ya Serikali Kuu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu njoo na jibu lililokuwa sahihi kabisa sasa hivi kuhusu ufuatiliaji wako wa suala la viwanda hapa Zanzibar linakwamishwa na nini, wazi wazi kabisa.

Mhe. Spika, kuhusu Sekta ya Uvuvi, pamoja na malengo mazuri yaliopo, lakini serikali imekuwa ni kipaumbele katika kukwamisha Sekta ya Uvuvi. Kwanza haikutajwa kikamilifu katika bajeti hii. Pili, taarifa tuliyonayo, nizungumze sasa katika *level* hii ya Kizanzibar, sio *level* ya kiwizara kwamba kuanzia mwaka 2006 zilikuwepo hapa *hundred million USD* mkononi za kujenga bandari na *processing plant* ya uvuvi wa samaki, ardhi ndio iliyoshindikana, pesa zile zimerudishwa katika mfuko wa Japan. Hizo zilikuwa mkononi tu sio pesa zote za *capital* ile, zile *initial budget* alizopewa yule muhusika ni *hundred million USD* zimerudishwa, kwa sababu ya mabishano ya ardhi.

Mimi namshukuru sana Mhe. Ramadhan Abdallah Shaaban leo alipokuwa akijibu swali lake. Alitumia neno kwamba bei za kuchukulia fomu zimepandishwa kwa sababu ya kuwapata wale wagombea *serious*. Naamini madhali tunaanza kuwapata wagombea *serious*, na huko siku za mbele serikali nayo itakuwa *serious*, kuliko hivi ilivyo sasa. Kwa sababu labda huko nyuma ilikuwa hatuwapati wagombea *serious*, ndio maana serikali ikawa sio *serious*, mpaka ikabidi fedha zirudi ziende kule. Kwa hivyo, mimi naamini maneno yake kwamba kwa kuwapata wagombea *serious* na serikali itakayopatikana *Inshaallah* itakuwa *serious*.

Mhe. Spika, suala la uvuvi wa bahari kuu jamani ni suala muhimu sana. Hebu twende sisi, mbali ya kipato cha wale wavuvi, lakini Zanzibar tuwapeleleze wale wananchi wanakula kiasi gani cha kitoweo, halafu tufike wakati tugeuze hii lugha, kile kitoweo tuje tukiite chakula, kwa sababu wenzetu wanatuambia wanaanza na kile kitoweo na sisi tunaanza na chakula. Kwa mfano, mimi nimekula wali kwa nyama, lakini wenzetu wanatuambia *meat and rice or served with rice or potatoes*, yaani anaanza na kile kitoweo.

Kwa hivyo, sisi bahari hii iliyotuzunguka bado tunakula wali kwa samaki na wala sio samaki kwa wali. Kwa maana hiyo, nadhani serikali iwalishe samaki kwa wali.
Kwa sababu bahari yote iliyotuzunguka pamoja na teknologia yote ilioko duniani bado tuna *survive* hapa hapa tu, kuna mlima wa wali na bahari ya mchuzi, lakini kijipande cha samaki. Ikiwa mama kanipa mzima basi ujue saladini ameingia siku hiyo.

Kwa hiyo, tuibadilishe hali hii na lazima Zanzibar tuiweke mahala pengine, yaani bahari hii tuitumie, kwa sababu serikali bado haijawa *serious* kwani haijatajwa. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho namuomba aje na maelezo kwa suala la kutoitaja bahari au tuko bara sasa hatujazungukwa na bahari *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa kweli mambo ni mengi, lakini naheshimu muda wako kwa hiyo napenda kumalizia kwa kusema kwamba, tunashukuru sana viongozi wetu wawili kukaa kitako na kufikiria wananchi. Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, waliondoa ndani ya nafsi zao ubinafsi na kusema jamani twende katika njia hiyo.

Kutokana na hali hiyo, mimi nawaomba waheshimiwa wenzangu pamoja na wananchi wote wanaotusikia na watakaotusikia wajitokeze kwa wingi siku ya tarehe 31 Julai, 2010 kwa kuitikia wito wa kupiga kura ya maoni. Lakini akili yangu iko katika kusema kukubali hili kwa masuala matatu.

Kwanza hiyo amani na utulivu unaotajwa, lakini wenzetu wanasema kwamba watu wakiwa wanasikilizana ndani ya nchi viongozi wanatulia. Vile vile watu wakiwa wanasikilizana katika nchi *compliance* ikiwa ya ushuru au sheria na mambo mengine inaongezeka. Kwa hivyo, itakuwa hakuna misuguano.

Pia kuna gazeti moja ambalo linalozungumzia kuhusu masuala ya usaidiaji wa jamii. Kwa maana hiyo, jamii itakuwa ikisaidia na zile kero zitaondoshwa na wenyewe.

Kwa haya machache Mhe. Spika, naomba nimalizie hapa, naitakia njema Zanzibar pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi ije itupe ufafanuzi wa haya tuliyoyauliza na Mwenyezi Mungu atusaidie *Inshaallah (Makofi).*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Serikali. Kabla ya kuanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kufika hapa kwa salama.

Aidha nikushukuru na wewe kunipatia nafasi hii ya kuzungumza hapa, ukiwa katika hali ya utulivu na makini kwa kusikiliza michango wa wajumbe wako.

Vile vile niwashukuru wananchi na hasa wapiga kura wa CUF walioanza kunionesha njia kwamba naweza kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunipa kura nyingi za ndio kwenye Kura ya Maoni. Naamini kwamba ngazi inayofuatia bila ya shaka kutakuwa na hatua nzuri ya busara *(Kicheko/Makofi)*. Mhe. Spika, bajeti hii tumeambiwa na Mhe. Waziri kwamba ni Bajeti ya Demokrasia na Maendeleo. Mwaka jana ilikuwa ni Bajeti ya Miundombinu, ambayo kwa kweli ilitafsiri Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya miaka kumi, kwa sababu mwaka jana bajeti nzima ilikuwa imejikita kwenye masuala ya maendeleo ya miundombinu.

Kwa hivyo, naomba nikiri kwamba Serikali ya Awamu ya Sita kwa kiasi fulani imepiga hatua kwenye suala la miundombinu, isipokuwa zipo dosari ndogo ndogo ambazo lazima tuzieleze, ili serikali kupitia Mhe. Waziri aweze kuziangalia *(Makofi).*

Mhe. Spika, niende kwenye suala la Bajeti ya Elimu. Bajeti hii zaidi imezungumzia ongezeko la majengo pamoja na takwimu za wanafunzi, lakini Mhe. Waziri hakutueleza ni hatua ipi atachukua kwa ajili ya kutekeleza ahadi ya serikali ya kumaliza majengo yaliopo.

Kwa kweli serikali imewashajiisha wananchi kujenga majengo ya skuli na yanapofikia hatua na kuezeka basi serikali itamaliza majengo hayo. Lakini hivi

sasa Unguja na Pemba majengo mengi yamejengwa bila ya hatua ya kumalizwa na serikali. Sasa hatua ya serikali kuzungumza zaidi takwimu za wanafunzi bila ya kuyamaliza majengo, nadhani bado hatujafanya kitu kwenye sekta hii ya elimu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anielezee hasa msimamo wa serikali kwenye bajeti hii, kuhusiana na kumaliza majengo yaliopo pamoja na kuendeleza majengo mengine ya skuli kwa Unguja na Pemba.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu umuhimu wa Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*). Kwa kiasi gani serikali hutumia tafiti za Chuo Chuo Kikuu cha (*SUZA)*. Kwa sababu kwenye nchi yoyote duniani Vyuo Vikuu ndivyo vinavyotoa ushauri mkuu kupitia tafiti kwa serikali husika. Kwa Zanzibar ni kiasi gani serikali huchukua ushauri na tafiti za Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA)* kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu hadi leo wanafunzi wa Zanzibar wamekuwa wakienda Dar-es-Salaam kwa ajili ya kufanya *practical* zao, kwa kuwa *SUZA* hawana maabara ya kisasa yenye kulingana na hadhi ya Chuo Kikuu.

Kwa kweli mpaka leo serikali huwapatia *SUZA* shilingi 50 milioni kwa ajili ya kujengea maabara hazitoshi si kwa SUZA tu hata kwa Skuli ya Lumumba. Kwa hivyo, hali hii ndio inayosababisha kwamba wanafunzi wa Zanzibar kuelekea Dar-es-Salaam kwa ajili ya kuendelea na masomo yao ya Chuo Kikuu.

Mhe. Spika, naiomba serikali kwenye bajeti hii kuzingatia umuhimu wa Chuo Kikuu pamoja na kuendelea kwa elimu ya teknologia.

Jambo jengine ambalo nataka nilizungumze kwenye elimu ni kuhusu uendelezaji wa teknologia, kwa kweli sijaona kwenye bajeti hii kwa kiasi gani serikali imejipanga kuendeleza wanafunzi kiteknologia. Kwa sababu skuli nyingi wanafunzi wengi hawajui masuala ya *computer*, yaani hata wale waliomaliza vyuo hawana taaluma ya *computer* na bado tunapuuza.

Lakini tukitizama wenzetu Wakenya bajeti yao hii ya juzi kila jimbo wametenga *computers* 300 na Rwanda. Kwa hivyo, naomba kujua Zanzibar mpango wa serikali uko vipi kuhusiana na fani hii.

Vyenginevyo tukiingia kwenye Jumuia ya Afrika ya Mashariki wenzetu watatuacha mbali sana, ikiwa Rwanda kila mwanafunzi anayo *computer* moja

na Zanzibar hakuna mpango huo. Basi maana yake Zanzibar tutaendelea kuachwa mbali sana kwenye fani hii ya sayansi na teknologia.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu ujenzi wa barabara Unguja na Pemba. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba barabara zimeangaliwa kwa kiasi kikubwa, ingawa zipo ambazo zinasababisha kilio, lazima tuzungumze, ili Mhe. Waziri aweze kulizingatia.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mipango mingi ambayo ni mizuri kuhusiana na ujenzi wa barabara. Lakini utekelezaji wake unakuwa wa kusua sua. Kwa sababu zipo barabara ambazo zimefikia asilimia mia moja na nyengine ziko kwenye asilimia zero.

Kwa hivyo, hatuwezi kuona Bajeti hii ya Demokrasia na Maendeleo huku tukiacha wenzetu wengi wakiwa nyuma kwenye barabara. Sasa katika hili nataka nijue, kwa sababu mwaka jana sikuridhika kabisa na matumizi ya shilingi 30 milioni ya ujenzi wa barabara ya Mgagadu hadi Kiwani kwa teknologia ya *RO-MIX*.

Hivyo, mara hii nataka kujua matumizi ya shilingi 600 milioni ya barabara ya Mgagadu hadi Kiwani na kwenye kitabu hiki kinaonesha kwamba zimeshatumika asilimia 76 ya fedha zile. Mhe. Spika, mimi si mtaalamu wa barabara sizioni shilingi 450 milioni ambazo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile. Ikiwa kweli kukata mlima mmoja wa dongo na kusambazwa barabarani ndio shilingi 600 milioni basi zimetumika.

Mhe. Spika, naomba nielezwe kwa niaba ya wananchi wa Kiwani nielezwe kuhusu asilimia 76 ya ujenzi wa barabara ya Mgagadu hadi Kiwani ni kwa namna gani, kwa ule mlima ambao umesababisha matope gari haziendi au kuna njia zipi za kifundi fedha hizi zimetumika.

Kwa kweli siridhiki na hesabu hii mpaka Mhe. Waziri kwa heshima kubwa anipatie matumizi sahihi kupitia kwako Mhe. Spika, ili wananchi wa Kiwani wakanipe heshima kubwa ya kuja hapa tena mwakani *(Makofi)*.
Mhe. Spika, nadhani barabara ile haina bahati, kwa sababu barabara ile alikuwemo Mhe. Salim Juma Othman, yaani mimi karibu mtu wa tano. Lakini masikitiko yangu ni kwamba barabara ile imekuwa na nuksi. Kwa sababu mpaka leo mipango mizuri ya serikali hupangwa, lakini utekelezaji wake unakuwa mbovu.

Kwa hivyo, kwa heshima kubwa na kwa kuwa naamini kwamba serikali nia yake ni njema, basi nipate matumizi haya yaliyotumika, ili watu wa Kiwani wapate kuridhika. Ikiwezekana kazi ile iendelee kwa kasi kubwa, kwa lengo la

kwamba Rais anayekuja tumpatie sifa kubwa kwa ajili ya barabara ile ya Mgagadu hadi Kiwani.

Mhe. Spika, barabara nyengine ambazo nataka nipongeze ni kuhusu zile za *NORAD* ambapo nimefarajika na barabara ya Mtambile hadi Mwambe, ingawa kwenye kitabu hiki imeandikwa Mtambile hadi Kengeja. Kwa hivyo, naomba kwa heshima kubwa ile ni barabara ya Mtambile/Mwambe, kwa sababu bila ya Mwambe hakuna barabara, ikiwa *computer* ama binadam basi ile barabara iitwe Mtambile/Mwambe ndiko kwenye hizo barabara.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri Kiongozi juzi alikuja na kuiona *speed* ya ujenzi sio mbaya, wala hakufika pale Kengeja tu alikuja mpaka Mwambe, kwa maana ya barabara ya Mtambile/Mwambie na wala sio Mtambile/Kengeja *(Makofi)*.

Kwa kweli ujenzi wa barabara ile unaendelea vizuri, isipokuwa wasiwasi wangu ni mmoja tu, kwamba zile barabara ni sita na zimepangwa ndani ya miaka mitatu. Sasa ikiwa barabara moja imechukua miezi 9, je hizo barabara tano zilizobakia zitachukua muda gani.

Mhe. Spika, ushauri wangu kama kuna kikwazo ambacho kipo basi kiondoke haraka, ili wenzetu wa Kangani, Wambaa, Pujini na Chambani na wao waweze kufaidika na wala isiwe kufaidika Mwambe na Mtambile tu *(Makofi)*.

Kwa hivyo, wasiwasi wangu ni muda ambao tayari umeshakwenda mkubwa na wala sioni ufanisi wake kwa barabara nyengine kama vile ya Mtambile/Kangani.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze hapa ni kuhusu Sekta ya Usafiri wa Baharini na hasa marekebisho ya Shirika la Meli. Kwa kweli mimi sikuona kwamba serikali iko *serious* kweli kufanya marekebisho makubwa kwenye Shirika la Meli. Kwa sababu ni muda mrefu sasa kumekuwa na kilio, kwamba Shirika la Meli lina wafanyakazi wengi ambao hawana tija na zaidi wafanyakazi wale wanaendelea kuchukua mshahara pamoja na kuongeza gharama za shirika.

Kwa hivyo, ushauri pekee wa kuwasaidia wale ni kuwastaafisha na kuwapa haki yao au kuanzisha utaratibu wa *sign on and off*. Lakini wafanyakazi walioko ndani ya afisi hawazalishi isipokuwa wale wachache ambao wako kwenye meli.

Vile vile nimepata taarifa kwamba hivi sasa meli ambao ipo ni MV. Maendeleo kwa sababu MV. Ukombozi nayo ni mbovu, kwa hivyo hata ile faida inakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilifahamu, tumeambiwa kwamba serikali imeuza meli ya MV. Mapinduzi, lakini je fedha ziko wapi na Shirika la Meli wameshirikishwa vipi. Kwa sababu wasiwasi wangu ni kwamba tuliwahi kuuza *Kilimani Bar*, lakini baada ya kupelekwa utalii ilipelekwa hazina na hatimaye pale kuna uzio mzuri unajengwa wa mtu mwengine.

Sasa wasiwasi wangu hapa ni kwamba meli imeuzwa na fedha ziko Hazina, lakini Shirika la Meli wenyewe halitafaidika. Kwa maana hiyo, nataka nijue fedha ziko wapi na mpango wa serikali uko vipi kuhusiana na ununuzi wa meli mpya, kwa ajili ya ukombozi wa Unguja na Pemba kwa usafiri wa baharini.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu suala la nishati, ambapo Mhe. Waziri nimuombe sana kupitia kwako Mhe. Spika. Kwa kweli bila ya kuzungumzia mafuta na gesi Zanzibar hatukuelewi. Mhe. Spika, kweli Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi tunamheshimu pamoja na kumpenda sana, lakini naamini kwamba alisahau, yaani wataalamu wamesahau kuliingiza suala la nishati ya mafuta na gesi.

Kutokana na hali hiyo, atueleze kuhusu makelele yote ya Waheshimiwa Wawakilishi, viongozi mbali mbali, Baraza la Mapinduzi na hata wananchi wa kawaida kuridhia tamko lile, basi leo hakuna hata sentensi moja kuhusiana na nishati ya mafuta na gesi. Isipokuwa naamini amesahau na bila ya shaka atakapokuja atatujibu vizuri, ili tuweze kujua.

Sambamba na hilo sisi tulifikiria chanzo kikubwa cha mapato Zanzibar ni Bahari Kuu. Kwa kweli tumegombana sana hapa kwa ajili ya kutetea haki yetu, lakini Bahari Kuu Mhe. Waziri hakuizungumza kabisa kwenye kitabu hiki kama ni chanzo ambacho Serikali ya Mapinduzi Zanzibar matarajio yake kupata fedha kwa ajili ya uchumi wa Zanzibar.

Kwa maana hiyo, mafuta, gesi pamoja na bahari kuu nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuelezee, ili tuweze kufaidika pamoja na wewe, watu wa Dimani wakupe baraka nzuri *(Makofi)*.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nimalizie ni kuhusu deni la taifa. Kwa kweli kwenye kitabu hiki limezungumzwa deni la taifa lakini zaidi kwa takwimu, hivyo mtu wa kawaida ambaye hajui historia ya madeni basi inakuwa

tabu kuyajua. Mimi sijui takwimu hizi pamoja na mahesabu haya kwamba mlikopa nini na mlikopeshwa nini.

Lakini nikitaka kujua nadhani nikwambie kwamba miezi miwili nyuma nilibahatika kwenda Malaysia pamoja na wenzangu. Kwa kweli kule tulipata masikitiko kwamba Zanzibar zaidi ya miaka 20 inadaiwa deni la mchele, sasa ikiwa *level* ya viongozi haizingatiwi. Kwa mfano, kule tuliambiwa sisi ni wawakilishi na kesho akiambiwa Sheha na kesho kutwa anambiwa mchuuzi kwamba Zanzibar inadaiwa kwa kweli ni aibu.

Nadhani tungefanya utaratibu, deni la taifa kuhusu mchele ambalo liko kule nje tukalilipa, kwa sababu baada ya kuambiwa Mhe. Waziri wa Fedha anambiwa Mwakilishi, kesho kutwa Sheha na hatimaye Mchuuzi kwa kweli ni aibu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tulivyoambiwa kwamba hatujakuwa *serious* katika kulilipa deni hili. Kweli tunadaiwa mpaka riba, lakini mkopeshaji amesema apewe hata ile fedha yake, lakini tunakimbia. Sasa kama hivi ni kweli Mhe. Spika, sisi hatupendi kusikia Zanzibar nchi hii ndogo pamoja na umasikini wake basi hata mazungumzo yashindikane kufanywa, ili deni lile likaondoka.

Baada ya maelezo hayo nadhani nikipata ufafanuzi wa matumizi ya fedha za ujenzi wa barabara ya Mgagadu/Kiwani shilingi 450 milioni, basi nitaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mawili matatu kuhusiana na Bajeti hii ya Serikali.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala kwa kutujaalia sote kwa pamoja na kutuwezesha kufika hapa katika kipindi hiki cha mwisho cha bajeti, kuhusiana na kupitia mipango hii ya Maendeleo ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya mwaka 2010/2011. Vile vile kuzungumzia juu ya utekelezaji wa bajeti iliyopita.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote kwa jumla kwa kuandaa bajeti hii nzuri *(Makofi)*.

Kwa kweli kila mmoja alipoisoma aliona kwamba ni bajeti inayoweza kuleta matumaini mbali mbali pamoja na kasoro zilizomo, kwa sababu bajeti hii haikukamilika inayo kasoro za hapa na pale. Ndio maana leo tupo hapa kwa

ajili ya kutoa michango yetu mbali mbali na kuweza kuwafahamisha wenzetu juu ya kasoro zilizomo, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia naweza kufanya mabadiliko kidogo, kwa lengo la kwenda na wakati tulionao.

Mhe. Spika, pia nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni kwa kunipa mashirikiano makubwa kwa muda wote wa miaka mitano, ambapo hivi sasa tunakaribia ukingoni. Kwa kweli mashirikiano yao yameniwezesha kufanya kazi zangu kwa wepesi pamoja na kuwawakilisha vyema kwenye Chombo hiki cha Kutunga Sheria, ikiwa pamoja na kuwasilisha malalamiko, maoni, ushauri wao kwa serikali na kuona kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Inshaallah Mwenyezi Mungu akinijaalia nategemea tena kuchukua fomu ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, matumaini yangu ni kwamba wananchi watanichagua tena kwa kura nyingi kwa kishindo *(Makofi).*

Vile vile nitumie nafasi hii kumshukuru sana kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Amani Abeid Karume pamoja na mtendaji wake mkuu Waziri Kiongozi Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi *(Makofi).*

Mhe. Spika, viongozi wetu hawa wawili wanahitaji kupewa pongezi kubwa sana. Kwa sababu mimi mwenye na nyinyi wengine pamoja na wananchi ni mashahidi, kwamba katika kipindi chao hiki cha miaka kumi tumeweza kushuhudia maendeleo makubwa sana. Maendeleo ambayo yamegusa kwenye nyanja mbali mbali ikiwemo afya, elimu, barabara, ustawi wa jamii pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli nikianza kuyataja hapa Mhe. Spika, hizi dakika zako 30 ulizonipa zinaweza kumalizika. Mhe. Spika, leo sisi wanachama wa Chama cha Mapinduzi tunatembea kifua mbele na tunathubutu kusema hata kama uchaguzi utafanywa leo, basi Chama cha Mapinduzi kitashinda na kitasimama kidete *(Makofi).*

Kwa hivyo, niwashukuru sana viongozi wetu hawa kwa kusimamia vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na uwezo wao umeonesha dhahiri kwamba ni viongozi jasiri, ambao wanaweza kusimamia vyema masuala ya wananchi *(Makofi).*

Vile vile Mhe. Spika, na sisi tusijisahau Waheshimiwa Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu katika kipindi chote hicho ni sisi tulioweza kupitia bajeti mbali mbali. Kwa kweli tumeweza kutoa michango yetu mbali

mbali pamoja na kusimamia masuala tofauti kwenye kamati, yote haya kwa pamoja kwa ajili ya kuona mambo yetu yanakwenda vizuri.

Kutokana na hali hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mhe. Spika, jambo la msingi juhudi hizi zinahitaji kuendelezwa na waendeleazaji ndio sisi*(Makofi)*.

Baada ya pongezi na shukurani mbali mbali sasa nije kwenye bajeti yetu. Mhe. Spika, bajeti iliyopita ya mwaka 2009/2010 ilikuwa ni Bajeti ya Kuimarisha Miundombinu ya Kilimo na Utalii. Kwa kweli sote tulifarajika kuona kwamba serikali imeweza kuona ni kipaumbele gani ambacho kinaweza kututoa hapa tulipo na kutusogeza mbele zaidi.

Kwa kweli suala la uimarishaji wa miundombinu ya kilimo hususan Kilimo cha Umwagiliaji Maji na ile ya Utalii, ambapo Sekta ya Utalii ni Sekta Kiongozi. Kutokana na hali ile kweli tulifarajika kuona kwamba serikali imekusudia kusogea hatua nyengine mbele zaidi.

Mhe. Spika, tathmini ya suala hili katika kipindi kilichopita inaonesha kwamba tumepiga hatua kiasi, kwa sababu tumeshuhudia miundombinu hasa ile ya utalii imeimarika. Kwa mfano, viwanja vya ndege, barabara pamoja na mambo mengine ambayo yatatuwezesha au yataiwezesha sekta hii kufanya shughuli zake vizuri. Leo taarifa zinaonesha kwamba watalii wameongezeka ukilinganisha na mwaka uliopita.

Pamoja na kwamba tumepiga hatua, lakini bado hatujafikia kwenye malengo. Kwa hivyo, naomba nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, mbali ya kwamba bajeti ya mwaka huu imebadilika ambayo inazungumzia suala la Maendeleo ya Demokrasia, lakini jambo la kulipa kipaumbele miundombinu ya kilimo pamoja na utalii linahitaji kuendelezwa kwa nguvu.

Mhe. Spika, kwa mawazo yangu nilitegemea kwamba mwaka huu Mhe. Waziri pamoja na mafanikio ambayo tumeyafikia, basi atakwenda katika hatua ya pili ya uimarishaji wa miundombinu ya kilimo pamoja na utalii, yaani mawazo yangu yalinituma huko kwa sababu ni jambo muhimu.

Tunapozungumzia suala la mfumko wa bei. Kwa mujibu wa wataalamu linatokana na chakula hususani kwa hapa Zanzibar ni wali ambacho ndicho chakula kikubwa, vile vile na kitoweo. Kwa kweli huu ni utaalamu ambao umetolewa na wenzetu wa Benki ya Tanzania (*BoT*). Wakati tutakapokidhi haja ya chakula kwa visiwa vyetu pamoja na kitoweo basi mfumko wa bei bila ya shaka utashuka chini.

Mwenzangu alizungumza hapa kwamba bado wananchi wa Zanzibar wanahangaika na jambo hili, yaani chakula. Kwa kweli kipato chao wananchi wa Zanzibar hakilingani na matumizi yao. Kwa hivyo, ni jukumu la serikali kuwatoa wananchi kutoka hapa walipo kwenda kwenye eneo jengine ni njia iliyokuwa bora zaidi hili la kuimarisha miundo mbinu ya kilimo, hususan kilimo cha umwagiliaji wa maji. Kwa sababu kilimo hiki hakitegemei mvua ni kilimo bora, sasa hivi kuna mabadiliko ya hali ya hewa tumeshuhudia zikinyesha mvua zinakuwa ghamidha, likitoka jua linakuwa halina utaratibu linakuwa kali. Kwa hivyo tutakavyojiweka sawa tukaongeza nguvu za uzalishaji wa chakula kupitia miradi hii ya umwagiliaji wa maji basi tatizo hili litapungua.

Mhe. Spika, jengine ningependa nuzungumzie ni juu ya suala la bajeti halisi, tunapozungumzia bajeti ya serikali maana yake tunazunguzia suala la mapato ya serikali pamoja na matumizi, lakini pia na ile miradi ya maendeleo hata bajeti ya Mhe. Waziri imegawanyika katika maeneo hayo matatu.

Lakini haya mengine suala la matumizi na suala la uimarishaji wa miradi ya maendeleo haiwezi kuja bila ya kuwa na mapato, kwa sababu vyote hivi vinahitaji matumizi na fedha. Sasa Mhe. Spika, nilipokuwa nikiipitia bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha juu ya suala la ukusanyaji wa mapato na hatua ambazo serikali inakusudia kuzichukua inasema hivi naomba kunukuu.

> " Pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya serikali katika mwaka wa fedha 2010/2011 serikali haikusudii kupandisha kodi yoyote na badala yake mkazo zaidi utawekwa katika kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato kutokana na vianzio viliopo".

Hili Mhe. Spika, ndio limenipa mashaka kwamba tunakusudia kukusanya mapato kutokana na vianzio viliopo, hebu tujiulize. Bajeti yetu au mapato yetu ambayo tunayakusanya je yanakidhi mahitaji yetu, pamoja na kwamba tunakusanya zaidi ya asilimia tisini lakini je mapato haya tunayokusanya yanakidhi haja yetu. Ukiangalia moja kwa moja mapato tunayokusanya kwamba hayatoshelezi mahitaji yetu isipokuwa tunatumia kulingana na kile kilichopo.

Kwa hivyo Mhe. Waziri kulikuwa na haja badala ya kutegemea vianzio vilivyopo tutafute vianzio vyengine vya mapato ya serikali na tutakapopata vianzio vyengine vya mapato ya serikali tunaweza kujikwamua kutokana na hapa tulipo na tukenda katika eneo jengine, lakini pia nitumie nafasi hii kuipongeza serikali kwa hatua iliyochukua ya kutoongeza kodi ya wananchi na kusimamia ile kodi iliyopo, hii ni hatua kubwa na nzuri zaidi.

Mhe. Spika, kuna maeneo ambayo yangeweza kutusaidia lakini sijui kwa sababu gani Mhe. Waziri maeneo haya hayakupewa kipaumbele, maeneo ambayo tumeanzisha sisi wenyewe tunayaelewa na kama tungeyashughulikia yangeweza kutusaidia kututoa hapa tulipo. Mfano tumeanzisha maeneo huru ya uchumi lengo la kuanzisha maeneo haya ni kuongeza mapato na kutukwamua na kuongeza uchumi wa nchi. Maeneo huru yametangazwa tokea mwaka 1993 lakini hebu leo tujiulize tokea mwaka huo yalipotangazwa maeneo huru ya uchumi ya Micheweni na Fumba maeneo haya yamepiga hatua ngapi, yapo je mpaka sasa na tunayaimarisha vipi, jibu lake hakuna linaloendelea na ni eneo muhimu ambalo linaweza kutusaidia katika mapato ya serikali. Mhe. Spika, bajeti ya mwaka huu tumetengewa Shilingi milioni mia moja (100,000,000/=) kwa ajili ya kuyaimarisha hebu tuangalie hizi kweli zinaweza kuimarisha maeneo haya?

Mhe. Spika, eneo la Micheweni ambalo sasa hivi halina miundombinu yoyote, peke yake miundo mbinu ya maji yanahitaji zaidi ya shilingi bilioni moja kutoa maji katika eneo moja kuleta kwengine, zaidi ya shilingi bilioni moja. Sasa tunapotenga shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kuimarisha, maana yake tunakusudia nini. Kwa hivyo pamoja na hali yetu ngumu ya uchumi lakini kuna haja maeneo haya kupewa kipaumbele kikubwa ili tuone angalau kila mwaka tunaweza kuondosha tatizo moja. Kule kuna matatizo ya maji, matatizo ya umeme, matatizo ya barabara na bila ya kufanikisha haya basi hao wawekezaji watakuja kuchungulia halafu wataondoka.

Mhe. Spika, mbali na maeneo huru lakini pia kuna jambo ambalo waheshimiwa wamekuwa wakilizungumza sana hapa na naamini kila atakayesimama hapa atalizunguza juu ya umuhimu wake, suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Hili jambo ni muhimu sana na ndio maana kila mmoja hapa leo anashangaa Dk. Mwinyi vipi mbona kimya? Ilikuwaje na tulikaa tukajadili na tukatumia mawazo yetu na nguvu zetu tukaambizana na tukafika pahala tukakubaliana anasema kuna sera ya mafuta inakuja sasa iko wapi? tulitegemea serikali itakuwa na mpango kabambe juu ya kusimamia suala hili lakini ziro.

Lakini huku serikali ikilalamikia mapato sisi mwenyezi Mungu ametujaalia kutupa rasilimali hii kwa ajili ya wananchi wetu na sisi ndio viongozi tuliochaguliwa kwa ajili ya kuwasimamia wananchi. Leo wananchi wetu wana dhiki ya maisha, wana dhiki ya chakula rasilimali ipo, serikali ipo, viongozi wapo tutakwenda kuwaeleza nini wananchi na sisi ndio viongozi.

Mhe. Spika, mwenzangu amesema labda kompyuta imeruka au labda mipango haijakaa sawa lakini kwa kweli Mhe. Dk. Mwinyi tunataka uje kutueleza hapa, kwa nini bajeti yako haikuzungumzia mpango wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta kwa Zanzibar, utueleze vizuri turidhike?

Mhe. Spika, jengine ambalo nalo linaweza kutusaidia ni suala zima la kusimamia uwekezaji eneo hili tumelichagua sisi wenyewe, tulijua kwamba uwekezaji utatusaidia kuongeza mapato lakini sasa hivi inaonekana kwamba jambo hili haliendi vizuri, tuna chombo ambacho tumekiunda sisi wenyewe ambacho tunakiita *one stock centre.* Ni eneo ambalo litasimamia uwekezaji lakini leo unashangaa kwamba *one stock centre* kikao kinapoitishwa pale na ZIPA basi tunapeleka wale maofisa wa chini kabisa wasiokuwa na maamuzi. Yanaweza kuamuliwa mambo lakini matokezeo yake wakubwa wa juu wakifika kule wakayapinga yale yale ambayo wamekubaliana pale.

Mhe. Spika, siku moja Mhe. Rashid Seif alisema wazungu wanatuuliza *are you serious?* Sisi tutahisi tunatukanwa, lakini utaona kweli hatuko s*erious.* Tumeanzisha sisi wenyewe kwamba tufanye chombo hiki ambacho masuala yote ya uwekezaji maana yake yamalizike hapa. Tukiondoka hapa tukikubaliana maana yake unabakia utekelezaji. Lakini leo utakuta jambo limeshapitishwa tunarudishana nyuma. Pemba kuna miradi kama minane imeshapitishwa na ZIPA lakini imekaa mpaka leo inasubiri hati miliki ya kiwanja tu. Wafadhili wapo, fedha zipo ukiwauliza wanakwambia tunasubiri hatimiliki ya kiwanja na kiwanja chenyewe kipo kimeshapimwa bado saini ya Mhe. Waziri tu ili shughuli zianze. A*re you serious?*

Sasa haya ni maeneo ambayo yatatusaidia kuongeza mapato yetu na tumeamua sisi wenyewe kwamba tufungue milango sera za uwekezaji ili tuone kwamba tunapata mapato, mwenzangu kasema hapa kwamba kuna viwanda hapo maeneo huru ya viwanda vidogo vidogo kuna viwanda vimesimama sasa hivi vimeshajengwa eti tunakwenda tunaambiwa yule mtaalam aliyeweka hiki kiwanda kakataliwa kupewa kibali cha muda kufanya zile shughuli pale, kupewa ile *permit.* Ukiulizwa sababu hujui kitu gani kiwanda kimesimama lakini huku tunazungumzia sera ya viwanda tuongeze uzalishaji ili twende mbele, lakini mambo yanakwamba kwa sababu ndogo ndogo ndio mapato yenyewe.

Mhe. Spika, jengine suala hili ambalo linazungumzwa kila wakati suala la *Joint Financial Committee* (JFC) hili jambo lipo miaka mingi limeshatayarisha kila kitu sisi kamati yetu kila mwaka tunakwenda mpaka wale wenye kamati wamekata tamaa, mwisho juzi wakati wa kupitisha kamati tumemwambia Mhe. Waziri hebu tuletee huyu Waziri wa Fedha Mkulo, tuzungumze nae kwenye kamati tujue tatizo lake nini? Wapi tumekwama? Kwa sababu hapa ndio kwenye fedha zenyewe. Tunataka kujua rasilimali hii tunagawana vipi mpaka leo kimya? Hakuna linaloendelea, hakuna linalofanyika makabrasha na masemina tumefanya na mambo mbali mbali lakini mpaka leo miaka mitano imekwisha tunaondoka, mingine ijayo itakwisha , tutakwenda hivyo hivyo huku wananchi wetu wakihangaika kipato chao kidogo hakilingani na

matumizi. Hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini sana lakini pia tunahitaji serikali kufungua milango kwa wawekezaji waje kuwekeza tutakapofungua milango maana yake tija itapatikana.

Kuna eneo zuri pale la ujenzi wa gati kwa Afrika ya Mashariki, maeneo ya Mpigaduri, zinahitajika dola milioni mia nne kwa ajili ya ujenzi wa gati, sisi kama Zanzibar hatuwezi, lakini wapo watu wenye fedha wanaweza kujenga pale basi tufungue milango wawekezaji waje wawekeze ili tuone na sisi tunapiga hatua mbele. Lakini kwa hiki kijio tunachokusanya hakiwezi kutukwamua ni kiwango kidogo mno.

Lakini jengine la kutisha ambalo Mhe. Waziri Kivuli amelizungumza juu ya mgawanyo huu wa misaada ya kibajeti ambayo wenzetu wahisani wanatoa fedha tunaambiwa tunapata 4.5 kiwango hicho hicho tumepewa bilioni hamsini, kwenye bajeti yao kubwa wamepata mapesa chungu nzima. Lakini hii misaada yote inakwenda kule hivi hii nayo Mhe. Waziri utatwambia mnaifuatilia kwa kiasi gani hii misaada mbona inaonekana pana ujanja ujanja hapa, leo tunapewa 4.5 lakini hiyo 4.5 yenyewe hairidhishi.

Mhe. Spika, mwisho kabla ya kumaliza muda wako nizungumzie suala la *scheme of service* ambapo bajeti iliyopita Mhe. Waziri ametuahidi kwamba mwezi wa Januari yale marekebisho yote ya muundo wa utumishi serikalini na mambo mengine mengine yatakuwa tayari, sasa atwambie humu hakueleza vizuri atwambie hili limemalizika vipi na kuna hatua gani ambazo zimefikia mpaka sasa hivi? Wataalam wetu wanatukimbia na walikuwa wako tayari wanakwambia tunasubiri *scheme of service* lakini humu hatujaelezwa chochote wala hatukufafanuliwa. Nimeingia kwenye vitabu vyake hivi alivyotupa viwili safari hii katufanyia mambo ya ajabu ajabu hamna chochote kilichoandikwa humu ndio kilichoandikwa huku (*Kicheko).*

Mimi Jimboni kwangu nina tatizo juu ya suala la mfuko wa AK na JK mara zote nimekuwa nasema kwamba katika jimbo langu hakuna mwananchi hata mmoja aliyepata pasa hizi za mkopo iwe AK au JK, nikajaribu kuangalia humu katoa maelezo kwenye kitabu hiki kuhusu mfuko wa AK na JK anasema.

"*Aidha mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi wa JK na AK umetoa Tanzania shilingi bilioni moja nukta mbili kwa watu binafsi wangapi na wangapi, kaimba akisha akasema wajasilia mali Unguja na Pemba".*

Sasa nikasema hebu niende humu kwenye mapitio ya hali ya utekelezaji wa mwaka uliopita kaandika maneno hayo hayo, nilitegemea zile fedha zilizoandikwa humu ningeona zimegaiwa hivi nikaona labda wale wananchi wananidanganya, lakini aliyoandika huku ndio haya haya yaliyoandikwa

kwenye kitabu hiki cha mapitio na mengine hali kadhalika hivyo hivyo. Kwa hivyo safari hii kidogo Mhe. Waziri vitabu vyako vitatu vyote vinafanana umechukua huku ukaingiza huku, hili nalo naomba uje unieleze kwa nini wananchi wa jimbo langu hata mmoja hakupata na wameomba au wao hawana haki katika nchi hii, hizi pesa zimegaiwa wao hawana haki ya kupata rasilimali za nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kuzingatua muda niliopewa wa nusu saa umekwisha nilikuwa na mengi ya kueleza lakini la mwisho ni suala la misamaha ya kodi nakubaliana na rai iliyotolewa juu ya misamaha ya kodi, kwamba kuna haja ya kufanya mapitio juu ya kuona kwamba kodi zinazosamehewa zinasamehewa kwa zile njia ambazo tumekubaliana, kwa sababu kunaonekana kuna njia za ujanja ujanja ambazo zinatumika. Sasa mimi nakubaliana nalo sana na zipo njia za ujanja ambazo zimetumika lakini nategemea kuzizungumza kwenye bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi nitaziwacha wazi nyote mtaziona, kuna njia ya ujanja imetumika lakini leo sitoizungumza hapa nasubiri wakati wa bajeti wa Wizara ya Fedha ambayo nitazungumza.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magomeni tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia juu ya mia ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Said Kheelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi, pia sina budi kumpongeza kwa hotuba yake jinsi alivyotusomea kwa masaa mawili na nusu, pia sina budi kuwapongeza watendaji wake wote. Kabla sijasahau nasema naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Nikianza kuchangia katika kitabu hiki nimeona kwamba kuna viwanda saba na kimoja kimefufuliwa cha Mahonda, mimi nimefurahi sana kuona kiwanda cha Mahonda kimefufuliwa kwa sababu wananchi wetu wengi wa Kaskazini wanapata ajira katika kiwanda kile, lakini mimi naona huyu muwekezaji wa kiwanda hiki ana matatizo kwanza kufahamishwa huwa hataki anafanya anavyotaka yeye mwenyewe tu.

Safari moja tuliondoka na Kamati yangu tukenda Mahonda na tukatembelea bonde la miwa tulipotembelea kule tulipiga kelele sana kwamba miwa haiwekwi usafi hasa katika sehemu za mabarabara inakuwa chafu sana, sasa aliwahi kufyekea sehemu ndogo tu hivi kwa bahati siku ile tuliyokwenda sisi siku ya kwanza, siku ya pili wakatia moto wao wenyewe ukaharibu maekari ya miwa lakini salama wakati ule na wao walikuwa wanasaga ile sukari, lakini kama wangalikuwa hawasagi sukari ingalikuwa hasara sasa huku sio kufufua ni kujilisha hasara.

Naomba serikali ikae na mwekezaji huyu afahamishwe maana hata huko kiwandani mara anafukuza, mara anatoa sasa hivi ndio kufufua hivi Mhe. Spika. Pia aitwe kama kweli anataka kiwanda kifufuke basi lile bonde amalize kulima maana yake watu ukifika wakati wa kulima mpunga wanakwenda kulima kule si ruhusa lakini njaa ndio inayowapa kufanya vile, watu hawana pa kulima sasa inabidi lazima waende kule kwa kulima wakifika wanakamatwa na wanapelekwa polisi na wakipelekwa polisi wanajua Mwakilishi au Mbunge sasa sijui tuwafanye nini?

Mhe. Spika, naiomba serikali ikae na mwekezaji huyu afuate hayo masharti ya kulima lile bonde, na huko kiwandani tokea alipoanza kusaga sukari sijui ni kiasi gani kilichopatikana na hiyo sukari yake sijui ina grade gani? Mimi naomba suala hili lifuatiliwe Mhe. Spika.

Sina budi kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanza kutuletea magari ya kutengeneza barabara ya Bumbwini, maragi yameshaingia na pahala pa kuchimba kifusi pameshapatikana, njia ya kwenda kwenye kifusi imeshatengenezwa. Lakini sasa bado kazi haijaanza kwa ukamilifu isipokuwa yale magari yamewekwa tu pale hatujui magari yale yatafanya kazi lini, nilimuomba Mhe. Waziri basi angalau atutajie siku gani wataanza ile kazi kwa sababu wasituonyeshe tu kama kutupoza moyo tumechoka, juzi tu usiku imebiruka gari kwa kukimbia shimo sasa hii ni hasara kwa upande wetu. Namuomba Mhe. Waziri hili suala alione.

Mhe. Spika, lakini pia kuna matatizo kuhusu hii njia ya Bumbwini kwa sababu kwanza hapo walipotaka kuchimba kifusi wenye mashamba wamekataa, lakini tukatoka mimi na Mkuu wa Wilaya tukenda kuzungumza nao na wakakubali lakini kitu wanachokiomba serikali kwamba yale mazao kama mgomba, muwembe ambao umeambiwa una thamani ya Shs. 12,500/= mgomba Shs. 1,500/= mhogo shina moja Shs. 120/= kwa vile wanaondoshwa na pale ndipo wanapotegemea maisha yao wanaombwa angalau waongezewe bei au ile miti ikishangolewa basi waachiwe wenyewe wachukue.

Mhe. Spika, nimeshasema kwamba njia sasa hivi iko karibu na kutengenezwa lakini pia watu hawajalipwa mafao yao kwa sababu kuna wengine wanang'olewa miti yao hiyo, kuna wengine wanabomolewa nyumba sasa tunataka kujua lini wataanza kulipa hizi fidia za hawa wananchi.

La mwisho Mhe. Spika, kuhusu ukulima katika jimbo langu kumeingie ule ukulima wa mboga mboga na huu mpunga wa kuzalisha juu, kule wamepata watu wawili hii mbegu ya mpunga lakini wanasema huu mpunga wameupata wakati wa mvua nyingi sasa hawajui wakati wa kiangazi kama mbegu ile

itahimili kupandwa juu. Sasa kama itahimili basi tunaomba hii mbegu iongezwe zaidi na isambazwe kwa sababu wananchi hawana
pakulima wanakimbilia kule kwa mchina kwenye shamba la serikali, hawawezi kuachiliwa wakalima. Kwa hivyo akipata hii mbegu itawasaidia zaidi kwa kulima juu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi sina zaidi isipokuwa naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: nimeombwa niwatangazie waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwamba mara baada ya kuondoka hapa hivi saa saba, basi wana mkutano pamoja na jumuiya ya walimu Zanzibar (ZATU) hapo kwenye ukumbi wa juu, basi wanaombwa wafike hapo ili kwenda kufanya mkutano wao huo.

Waheshimiwa Wajumbe jioni tutaanza na Mhe. Abubakar Khamis Bakari, Mhe. Haji Faki Shaali. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Juma Duni, Mhe. Moh'd Ali Salim na wengineo kwa maana hiyo niwaombe hao niliowataja tufike mapema pamoja na wajumbe wengine ili tuweze kuendelea kutoa michango kwa bajeti hii ambayo ndio inatoa maduhuli kwa mambo yetu ya nchi.

(Saa. 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya jioni na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa bajeti ya serikali. Kwanza kama ilivyo kawaida yetu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kufika hapa ili kufanya shughuli hii muhimu ya taifa letu. Lakini pia ingawa kwa kidogo sana napenda niwashukuru wananchi wangu na wanachama wangu wa jimbo la Mgogoni lakini shukurani zaidi nitazielezea wakati wa Afisi ya Waziri Kiongozi ambapo ndio msemaji wa sehemu hiyo. Nashukuru sana kwa imani yao na *Ishallah* tuko pamoja wakati wote.

Mhe. Spika, katika bajeti hii kuna mambo mawili au matatu ambayo ningelipenda nipate ufafanuzi. Kwanza katika ukurasa wa 52 wa kitabu hichi kuna suala la kiwanja cha Gombani. Suala la taa imekuwa ni nyimbo ya kawaida na nyasi pia zimekuwa ni hadithi za zamani. Hii nafikiri nitaeleza sana wakati wa Wizara ya Habari, ikiwa kila siku anasubiriwa mtaalam kutia saa,

atwambie Waziri huyu mtaalam ndio kwanza yupo mwaka wa kwanza katika Chuo Kikuu na hakuna wataalamu wengine kwa hivyo tusubiri miaka mitatu au yupo wapi?

Lakini la pili suala la nyasi habari nilizonazo ni kwamba fedha hizi za nyasi zimeshakuwa matumboni mwa watu. Hii tutaielezea zaidi katika Wizara ya Habari na Utamaduni. Kuna mtu huko anaitwa Mwakalebela sijui Mwakale, nani huyu nasikia ndiyo mkorofi, kwa hivyo hili suala la nyasi kwa Gombani nafikiri kama ni ndoto. Hebu twambieni serikali habari hii tusubiri nyasi mpaka lini?

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 75 kuna hili suala la ugawaji mkopo, SMZ bado tuna asilimia 4.5. Suala hili linazungumzwa zamani na Tume imeundwa. Tume hii nafikiri sasa unafika hata mwaka wa 10 bado kila siku wanaendelea na shughuli zao. Tunapenda tujue kucheleweshwa huku na Tume hii ikaja ikasema kwa mfano SMZ ipewe asilimia 10 hii *difference* tutaipata sisi wenyewe au wanafanya hivi makusudi. Kwa sababu wana hakika na mimi nina hakika kwamba *formula* itakayokuja kwamba itakuwa zaidi ya asilimia 4.5 haiwezi kuwa chini ya hapo. Je, hii *difference* yetu tutaipata au kuna utaratibu gani?

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 76 limezungumziwa suala la uwezo wa SMZ kukopa. Mhe. Spika, mimi sifikirii kwamba SMZ inaweza ikakopa, SMZ bado imetiwa katika mabano. Haya yaliyoelezwa hapa kwa kweli ni danganya toto. Ikiwa mimi naweza nikakopa sitakiwi nende kwa mtu mwengine yeyote. Serikali ikiwa inauwezo wa kukopa ina maana serikali yenyewe ndiyo ijichukulie *guarantee*. Lakini hapa kwa mujibu wa maelezo yake kwamba serikali ya SMZ inapotaka kukopa ionane na BOT. tunaweza tukasamehe hili suala la BOT kwa sababu ndio *center bank* yetu na mikopo bila shaka tunapata *guarantee* kutokana na Benki Kuu. Suala la SMT kwamba Wizara ya Fedha ihusike je, hilo si suala lile lile la kusema kwamba bado SMZ haijawa na uwezo wa kukopa.

Mimi kidogo ningelivuta pumzi mngelinambia kwamba SMZ imeruhusiwa kukopa nje *guarantee* atakuwa ni BOT na sisi wenyewe tunaweza tukenda mwahala mwengine kama kawaida, hiyo angalau inaeleweka. Lakini ulipotia kijifungu kinachosema kwamba SMT nayo Waziri wa Fedha lazima tuonane naye. Kwa hivyo hakuna uwezo wa SMZ kukopa mpaka watu hawa wawili BOT na SMT wakubali. Kwa hivyo tuko pale pale isipokuwa tumefunikwa katika majoho ambayo tunahisi kama kwamba tuna uhuru.

Mimi nafikiri Mhe. Spika, uhuru huo haupo na SMZ haina uwezo wa kukopa kwa masharti haya. Pale ambapo ingelikuwa SMZ inaweza kukopa mimi nafikiri ingelikuwa inaweza kwenda pahala popote ikakopa wao wenyewe au

sisi wenyewe tukaji-*guarantee* na pengine BOT wakatoa dhamana nyengine. Lakini hapa ilikuwaje SMT wakaingia ndani? Kwa hivyo hiyo haina *independence* ya kukopa kwa serikali.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 83 kuna suala la (CDF). Mimi napenda niishukuru serikali na nimshukuru Waziri kwa kulizungumza suala. hili la *Constituency Development Fund*, mabunge mengi yanayo hizi (CDF) na zimesaidia sana katika majimbo na katika nchi. Ninachomuomba Mhe. Spika, kwamba hili lifanywe haraka, kwa sababu linaweza likaleta matatizo. Bunge wao wameshakubaliana kwamba (CDF) ianze na imeshaanza, sasa ikiwa mbunge katika jimbo ana (CDF) lakini mwakilishi hana, hapo panaweza pakaleta *confusion*. Lakini wanapokuwa mbunge na mwakilishi wote wana (CDF) wanaweza wakazi *utilize* (CDF) hizi kwa faida ya jimbo na kwa faida ya wananchi wetu na tunaweza tukapiga hatua nzuri. Ombi langu Mhe. Spika, ni kwamba hii (CDF) tuiharakishe ili iweze kuanza haraka.

La pili katika suala hili ambalo halikutajwa ni suala la pesa za matumizi za bajeti katika Baraza. Mhe. Spika, ni utaratibu wa kawaida na wa siku nyingi kwa mabunge mengi kwamba fedha zao zote wanapewa wao na wanazitunza wao katika shughuli za Baraza au za Bunge. Unapofanya hivyo ni kwamba lile Bunge au Baraza unalipa nguvu zaidi. Hapa tumeshawahi katika Baraza hili kutokewa na mambo ya dharura na tukawaeleza wenzetu Wizara ya Fedha lakini kwa sababu moja au nyengine fedha zile wanakwambia hawana. Kwa hivyo yale mambo yote ambayo yalikuwa yanafanywa katika Baraza yanakosa kufanywa kutokana na ukosefu wa fedha au pengine kutokana na kuelewa finyu kwa maafisa wanaohusika katika suala hilo.

Mimi pendekezo langu Mhe. Spika, lazima *Parliamentary Fund* ya Baraza iwekwe na iwe *controlled* na Baraza yenyewe. Utaratibu uliopo pale ambapo fedha zile umemaliza mwaka na zimebakia kwa. hivyo zinakuwa *roll over* katika kipindi kinachofuata baada ya mahesabu mazuri.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 92 hapa kuna mambo ambayo yamezungumzwa. Ukurasa huu unazungumzia suala zima la vivutio hasa vya kilimo. Mimi nafikiri hatuko-*serious* katika hili, kwa sababu wakulima wetu wote ni wakulima wadogo wadogo hawajawa wakulima wakubwa wa kuweza kutumia zana kubwa, zana ambazo zina utaalamu mkubwa. Wakulima wetu ni hawa hawa wa kuburura majembe ya ng'ombe madogo madogo, majembe ya kawaida haya, mbolea zilizopo za kawaida. Unaposema kwamba unatoa *exemption* kwa mashine za kuvunia au kwa zile *green houses* hizi tunatoa kwa nani? Hapana Unguja na Pemba mwenye mashine ya kuvunia wala haitakuwepo kwa sababu mabonde yenyewe ni ya heka mbili au tatu au kama yapo itakuwa ni mmoja, hakuna *green houses* labda tungekwenda Arusha huko

ambako mtu ana eka 100 kwa mfano za mauwa wale ndio wanaohitaji *green houses* hizi. *green houses* zetu sana ni kutoka hapa mpaka alipo katibu pale ukaezeka makuti basi.

Kwa hivyo hii hatukuichukulia *seriousness* hawa wakulima wetu wa kawaida hatukuwashughulikia chochote. Mimi nafikiri Mhe. Spika, hapa tungeliondoka tukatizama sana kwa wakulima suala la mbolea, majembe ya ng'ombe yale, viwanda vidogo vidogo, humo ndio kweli tungeliwasaidia wakulima wetu, lakini humu halikuzungumzwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo halikuzungumzwa ni suala la uvuvi. Uvuvi ni kitu muhimu sana kwa visiwa kwa nini hatukusema kwamba wavuvi wetu tutawasaidia kwa hili na hili. Nchi nyengine uvuvi unachangia asilimia kubwa sana katika bajeti ya serikali katika mfuko wa serikali. Mimi nilifikiria kwamba Waziri angelisema kwamba uvuvi tutaufanya hivi na hivi na huu tunatarajia kuchangia mfano asilimia 25 ya bajeti ya serikali lakini hayo hayamo.

Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo yangeliwekwa katika bajeti hii angalau sisi tukajisifu kwamba bajeti yetu imewasaidia wakulima, imewasaidia wavuvi ambao hawa ndio wanaosaidia hali ya maisha.

Mhe. Spika, jengine ni suala la mikarafuu, hili halikuzungumzwa kabisa, sasa je, hii mikarafuu haipo, haitakiwi au ndio basi. Nimalizie naona unanitizama kidogo.

Mhe. Spika, ukitizama ilani ya uchaguzi ya CCM, hii hapa ninayo. Sisi huu ndio wajibu wetu wanasheria usome kila pahala. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ukurasa wa 73 imesema kwamba:

> "Sekta za huduma ya jamii ambazo ni hususan kwa Zanzibar"

Na katika ukurasa wa 94 umezungumzia suala la kilimo, naomba ninukuu kidogo.

> "Kusimamia utekelezaji wa sera mpya ya kilimo na kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima kuendesha kilimo cha kisasa kitakachowezesha kutoa mazao mengi katika eneo dogo" .

La pili,

> "Kuendeleza kilimo cha matunda na viungo kwa kuchanganya na mikarafuu na minazi, likizingatiwa tatizo la ufinyu wa ardhi na haja ya kuongeza mazao ya biashara".

Mhe. Spika, hii sera haikufuatwa, humu hatujazungumza matunda na viungo wala suala la machungwa, machenza, ndimu na mambo kama hayo ambayo yangeliwasaidia wakulima wetu, suala la mikarafuu ndio kabisa halikuzungumzwa. Mhe. Waziri alisema katika *opening speech* kwamba anatekeleza ilani ya CCM ya uchaguzi. Mimi nikisoma ilani ya CCM hamna hayo, sasa inatekelezwa vipi? Mimi nafikiri hapo kuna kosa kubwa ambalo tulilifanya ya kwamba haya yaliyoelekezwa katika hii ilani hatukuyatizama wala hatukuyafikiria. Haya ndiyo yaliyolengwa kwa kuwasaidia wakulima wetu wadogo wadogo. Hilo ni kosa moja kubwa ambalo sera ilisema lakini bahati mbaya serikali haikusema.

Jengine katika sera hiyo hiyo ni suala la uvuvi, hili limeelezwa vizuri sana na limeeleza namna gani wavuvi wadogo wadogo wakavyosaidiwa kwa kuwapa vifaa vya aina mbali mbali ili kusaidia katika pato la taifa.

Mimi naomba Mhe. Waziri anambiye uvuvi utatoa kiasi gani katika pato la taifa. Haya ndio mambo ambayo nafikiria Waziri angelilieleza katika bajeti hii na kusema hasa tungelipata kitu gani kwa kufanya mambo haya.

Mhe. Spika, la mwisho ukitizama hii bajeti yote utaona suala la kilimo halikupewa nafasi kubwa. Suala la kilimo ukifanya kwa *percentage* lina asilimia 6.16 na sisi hatuishi peke yetu, tunaishi na wenzetu.

Kuna hii *Maputo Resolution* au *Maputo Declaration* ambayo kama nakumbuka sawa sawa ilisema kwamba kwa nchi hizi za SADC tujitahidini angalau kilimo tukipe umbele kiwe angalau asilimia 10 kwa kuanzia. Wengine wanazidi lakini sisi tumekuja asilimia sita je, tunakwenda kwa mujibu wa *Maputo Declaration* na sisi ni wajumbe wa SADEC au tunakwenda kwa ajili ya nini.

Mhe. Spika, hayo nafikiri tukiyaunganisha mimi nafikiri tunaweza tukapata bajeti iliyokuwa nzuri zaidi kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya Wazanzibari. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii kuwa mchangiaji wa pili kwa jioni ya leo. Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa rangi ya kitabu. Rangi ya kitabu kwa kweli imesadifu vyote kwa kweli hapo kidoge kenda sawa sawa.

La pili kwa moyo mkunjufu kabisa nimpongeze Makamo wa Rais Dokta Ali Moh'd Sheni, Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda na ndugu yangu Shamsi Vuai Nahodha kwa kuweza kututatulia makero sita ya Muungano miongoni mwa mamia ya makero yaliopo. Kwa kweli si hatua ndogo nafikiri katika kipindi hiki cha miaka mitano wameweza kutatua kero sita za Muungano. Baada ya

karne moja wanaweza wakatatua 60 kwa hivyo si hatua ndogo na inafaa tuwapongeze.

Jengine ambalo nataka nichangie Mhe. Abubakar na wachangiaji wengine wamelitaja, lakini kwa utamaduni wa Zanzibar usipolitaja hujachangia bajeti nalo ni zao la karafuu. Katika hotuba ya Waziri anatwambia kwamba karafuu imeshuka kutoka tani 4,007 mwaka 2008 hadi tani 3,536 mwaka 2010. Suala hili kila mwaka tunalizungumza kwamba karafuu zinashuka, mikarafuu inakufa lakini bado dawa hatujaitafuta. Jibu la mkato utakaloambiwa hapa kwamba ZSTC wanatoa miche, wanawapa wakulima bure au kwa bei nafuu. Lakini mimi nasema ile yote bado.

Mhe. Spika, mimi nadhani ipo haja tukae kitako, tujiulize huko nyuma kulikuwa na nini mpaka Zanzibar ilikuwa inazalisha tani 40,000 za karafuu kwa mwaka hata leo tukawa tunazalisha tani 3,500. Mimi bahati nzuri naishi Pemba naona mikarafuu mingi imekufa hasa yale mashamba yenye eka, mashamba yale ya eka tatu tatu ama utaikuta ishakufa au kama iko hai basi iko ndani ya pori, mtu mpaka uzae ndiyo anakwenda na panga anafekea angalau apate kukata ile mikekewe isimpapure ili apate akachume.

Mhe. Spika, hapa ninachokiona wazi wazi kwamba kilimo hiki cha wakulima wadogo wadogo katika nchi ukakitegemea hichi tu na ikawa hakuna kilimo cha mashamba makubwa uzalishaji siku zote ni lazima utashuka. Wakati wa ukoloni ni nchi moja tu nadhani ni Malawi ndio kilimo chake kilichokuwa kikubwa na uzalishaji ulikuwa mkubwa kwa kutegemea wakulima wadogo wadogo.Lakini hakuna hata koloni moja wakati huo wa ukoloni lililokuwa likizalisha kwa kutegemea wakulima wadogo wadogo wote walitegemea kilimo cha mashamba makubwa. Kwa sababu mashamba makubwa ndio unatumia *mechanization* .

Mfano mzuri angalia Zimbambwe, wao wamechukua mashamba kutoka kwa Wazungu, wamepewa Waafrika matokeo yake yamekufa, njaa imetawala sasa watu wanakula tembo. Kwa sababu mashamba yanahitaji teknojia Muafrika hana, unakwenda kumpa shamba tupu, hana mashine yoyote, hana uwezo wowote, matokeo yake mashamba yale yamekufa, uwezo wa kuzalisha hawana, njaa imetawala katika nchi. Kuna kipindi watu walikuwa wanakula tembo nchi ambayo ilikuwa haijapatapo kuingia njaa hata mwaka mmoja.

Jengine la pili ni kushuka kwa uwekezaji binafsi. Tumeambiwa vile vile kwamba uwekezaji binafsi katika ukurasa wa 53 ibara ya 53 kwamba nao umepungua. Sababu tuliyoambiwa ambayo mimi sikubaliani nayo sana kwa sababu uwekezaji katika sekta ya utalii umepungua. Ah! Sasa sisi tulikuwa tunategemea uwekezaji katika nchi kwa sekta ya utalii tu. Hoja hii mimi

hainishawishi sana kuambiwa kwamba uwekezaji binafsi umeshuka kutoka dola za Kimarekani kutoka dola 1296.8 mwaka 2008 hadi dola za Kimarekani 270.4 mwaka huu. Yaani imeshuka mno.

Mimi nadhani ipo haja hasa viongozi wanaokwenda nje, wanapohubiri huu uwekezaji basi wasihubiri utalii tu yapo maeneo mengi hapa ya kuwekeza. Lakini leo ikiwa uwekezaji katika nchi umeshuka kiasi hiki, kwa kweli kunatia hofu. Mimi najiuliza maswali iwe suala ni kwa sababu ya utalii tu au wenzetu wana na sababu nyengine. Ningeomba serikali ikafanya utafiti ili kugundua watu hawataki kuja kuwekeza kwa sababu zipi. Mimi nadhani bora tungefanya uchambuzi wa kitaalamu tukafahamu watu hawaji kuwekeza kwa sababu zipi kuliko kufanya *general statement* kama hii ambayo mimi siiamini.

Mhe. Spika, jengine pana taarifa ya matumaini hapa tumetolewa kwa kuongezeka kwa mabenki ya biashara, kiwango cha amana kimeongezeka katika mabenki lakini suala mimi ninalojiuliza hizi amana zinazowekwa ni za nani? Za mtu wa Bambi, Micheweni au Makoongwe au za nani?

Mhe. Spika, hili mimi nafikiri wala halihitaji utafiti wa kitaalamu. Siku moja mtu atoke aende hapo *Federal Bank of Middle East* hii katika tawi la (FBME), ukiangalia hasa watu wenye amana kubwa pale ni nani? Ni wageni. Ukenda (NBC) watu wenye amana nyingi ni wageni. Pesa ambayo siku moja inatoka na inakwenda kutumika katika nchi nyengine.

Mimi nadhani kuongezeka kwa amana nakuchukulia ni hatua ya maendeleo, lakini hofu yangu kwamba hizi amana nyingi zilizopo si zetu ni za wageni ambazo wakati wowote mtu anazichukua anakwenda ku-*invest* sehemu nyengine akiona hapa kidogo pana yumba yumba anahamisha mtaji wake.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba hata hayo mabenki ya biashara yakiongezeka yakawa 10 inayofaidika zaidi ni nini? Ni (BOT) . Najua kama kuna kodi za ndani tunapata lakini hasa mfaidikaji mkubwa kuwepo kwa matawi mengi kwa Zanzibar sio Wazanzibari ni (BOT) ndio inayofaidika zaidi kwa sababu ndiyo inayotoa leseni ya hawa kuweka matawi yao. Kwa hivyo inawezekana tukaona fahari kuwa na matawi mengi ya benki. Kweli Dokta Mwinyi anapata zile *taxi* ndogo ndogo laini hasa ni (BOT) ndiyo inayofaidika zaidi.

Mhe. Spika, mimi naona ingekuwa kama hizi Benki zipo vijijini kama vile Wilayani kama Wete, Mkoani ili wananchi wa kawaida wakapata kuweka pesa zao ningejua kuwa amana nyingi ni za wananchi wetu. Lakini wananchi wetu wengi vijijini bado wanaweka pesa kwenye mitungi kwa sababu hakuna mabenki, mtu gani atakayetoka Wete, Micheweni kuja Chakechake kila siku kuja kuweka pesa zake au atoke Kisiwapanza aende Chakechake kuja kuweka

pesa. Kwa maana bado serikali haijataka wananchi wake waweke amana benki. Zaidi inasisitiza watu wa mijini na wageni ndio waweke amana. Kwa hivyo amana hizi tusiringie kwani ni amana za wageni zaidi.

Mhe. Spika, jengine kuhusu suala la ajira. Tunaambiwa kwamba kuna ongezeko la ajira kuna waajiriwa (arubaini na saba elfu mia tano hamsini na moja) 47,551 kati ya hao (thalathini na moja elfu mia tatu sabini na nane) 31,378 ni wa serikali na (elfu kumi mia mbili na thalathini) 10,230 ni sekta binafsi. Mimi nazungumzia hawa wa sekta binafsi,10,230. Mhe. Spika, hawa ukiwafatilia pengine hawa mia mbili ndio Wazanzibari, lakini hawa elfu kumi wote hasa ukenda kwenye mahoteli wote sio Wazanzibari.

Sasa hapa itakuwa tunajipongeza kwamba ajira imeongezeka sawa, lakini sio kwa wananchi wetu ambao ndio walengwa. Itakuwa imeongezeka ajira lakini ukienda pale utamkuta Mkenya. Ni majirani zetu na ndio sasa hivi tunaingia katika soko la pamoja hatuwezi tukakataa. Kadiri unavyoingia katika soko la pamoja ndio ajira hizi wenzetu watazitawala, kwa sababu wao wana elimu za aina mbali mbali sisi hatuna.

Wenzetu hata ukitaka *gardeners,* wale wataalamu wa *garden* utakuta wana *degree* za mambo ya *garden* tu, sisi hatuna. Utakuta mabustani ya Baraza la Mji yamekaa ovyo ovyo tu hapa. Sasa leo hapa hata wale *gardeners* pale Baraza la Mji utakuja kukuta Mkenya kaajiriwa! Kwa sababu wao wana elimu ya kila fani sio fani moja tu. Kwa hivyo, mimi hofu yangu ni kwamba wengi ni wageni kinyume na lengo letu.

Mhe. Spika, jengine nataka nizungumzie kidogo juu ya hii *cluster* ya huduma ya ustawi wa jamii, ambayo tunaambiwa katika mwaka 2009/2010 15% tu ya makisio ndio iliyopatikana. Nimechukua hii *cluster* moja. Sasa Mhe. Spika, mimi najiuliza maswali, ikiwa makadirio yetu katika *cluster* hii ya huduma na ustawi wa jamii, mwaka wa fedha uliopita tuliweza kupata 15% tu ya makadirio, inakuwaje tena mwaka huu tunaazisha miradi mingi? Tuna miradi 94, programu 25. Mimi nafikiri si busara kila mwaka kuongeza miradi na programu nyingi wakati zile za mwaka jana mmeshindwa kuzitekeleza kwa kukosa pesa kutoka nje.

Mhe. Spika, nadhani itakuwa bora mtu kuambiwa ukate koti kwa mujibu wa mwili wako. Lakini miradi 94 mnajipangia kwa mwaka mmoja, programu 25, matokeo yake unakwenda kutekeleza pengine 12 au 10. Mwaka wa pili unakwenda kuongeza zaidi, sijui inakuwa ni nini? Mimi nashindwa kufahamu lengo linakuwa ni nini? Kama ni kujaza makaratasi tu au lengo ni nini? Lakini mimi huwa sipendelei.

Jengine zaidi ni kwamba mwaka huu katika hiyo miradi 94 ambayo nimesema imepangwa na programu 25, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe itatoa asilimia 15.7 tu, na asilimia 84.3 tunategemea wahisani. Sasa katika hali kama hii, miradi na programu hizo hazitatekelezeka. Muhisani na yeye huwa na matatizo, mara utaambiwa uchumi umedorora, mara kuna hili na hili. Kwa hivyo, kama alikusudia kukugaia 50 atakupa 10 au 15 kwa ule urafiki, kwanza na yeye anaziba kwao. Kwa hivyo, naona bajeti yetu Mhe. Spika, niseme ni kama *make sheet plans*.

Jengine ambalo hili nataka nipongeze kusema kweli katika kitabu hiki, ukiangalia kitabu cha pili serikali imesema kweli. Imekiri kwamba kuna pengo kubwa la kipato, kuna *deference* ya *disparate* baina ya umasikini na matajiri. Ni kubwa na serikali ndio inaandaa mbinu za kuondokana na hilo pengo. Hilo kwa kweli ni kitu kizuri kukiri na kuwa na mkakati wa kuyaondoa.

Lakini sasa vipi serikali imepanga kuondoa *disparate* hii? Kwanza wanasema ni kuondokana na kilimo cha kizamani na kuja katika kilimo cha kisasa. Halafu kuimarisha utalii endelevu na uwekezaji katika viwanda. Haya ndio mambo matatu yaliyofikiriwa. Lakini Mhe. Spika, suala ndio lile lile tunarudia pale pale. Kilimo cha kisasa kwa mwananchi mmoja mmoja atakiweza vipi? Kilimo cha kisasa bwana ni *mechanized*, hakiwezi mtu mmoja mmoja labda utafute mwekezaji kutoka nje, lakini kwa mwananchi mmoja mmoja hakiwezi.

Halafu uwekezaji katika viwanda. Uwekezaji katika viwanda Mhe. Spika, naona Zanzibar viwanda vyote vinavyojengwa sasa hivi ni viwanda vya maji, sisi tunataka kunywa maji tu? Inaonekana tuna kazi kubwa ya kunywa maji, kwa sababu viwanda vyote kila kiwanda unachokiona ni cha maji ya kunywa, hakuna viwanda vyengine vinavyojengwa. Basi *Inshaallah* tujitahidi jamani tuyanywe maji vizuri. Mimi naona hapa kidogo *seriousness* katika Sekta ya Viwanda haijakuwepo. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, jengine nataka nizungumzie suala la hii programu ya mageuzi katika utumishi wa umma, ambayo hii nayo nasema ni hekaya za abunuasi. Hii imekuwa kama hekaya za abunuasi, huu nafikiri mwaka wa tano tunazungumzia habari ya programu ya mageuzi ya utumishi wa umma lakini haimaliziki. Kwa hivyo, imekuwa kama hekaya za abunuasi.

Lakini nafurahi kitu kimoja tu, kuona kwamba kumbe hata Sera ya Utumishi Serikalini hakuna. Kwa hivyo, mimi nashauri hiyo sera ifanywe haraka, iletwe Barazani, inawezekana pengine huu uajiri holela unakuja kwa sababu hatuna hiyo Sera ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Spika, waziri ajitahidi, kwa sababu imekuwa ya zamani mno. Jambo hili hii ni bajeti ya sita linazungumzwa, mpango gani huo miaka sita uliokuwa haumaliziki?

Mimi nadhani bajeti hii ni muhimu, kila mmoja ana hamu asema lolote kwa wale waliokuwa saa hizi hawendi kuchakarika majimboni kwao. Kwa hivyo, mimi acha nisimame hapa nitoe fursa kwa wenzangu ili kila mmoja apate robo saa atie baraka katika hotuba hii.

Mhe. Spika, nakushukuru. Ahsante.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: *Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika bajeti ambayo Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ametuletea mbele yetu tuijadili.

Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kutokana na kuleta bajeti hii na tukawa na ya kusema. Hii ni bajeti ya demokrasia na maendeleo, kama alivyosema mwenyewe na mimi nakubaliana naye. Aidha naipongeza Serikali pamoja na kambi nzima ya upinzani kama chachu ya maendeleo yote yanayopatikana katika nchi kwa muda huu.

Yale yaliyopatikana kwa mfano, kupatikana kwa umeme Kisiwani Pemba na vile vile kuunganishwa umeme uliokuwa umeharibika Kisiwani Zanzibar, ujenzi wa barabara ya kilomita 270.5, ujenzi wa gati Zanzibar, ujenzi wa Ukuta Wesha na ujenzi wa barabara ya ndege unaoendelea sasa hivi. Pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji 141 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar ni mdogo sana kama tunavyouona na tunajitahidi kwa kila njia kutafuta njia ya kuweza kuimarisha uchumi wetu ili maendeleo yazidi kushamiri katika nchi yetu. Kwa hivyo, hatuna budi kile kidogo tunachokipata tukisarifu vizuri ili tuweze kupata maendeleo ya haraka. Lakini tukianza kufanya ubadhirifu kwa kile tutachokipata, basi kuna hatari mbele ya kukosa kabisa kabisa.

Kwa mfano, tukiangalia Wizara ya Fedha ina jengo Pemba ambalo limeanguka chini. Ule ni upotevu wa pesa za Serikali na pesa za walipa kodi. Pale inatiwa shaka kubwa sana kuona kwamba labda kuna ubadhirifu umepita au ufisadi na kadhalika. Kwa hivyo, naomba kutoa indhari kwamba mali za serikali zifanyiwe kila njia inayowezekana ili papatikane matumizi yanayostahidi na yenye faida kwa serikali na kwa wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuweza kuona kwamba kuna umuhimu wa kuunda *Zanzibar Business Council* na *Government Council* kwenye *Private Sector* inaweza kusaidia sana kuweza kuwa na mazungumza baina ya serikali na wafanyabiashara. Hii ni hatua nzuri ni ya kupongezwa na tunaomba moyo huu uzidi kuendelea.

Mhe. Spika, kwa hakika uchumi wetu hasa ni uchumi wa kisiwa. Na mimi nimefurahi sana kuona kwamba Mhe. Waziri wa Fedha wa Zanzibar katangaza kwamba yeye katika bajeti yake hakuna ongezeko la ushuru au kodi. Lakini siku ya pili yake tu, Waziri mwenzake katangaza kuongeza ushuru wa kodi.

Hicho ni kielelezo dhahiri kwamba, nchi ni moja lakini ina chumi mbili. Tukitaka tusitake, tukipenda tusipende, hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu alivyotujaalia. Hapa kuna *Island Economy* na wenzetu wana *Mainland Economy*. Haiwezekani ikawa sawa sawa. *Population* yetu ni ndogo na ni uchumi wa kisiwa na ndio maana ikawa siku zote bajeti yetu na bajeti zao hazilingani. Hivyo basi, mimi nakuwa nashauri kila siku kwamba ipo haja ya kuwa na *TRA* iwe huko *Mainland* na huku kuwe na *ZRA*. Sisi tuwe na ushuru wetu na wao wawe na ushuru wao, kwa sababu hizi ni chumi mbili mbali mbali na hayo si ajabu duniani yapo.

Hong Kong na China ni nchi moja, bendera moja inapepea, Rais mmoja, tena hawakuungana aa! Ni nchi moja ya asilia tangu kuumbwa, lakini bado wameweka chumi mbili. Kwa sababu wakichanganya ikawa uchumi mmoja basi kuna hatari ya uchumi wa Hong Kong kuanguka na kuweza kuona kwamba kazi ya miaka yote iliyofanyika pale ni ya bure.

Kwa hivyo, nasema tukubali tukitaka tuseme kwamba Zanzibar ina uchumi wake na Bara kuna uchumi wake. Kuchanganya chumi mbili hizi ni makosa kiuchumi na itakuwa tunajidanganya, tunatoa bajeti za kujifurahisha lakini baadae inaleta madhara makubwa sana. Kwa sababu wananchi wanahisi kama wamedanganywa.

Mwananchi unamwambia kwamba hatuongezi ushuru lakini baadae kesho asubuhi akienda *TRA* anakuta ushuru umepandishwa, anakuta soda imepandishwa. Kwa hivyo, anahisi kwamba labda Serikali yetu haisemi ukweli inawadanganya wananchi. Hili si jambo zuri kisiasa kwa hivyo, tungeona kuwa ipo haja ya kulirekebisha suala hili.

Jengine Zanzibar sisi kama kisiwa tuna *advantage* kubwa ya kijografia ambayo bado tumeshindwa kuitumia. Na kwa hali hiyo, tunakosa fadhila nyingi za jiografia ya Zanzibar, hasa kwenye maendeleo ya kiuchumi.

Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki cha pili cha rangi ya manjano, ukurasa wa 6 na 7 kumetokea *exemption* za *VAT* kwenye vifaa maalum vya kilimo. Wenzangu wengi wamezungumza habari hii. Mimi sina tatizo kwamba ingelikuwa hii bajeti inawapa fursa wakulima ya kufanya miradi hii ambayo itawasababisha wao waagize vifaa hivi halafu wasitozwe kodi. Mimi ningefurahi sana. Lakini bajeti nzima hii haikuhusu kabisa kwenye miradi ya kilimo ambayo inahusisha vifaa hivi.

Kwa hivyo, utakuta kazi yote hii ni *zero*, haimsaidii kwa sababu katika bajeti yetu hakuna fursa au mradi unaomfanya mkulima ahitajie mashine yoyote au chombo chochote katika hii *exemption* iliyotoka.

Mimi ningedhani kwa sababu tukiangalia visiwa vyote uchumi wao, Mauritius, Singapore, Hong Kong, visiwa vya chini ya Amerika huko, vyote vimejikita katika masuala ya biashara, vimejikita katika masuala ya viwanda vidogo vidogo na utalii. Kwa hivyo, kama kuna fursa za ku-*exempt VAT* au kusamehe ushuru au kodi nyengine, tungeangalia katika pande hizo.

Kwa mfano, viwanda. Ukiangalia katika suala la viwanda bado tunafanya masihara, ukiangalia biashara bado tunafanya masihara. Lakini nasema kwamba, biashara na viwanda vinaweza kutoa mchango wa asilimia 70 ya mapato ya nchi hii. Biashara Zanzibar imedharauliwa kabisa kabisa wala sasa hivi hapana tena biashara pana mchezo tu. Wafanyabiashara wengi wamehama Zanzibar wamehamia Tanzania Bara na wanafanya kazi zao huko raha mustarehe. Sisi tunabaki kupiga piga maji!

Kwa kweli ukiangalia katika ukurasa wa 41 kitabu cha njano, utaangalia kwamba malengo ya mwaka 2010/2011 na mikakati inashangaza sana. malengo haya sisi hayawezi hata kidogo kuimarisha biashara hapa Zanzibar, wala mikakati hii haiwezi kutusaidia.

Mhe. Spika, imo humu katika kitabu tangu mwaka uliopita katika kitabui hiki kimeandikwa kitabu cha kwanza. Kwamba kunafanywa mchakato wa kuweza kuona vipi Zanzibar inaweza ikawa *free port* katika Afrika Mashariki.

Hili ni suala pekee ambalo linaweza likafanya Zanzibar kujikwamua katika uchumi, katika Umoja wa Afrika Mashariki. Tukiweza kufanya kazi ngumu hii ya kushawishi na kuweka msimamo wetu kwamba, Zanzibar iwe *free port* katika hii Afrika Mashariki nzima. Basi ni njia moja ya kuweza kujikomboa kiuchumi, kama si hivyo tutakuwa na hali mbaya sana pindipo Kenya, Uganda na Tanzania zitakapoungana. Lakini Zanzibar ikiwa ni *free port* ikaungana Kenya, Uganda, Tanzania, Zanzibar itainuka kidedea na uchumi wa Zanzibar

utapanda *very fast*. Kwa kweli tutajiona kipindi kifupi tumeweza kupanda juu zaidi na zaidi.

Viwanda bado havijapewa umuhimu hata kidogo katika bajeti hii wala katika bajeti zilizopita. Lakini viwanda jamani vinaweza vikatuokoa sana katika nchi yetu.

Kule India walipoanza sera ya viwanda vidogo vidogo walitengeneza kikamilifu michakato yote ya viwanda vidogo vidogo, wakaiweka pale ambapo kwamba wananchi wote wa India waliitwa, wakashajihishwa kufanya viwanda vidogo vidogo. India waliambiwa mtu atakayefanya viwanda vidogo vidogo kuanzia dola 50 elfu mpaka laki moja kwanza atakuwa halipi *income tax* kwa muda wa miaka mitano, ataweza kupeleka bidhaa nnje kwa asilimia 50, atapata fedha za kigeni. Na walifungua benki ya viwanda.

Hapa Unguja pana benki 9 au 10, benki moja tu ndio yenye makao makuu yake Zanzibar, benki zote hizi hapa ni matawi tu, matawi hayawezi kutusaidia kitu sisi, mikopo ya muda mfupi haiwezi kutusaidia kitu sisi, sisi tunataka mikopo ya muda mrefu ambayo itasaidia wananchi kujenga viwanda. Tupate *Industrial Bank* ambayo itawa-*support* wananchi kukopa kwa muda mrefu kwa riba nafuu ambayo itaweza kusaidia kuweza kuanzisha viwanda.

Benki hizi zinazokuja za matawi haziwezi kumkomboa Mzanzibari hata siku moja. Panatakiwa pawe na Benki ya Kilimo, Benki ya Viwanda na Benki ya Biashara. Benki ambazo zitaweza kuwasaidia na kuwakomboa wananchi wa nchi hii.

Ukiangalia wenzetu wale baada ya kuanza viwanda vidogo vidogo hata mtu mwenye uwezo mkubwa alifungua viwanda kumi vidogo vidogo. Mtu ana dola milioni moja basi anafungua viwanda kumi vidogo vidogo ili apate kuingia katika ile *transition period* ya kupata vile visamaha. Hivyo ndivyo wenzetu wa India walivyoanza viwanda vidogo vidogo na wakaweza kuendelea leo wakawa wana viwanda vingi, vikubwa na vinaweza kuwasaidia kuleta *employment* katika nchi yao na maendeleo makubwa ya kiufundi na viwanda katika nchi yao.

Zanzibar tunayo nafasi hiyo. Lakini basi, umeme kutoka Tanzania Bara hauwezi kutusaidia viwanda vyetu. Umeme huu ni ghali na kwa sababu bei ni kubwa hatuwezi kushindana na viwanda vya *East Africa*. Lazima tuangalie umeme mbadala ambao utatusaidia wananchi wetu waweze kufungua viwanda kwa kutumia umeme nafuu.

Vile vile tukiangalia katika suala la utalii. Ukurasa wa 45 unasema, "Kuendeleza utafiti kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Benki Kuu na Idara ya Utalii Tanzania Bara, ili kupata takwimu halisi za mapato yatokanayo na wageni wanaoingia nchini". Hii ni kasoro kubwa sana, kuona kwamba mpaka leo bado hatuwezi kujua tathmini ya fedha zinazoingia katika nchi hii kutokana na suala la utalii.

Hili si jambo la kufanya mchezo kwa sababu hatujui sisi tunachokiingiza katika utalii, hatujui mapato tunayopata katika utalii, hatujui kama tunapata hasara au faida. Idadi ya watu haiwezi kutupa taswira halisi ya faida au mapato.

Kwa mfano, Mauritius katika mwaka 1998 waliingiza watalii laki moja na ushei, lakini waliingiza dola milioni mia tatu.

Sasa sisi tujiulize, tumeingiza watalii laki moja na thalathini elfu au ishirini *whatever*. Je, tumeingiza kiasi gani? Hatuwezi kujua. Kwa hivyo, hapo hatuwezi kujua faida tunayopata. Ukiwa hujui faida unayopata pengine unapata hasara lakini mwenyewe huwezi kujua. Hili suala si la kufanyiwa masihara ni suala la kufanyiwa kazi na ninasikitika sana kwamba serikali mpaka sasa hivi bado haijafanya kazi hiyo. Ukiangalia katika mikakati ya utalii bado tunatekeleza sera ya mpango mkuu wa utalii, tunataka kuchapisha kalenda, *diary*. Kuchapisha kalenda na *diary* jamani si mkakati huo bwana, kila kampuni inachapisha *diary*, kalenda na haimo katika mkakati.

Kwa hivyo, ukiangalia mikakati yote hii ni mchezo mtupu, mikakati katika utalii, katika biashara jamani tunacheza. Mfanyabiashara yoyote yule mwenye kampuni yake anachapisha kalenda, *diary*, kalamu anasambaza wala hasemi ni mambo yamo katika bajeti, masuala ya *advertisement*, lakini sio mkakati. Sisi tunataka mkakati kuona vipi Serikali yetu hii, Kamisheni ya Utalii, au Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji inafanya mbinu gani katika hali ngumu kama hii ya kiuchumi duniani kuweza kuongeza idadi ya watalii wenye kutia tija katika nchi yetu?

Ukija katika suala la vitega uchumi. Vitegauchumi vimeshuka kwa asilimia hizo tulizozitaja katika kitabu chetu hiki. Zamani tumesema kwamba, *the way how we are doing* njia tunayotumia sisi, kuwaita wawekezaji katika nchi yetu. Mambo haya ya miradi ya kupita, lazima tuwe na utaratibu au mkakati ambao utaweza kuleta wawekezaji wenye fedha sio *every Tom and Jery. Every Tom and Jery* akija hapa aah! Mwekezaji.

Siku moja tumo katika ndege tunashuka uwanjani hapa, sisi tupo *business class* tunasikia tu, tu, zogo jamaa wanapiga mbele huko, tukajiuliza kuna nini huko?

Kumbe Wahindi wanakuja na *briefcase* zao. Ah! hawa Wahindi wanatoka *economy* wanakuja huku *business class* wana kitu gani?

Ngazi pale ikateremshwa tukaona mwanzo wameshuka wao, tukakuta akina Dr. Hikman wa *ZIPA* wanawasubiri pale. Ah, kumbe hawa wanatoka *economic class* huku wanakuja kupokelewa huku kwenye ngazi ya *first class*, wametoka huko kishindo nakwambia. Hii ndio hatari! Wamekaa jamaa chini pale wanawasubiri kina marehemu Fatma Jumbe na Dr. Hikman wanawasubiri watu wanashuka ndege na ma-*briefcase* ghasia, wametoka *economy* wameshukia ngazi ya *business class* hawakushuka ngazi ya *economy*.

Hii ndio hali halisi wa wawekezaji wetu tunaowapata. Kwa sababu gani? Hatuna taratibu za kimataifa za kuona kwamba tunapata wawekezaji wenye fedha kweli watakaoweza kuwekeza kweli tukapata miradi michache lakini miradi ambayo itatoa *employment* kubwa kwa wananchi wetu na Serikali yetu ikapata tija kubwa. Lakini ikiwa tutamkaribisha *every Tom and Jery* akaja akacheza hapa itakuwa si jambo la busara. Lazima turekebishe hii hali. Kwa sababu sasa hivi uchumi unaanguka, ulimwengu wote taabani huko, uchumi unazidi kuanguka. Kwa hivyo, wawekezaji wengi idadi itashuka na itakuwa ya chini kabisa.

Vile vile tusiwasahau wawekezaji wa humu nchini. Wafanyabiashara tuwashajihishe wafanye biashara za viwanda, tuwashawishi, tuwape *feasibility study* zinauzwa, kama India wanatengeneza katika Wizara ya Viwanda wanawauzia wananchi wao dola mia tatu *feasibility study*, wananunua kila mmoja anashawishika nitafanya mradi huu na anafanya mradi na mikopo inatolewa ya mashine.

China naona wako tayari kutoa mikopo ya mitambo kwa Zanzibar, tukifanya kazi ndogo tu, basi tutakopeshwa na wananchi wetu watafanya biashara ya mitambo ya viwanda vidogo vidogo na hii ndio itakayoweza kutuokoa katika suala la ajira.

Mhe. Spika, suala la elimu. Elimu sio tu elimu watoto wakawa wanafeli tu, *Form IV* wanafeli, *Form II* wanafeli aa. Ikiwa tunataka tuendelee tuwe na *quality education*, *quality*, kama si hivyo utakuta hata ukifanya taratibu za ajira, taratibu za kuwekeza miradi mikubwa mikubwa, utakuta watu wanatoka nchi za nje wanakuja hapa ndio wanaokuwa mameneja, wanakua nani, kila cheo kwenye kampuni wanakuja watu kutoka nje, na ndio hali iliyopo sasa hivi, ikifutwa tu ile *resident permit* yake kiwanda kinakufa kwa sababu Mzanzibari hakuna ambaye anaweza kufanya kazi ile ambayo inatakiwa ifanywe.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 24 katika kitabu cha kwanza na kitabu cha kijani cha bajeti ukurasa wa 35. Mimi nilivyofahamu kwamba hiki kitabu cha pili ndio mchanganuo wa bajeti na hiki cha kwanza ndio *summary* ya bajeti. Sasa nikichukua ukurasa wa 35, idadi ya waajiriwa ni 47,551 kwa mwaka 2009 kutoka waajiriwa 41,068 kwa mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Lakini ukienda katika kitabu cha kwanza ukurasa wa 24 kinapingana, kinasema walioajiriwa ni 46,591 mwaka 2009 kutoka waajiriwa 42,053 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

Sasa hatujui tukamate wapi, kitabu hiki kina takwimu zake na hiki kina takwimu zake.

Ukiangalia katika kitabu hicho cha kwanza katika ukurasa wa 16, katika jadweli nambari 3 utakuta kuna kilimo, mifugo, viwanda, miundombinu, huduma na mambo mengine. Lakini marekebisho ni ya asilimia 12.1, hii inaonesha kwamba Afisi ya Mtakwimu inafanya kazi ambazo si za uhakika. Huwezi kuwa na marekebisho ya 12. 1, *this is too much.*

Kwa hivyo, hizi *data* zinatia wasi wasi. Mhe. Spika, mimi ningeomba mkazo ukawekwa zaidi katika bajeti yetu kuona kwamba vipi tutaweza kuboresha biashara hapa visiwani Zanzibar na vipi tutaweza kuleta *education* lakini ya *quality* sio ya kawaida tunayoifanya sasa hivi. Ni lazima tubadilike na kama hatukubadilika basi hali itakuwa mbaya kiuchumi, kwa sababu uchumi katika dunia unayumba, bado uchumi haujatulia hali bado si shwari, sasa ikiwa hao walioko huko ni taabani basi sisi tusidanganye tutazidi kumalizika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kukushukuru sana kwa uvumilivu wako pamoja na wote. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, na mimi nikichanganyika na wenzangu naomba kwanza kukupongeza kwa kunipa na mimi ruhusa ya kuzungumza. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tupo hapa tukiwa wazima, tunajadili maslahi ya nchi yetu.

Pili, naomba kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi ambaye pia ni *swahib* yangu, Mhe. Mwinyihaji kwamba ametuletea bajeti, wamesema watu kuwa ni kubwa kidogo, lakini Mhe. Mwinyihaji sisi tunaopenda kuandika na kuweka makala, husema kila ukiandika kubwa unawapa nafasi watu wakuhoji zaidi. Kwa hivyo, umetupa nafasi ya kutamba katika *documents* zako, ndio maana mzee Mazrui anatamba vitabu vitatu anaweza kuona.

Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa na sio vizuri kurudia hayo kwa hayo. Lakini vile vile mwenzako anaweza kuzungumza jambo lile lile, akaeleza kwa

hoja tofauti na ile uliyoeleza wewe. Mimi nilishawahi kuwemo katika serikali na kuhusika kufanya mambo ya bajeti, siku zimepita toka niondoke lakini kidogo nakumbuka. Bajeti yoyote ina dhamira mbili ni kwamba hiki ninachokichuma ninakitumiaje? Hata ikiwa nyumbani ni hivyo hivyo, ukishapata mshahara unajiuliza tutafikaje mwezi ujao? Vipi tutapata umeme na tutapata pesa za watoto? Kwa hivyo, bajeti haipo hapa tu, bajeti iko kila mahali. Kwa hivyo, unachuma na ukishachuma unajiuliza utatumiaje. Lakini kwanza ni kuchuma.

Sasa Mhe. Spika, ukitizama hiki kitabu tumeonesha tutachuma bilioni 444,637. Mhe. Spika, nilikuwa ninasoma hotuba ya Waziri wa Fedha wa Bara, nikatizama kwamba hizi fedha zetu zote hazitimii hata wizara moja ya wenzetu. Sasa kwa kulinganisha fedha zetu ni kidogo sana, lakini kwa hali yetu ndio tulivyo inabidi tuzigawe kwa uwezo huo tulionao. Sasa ili upate fedha inabidi ukachume, kama ni kubeba magunia, kuvua, kulima lakini inabidi ukachume.

Sasa katika daraja moja ya serikali njia moja ya kuchuma ni kujinyima leo kwa faida ya baadae. Wataalamu wanasema unavyofanya *investment* maana yake ni kujinyima leo ili keshokutwa kikusaidie. Saving maana yake ni "*to leave the opportunity of today for the benefit of tomorrow".* Kuweka akiba ni kujinyima leo kupata mkate ili keshokutwa ninunuwe mabati kumi kwa ajili ya kibanda.

Kwa hivyo, tumefanya uwamuzi serikali. Juzi tulipokuwa na Mhe. Waziri wa Fedha kwenye wizara yake pale, nilimwambia katika watu tuliofanya maamuzi ya kuweka na maeneo huru, sisi ni mwanzo kuliko Bara. Wenzangu wakasema ni tangu mwaka 1993. Sasa kuanzia mwaka 1993 mpaka leo, mara hii nimepata nafasi ya kwenda kuyaona maeneo huru bado yako huru bwana, tangu hiyo 1993 Mhe. Spika, maeneo huru yako huru.

Mhe. Mwenyekiti, wangu pale Mhe. Salmin Awadh atanisaidia, hata kufika kule kwenye hilo eneo basi ilikuwa ni pata shika kwenye zile gari. Tulipofika kule katika kuzungumza na maofisa wale, basi tulikaa chini ya miti hasa kule Micheweni. Maana yake ni nini ninachotaka kusema? Ninachotaka kusema ni kwamba hakuna moja katika udhaifu wa mwanadamu kama kufanya maamuzi asitekeleze. Bora kutekeleza ukosee utajirudi, kuliko kuamua ukabaki hivyo hivyo. Maamuzi ya kufanya maeneo huru ni ya muda mrefu, lakini hatujafanya kitu. Sasa kama toka mwaka 1993 mpaka leo, angalau tungekuwa tunasema tunajenga zile barabara zinazokwenda kule kila mwaka kilomita 2 tu, basi leo tungekuwa tuna mahali.

Mhe. Spika, huwa ninawafurahisha wenzangu tunapokuwa kwenye kamati. Samahani kwa kutoa mfano wa kwenda kwenu Mhe. Spika. Unapokwenda Makunduchi ukifika pale Kibele unaliona posi la umeme kulee liko mbali,

halafu unalipita mwiiii! Halafu unaanza kulitizama jengine hivyo hivyo, basi unajikuta uko Makunduchi. Kwamba kila muda ukipita kama ulikuwa unafanya kidogo kidogo, basi kuna siku unaweza kusema leo nimefika hapa. Lakini kama hufanyi, inakuwa kama wale wanajeshi katika mchaka mchaka wanatikisha kwanza miguu, hatufanyi tunaamua tu tuko hapa hapa. Kwa hivyo, hii ni moja katika udhaifu.

Mhe. Spika, kuna lile dudu linaloitwa *ZIPA*, yule Mkurugenzi tulipokutana naye, majonzi yake na masikitiko yake nilimuonea huruma, kazi yake ni kuvutana na mabarua wanabishana wenyewe kwa wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, wangu asubuhi alisema ni *one stop center*. Mimi nilikuwa nasema hapana, ni *one center to stop everything.* Yaani badala ya kwamba ukifika pale mambo yote yaishe, lakini yakifika pale yote yanakwama. Mwenye matatizo, yule barua ya *immigration* hataki, tena mara hii katupa *copy* za barua ukizisoma utafikiri hizi ni barua za serikali au ni za watu binafsi. Sitaki, alaa! Wee kwani ni ya babu yako hiyo afisi? Ni kitu kidogo lakini kinasikitisha kwamba kuna matatizo. Kwa hivyo, hilo ni la kwanza ambalo nilitaka kusema kwamba tukifanya maamuzi basi tufanye, hata sekta ya ujenzi wa barabara ambayo nitaeleza baadae au miundombinu, ingekuwa ile *center* ya barabara na miundombinu, katika kule kujenga kwakwe barabara ikawa inaoneshwa na ile maeneo huru basi ingekuwa unaona kwamba barabara zinajengwa kwa mashirikiano kuwa na maeneo huru yanaimarika. Au katika kuweka umeme, ikawa ule umeme katika mipango yao unaimarishwa, lakini kila mmoja anafanya lake sio vizuri.

Mhe. Spika, katika kutafuta fedha kuna njia za kuwekeza ndio hizo tumesema na wenzangu wamejaribu kusema sana. Lakini kuna njia za kodi na mapato. Sasa mashirikiano yetu na ndugu zetu Bara, walituambia tusiende kwenye *OIC*, Mhe. Spika, walituambia watakwenda wao, wakienda wao maana yake ndio tutafaidika na sisi. Wao hawakwenda na sisi hatumo. Sasa kama kweli ni ndugu wanaotupenda basi angalau wangesema kwamba hapana nyinyi msiende hiki mnacho kihitaji basi tutawafidia, ndio undugu huo wenzangu. Usilime hapo mwaka huu, lakini mzee sina chakula mimi basi nitakupa pesa. Usiende *OIC*, lakini jamani bajeti yetu hii tunatafuta misaada, hapana usiende nitakwenda mimi. Lakini mheshimiwa nina *deficit* ya bilioni 5, basi nitakupa. Hakuna neno, wenzetu wanajua zaidi.

Suala la *JFC* limezungumzwa kwa urefu. Mhe. Spika, tangu mimi niko serikalini suala hili linazungumzwa, kiasi miaka 18 au 20 nyuma au zaidi. Nilikuwa na Mhe. Salmin wakati ule ikaundwa kamati ikiitwa Salmin *commission.* Namkumbuka rafiki yangu Frigen Kazaula, mimi nimekaa huku na yeye amekaa kule tunashindana kitaalamu, Mhe. Rais Nyerere Marehemu

Mungu amrehemu huko aliko alikuwa yu hai. Akapelekewa *report* kuhusu mambo haya, mpaka leo hayajesha.

Bahati mbaya Mhe. Spika, suala hili la *JFC* ni la kikatiba na limetajwa katika kifungu cha 133 na Mhe. Waziri kakitaja humu. Moja katika kitu ambacho watu husisimkwa na mwili ukikitaja ni unapotaka kuvunja katiba. Hiyo ni kinyume na katiba, hasa wenzetu dhidi yetu. Usifanye hivyo, katiba haisemi hivyo, hii ni kuvunja katiba. Hili tangu mwaka 1977 limo kwenye katiba inavunjwa ndugu zangu katiba. Imekwenda imeunda hiyo *commission* imepitishwa sheria wakubwa wanakutana. Mwisho tukamwambia Mwenyekiti, tuitie waziri. Akasema simpati, nikamwambia mtengenezee semina aje atuhutubie labda tutapata kusema naye.

Mhe. Spika, hili ni moja kati ya yanayotunyima mapato mengi sana. Shahidi ni wenzangu tulikwenda kwenye ile afisi ya wale vijana, hiyo afisi inayoitwa ya *JFC*. Sio siri walisema jamani tumechoka maana hakuna adabu mbaya kama kukaa bila kazi. Mhe. Spika, tusiombe, umeamka asubuhi umekaa kitako pale, mchana unaletewa chakula mpaka usiku, wiki moja tu basi utaona kama labda ungefungwa, kukaa bila kazi ni kifungo kikubwa kuliko kufanyakazi. Wale wanasema mzee tumekaa tu hapa asubuhi tunaamka tunapanda daladala tunakuja hapa tunaandika nyaraka, zinapelekwa kwa wakubwa hakuna jibu. Mhe. Spika, nadhani hili linahitaji kushughulikiwa kama sisi ni ndugu.

Maana kinachofurahisha basi Kenya, Uganda na Tanzania Afrika ya Mashariki ilikufa imefufuka. Wenzetu Rwanda na Burundi wameona nzuri wamekuja, Muungano uko zaidi ya miaka 50 hakuna waliosogea, tuko sisi wawili tu. Sasa pengine ni kwamba wanashindwa kupata *confidence* ya kuona kwamba mbona hivi na sisi ni ndugu, tunachotaka sisi ni kwamba tufaidike sote, kasema Mhe. Nassor Mazrui hapa. Sio kwamba labda kunataka mmoja awe hivi na mwengine awe hivi, hapana tukinufaika sisi na wakinufaika wao ni vizuri. Kwa hivyo, lile lenye faida lingefanywa.

Mhe. Spika, nije kwenye bajeti, ili nisipoteze muda niwape na wenzangu nafasi. Nilichukua vitabu tulivyopewa na kuonesha zile *allocation*, nikaiweka bajeti ya kawaida, nikaiweka na bajeti ya maendeleo na nikaweka na jumla, sikufanya kazi kubwa, jumlisha na toa. Nikapata bajeti ya mwaka huu nambari moja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 21 bajeti nzima hii, nambari mbili Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, nambari tatu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Huwezi kushangaa moja au mbili ni zile zinazoitwa miundombinu na hii moja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kwamba watoto wetu wasome. Lakini nambari nne ni Wizara ya Fedha na Uchumi, nambari tano ni mfuko wa serikali, nambari sita vikosi na nambari

saba kilimo. Hapana, sitaji zote Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji nambari 12.

Mhe. Spika, kuna mambo mawili, kuna sekta za kiuchumi na sekta zinazohudumia uchumi. Ndio zile zinaitwa *cluster one* na *cluster two*, maana hili neno *cluster* nimelikuta humu ndani sijalizowea, hivyo nikikosea niambieni. Lakini kilimo, Mhe. Abubakar alisema hapa imepewa 6 na ilitakiwa ipate 10. lakini sekta ya biashara mmesema kwamba huku ndio kuna mambo mangapi? Kuna utalii, viwanda, uwekezaji yote ni mambo muhimu. Utalii tumesema ndio sekta kiongozi, kwa hivyo haiwezekani sekta kiongozi wizara yake nzima ikapata 1.01 bajeti ya nchi, kunaweza kuwa na maelezo.

Sasa nikafanya zoezi jengine. Nikachukua bajeti ya maendeleo, nikachukua hizo *cluster* mbili za uchumi na huduma, nikaichukua mawasiliano, kilimo na biashara kama ni kundi moja. Nikaichukua na maji, elimu na afya kama ni kundi jengine halafu nikazi *rank*. Nambari moja ni wizara ya maji, nambari mbili wizara ya mawasiliano, nambari tatu wizara ya elimu, nambari nne kilimo, nambari tano afya na wizara ya biashara nambari sita.

Mhe. Spika, wataalamu wa Mhe. Waziri wananisikia hapa, sio kwamba nakejeli hivi, hapana. Najaribu kuonesha kwamba tunapozingatia lipi muhimu na tunataka nini tujinyime leo, nilianza mwanzo kwenye mjadala wangu kusema hili, kwa faida ya kesho, lipi muhimu. Sio lipi muhimu tu Mhe. Spika, lakini katika huo umuhimu katika miaka miwili au mitatu hii acha nyengine zipate tabu kidogo, lakini kesho tujione kwamba tumepita *pole* mbili na tumepita *pole* tatu. Moja katika kosa kubwa ambalo tumefanya katika mipango yetu, zamani kulikuwa na mipango ya muda mrefu, muda mfupi na ya kila mwaka. Tulikuwa tunajiona tutafika kule baada ya miaka mitano, tutafika hapa baada ya miaka miwili na mwaka mmoja tutafika hapa. Kwa hivyo, ulikuwa unajua kwamba naelekea huku, tunahitaji kujirekebisha kwa hilo. Mimi nina lugha moja huwa nasema hatujachelewa.

Mhe. Spika, mimi sio mtaalamu wa afya, lakini nikimuomba Waziri wa Afya kuanzia leo nikasome *nursing*, nina hakika baada ya miaka mitatu naweza kuwa *nurse* mzuri. Lakini nianze leo. Kwa hivyo, tufanye maamuzi ili sisi tutakapokuwa tunachukua hiyo pensheni ya 25 basi tuweze kusema kwamba lile tulilifanya sisi tuongezeni angalau ifike 30.

Mhe. Spika, naomba nimalizie na misamaha, sitaki nichukuwe muda wako mkubwa maana kuna hatari. Mhe. Spika, misamaha imezungumzwa hapa. Wamesema hapa kuwa sijui sisi tunaweka makuti tu. Mimi natoka katika familia ya wakulima na wavuvi, baba yangu alikuwa mvuvi Mwenyezi Mungu amrehemu na mimi kama anavyoijua Mhe. Haji Kheir bahari naijua kidogo,

tunaweza kushindana hapa na Bawe kwa kuogelea. Kama tungeamua kusema tunataka kusamehe, basi tungesamehe vifaa vya uvuvi. Hawa kina Juma Duni na jamaa zake wenye viboti.

Mhe. Spika, nimejaribu kuweka hesabu Mhe. Spika, ili upate mtego wa dagaa unahitaji mapande sita ya nyavu. Pande moja ni milioni 1,200,000/=. Mhe. Ame Mati Wadi nisaidie. Kwa hivyo, kwa yote sita ni milioni 7,200,000/=, hujapata *engine* ya boti ambayo haipungui milioni 7,000,000/=, hujapata ile mashua yenyewe, hujapata vitu vinaitwa vidinge, hujapata karabai na vidudu vingine kamba za kuvutia, ili upate mtego ule wa dagaa tu, basi sio chini ya milioni 20 mpaka 25. Sasa kama tunafikiri kumsaidia masikini, basi katika kusamehe tungedhania kusamehe watu hawa. Basi dagaa lingeongezeka bwani japo tonge kwa tonge na vibua vingeongezeka. Lakini uwezo wa maskini kupata mgego wa uvuvi ni ghali mno.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kitu kimoja. Wakati fulani nilikuwa kwenye *workshop*, akaja mtaalamu mmoja akatupa picha ya farasi imekatwa vipande kama vitatu au vinne hivi. Kipande kimoja kimeelekea huku na kipande kingine kimeelekea kule, yaani kila kimoja kimeelekea kwake, akasema hebu mpange huyo farasi mpaka umuone kwamba anatembea. Mhe. Spika, alipatikana mmoja tu. Kwa nini alipatikana mmoja. Kwa sababu mazowea ya akili kwamba farasi atakaa hivi na atatembea hivi, kumbe yule jamaa alikua kamweka aonekane kama anaruka ukuta, kwa hivyo alikuwa kakaa hivyo, sio rahisi hatukumuona bwana, alitokea mmoja tu.

Maana ya kusema hivyo Mhe. Spika, nisichukuwe muda wako mkubwa ni kwamba tunahitaji kufikiri nje ya boksi, tunafikiri kimazowea mambo vile vile. Tunahitaji kubadilika, tufikiri kidogo nje ya yale tunayofanya kila siku ili tupate mwamko mpya. Kuna mtikisiko wa dunia, kukitikisika watalii hawaji, lakini sio kutikisika watalii hawaji tu, tunajua hapa historia yetu jamani, siku wanaambiwa tu leo CUF wanaandamana, wanasema hee! Kwa hivyo, sio sekta ya kuitegemea. Lakini sio nje tu, mambo yakiharibika Bara hapo tu, tumeyaona kwenye bajeti ya jana tu, inamugharimu mnywaji soda wa darajani. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo, nakushukuru sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsnte Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti kuu ya serikali kwa wakati huu wa jioni, nikiungana na wenzangu walioanza tangu asubuhi. Kwanza nimshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna na watendaji wake wote ambao wameandaa bajeti yetu hii ya mwaka huu na kuipa jina la bajeti ya demokrasia na maendeleo. Jina zuri na bajeti imepangika vizuri.

Mhe. Spika, nitakuomba uniwie radhi kwamba yapo mambo yamezungumzwa, lakini na mimi nitayazungumza na niyatolee mawazo kwa upande wangu, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo niingie kwenye bajeti moja kwa moja. Kwenye ukurasa wa 83 kifungu cha 155 mfuko wa maendeleo ya jimbo *CDF*. Wenzangu wamezungumza na mimi naomba nizungumze, halafu nitowe mawazo yangu. Kwanza naipongeza serikali kwa kutoa wazo hili ambalo tayari wenzetu wabunge wameanza kuutumia mfuko huu na sisi yanafanywa maandalizi ya mwisho ili tuweze kuutumia. Sio jambo baya ni jambo zuri.

Ushauri wangu ni kwamba Mwakilishi na Mbunge ni viongozi wa jimbo wanaoongoza katika eneo moja. Tunavyoona sisi pamoja na wananchi wengi kwamba mbunge na mwakilishi ni watoto pacha, sasa naomba na serikali hilo ilizingatie. Kwa sababu ikiwa watoto wamezaliwa pacha mmoja ukamshonea suti na mmoja ukamtafutia mitumba, kwanza unamdhalilisha, halafu vile vile hawatofikia ile dhamira waliyokusudiwa. Maana ya kuzungumza hivyo ni kuwa wenzetu wana kasi kwa kwenda, sisi tunatambaa, lakini mnataka mtuchanganye, tutafika kweli. Nadhani Mhe. Waziri uje ulijibu swali hili.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema hivyo. Kwa sababu wenzetu wameanza afisi zimesha jengwa, sisi tunaambiwa utaratibu utafanywa, lakini kwenye bajeti sikuona. Hii *CDF* wenzetu wameshafanya, sisi tunaambiwa inaletwa sheria. Sasa ningeshauri kwamba hiyo sheria inayoletwa, kwa sababu sasa hivi wenzetu imeingia moja kwa moja katika mfuko, kwa sababu wenzetu ni wajumbe kwenye Halmashauri za Wilaya, sisi kwetu hatumo, wenzetu wamo kabisa kwenye sheria, pesa zimekwenda zimewakuta tu. Sisi mpaka mfanye sheria tutiwe kwenye Halmashauri, halafu tuingizwe kwenye huo utaratibu wenyewe, muda utakuwa mkubwa. Lakini cha msingi zaidi kile ambacho wanatiliwa wao na sisi kitalingana. Tungeomba serikali ituambie kabisa ili kuondosha huu utata, wenzetu wameshatiliwa milioni 25 huko, sisi tukitiliwa milioni 16 haijii.

Kwa hivyo, kama mnataka twende sambamba kama watoto pacha, basi mkashauriane na wenzetu Bara kabisa. Ee! Bwana milioni 25 nyingi wekeni milioni 10 au 50 ili twende pamoja na hii ni sawa sawa na mfuko wa AK na JK zimekwenda pamoja. Kwa hivyo, naomba na hili tusilifanyie haraka, kama bado tuambiwe tu bado ili tujigandize huko kwa mbunge kama tunavyojigandiza sasa hivi kwenye afisi, kama bado tuambiwe bado, basi tutajiweka ubavuni kwa mbunge twende hivyo hivyo na Mwenyezi Mungu atatusaidia. Kwa hivyo, naomba na hili Mhe. Spika, limekuja kwa nia nzuri, lakini liende kwa utaratibu.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa mwengine wa 50 kifungu cha 94 uwezeshaji wa wananchi. Tunawashukuru marais wetu wote wawili wameleta mfuko huu, lakini huko nyuma pia ilikuwepo mifuko mingine mbali mbali ya TASAF, mfuko wa kujitegemea na mifuko mingine ambayo ilisaidia wananchi katika kuwatoa katika umaskini. Hapa pia kumetokezea tatizo, mfuko ulivyoletwa na tulivyoufahamu sisi pamoja na wananchi ni vyenginevyo. Tulitegemea kuwa yule mwananchi mnyonge ndio utamsaidia mfuko, lakini sivyo ilivyo. Wale ambao wanacho chochote ndio waliopata mfuko ule na ndio unawaendeleza. Sasa huyu mwananchi wa chini atazidi kwenda chini zaidi.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba nitowe ushauri kuwa hapa paliposalia kwa huko tunakokwenda kama ni ushauri mzuri basi ungefuatwa. Kwanza kwa wenzetu huu mfuko unatolewa na watu wa mabenki, benki kuna taratibu zake. Benki suala la mwanzo ukishajaza karatasi ile ambayo mnapewa na masheha katika maeneo unasema mimi nitafuga kuku wa nyama elfu mbili, banda langu vyumba sita na chakula kiasi fulani, wale wanakuja kuangalia kweli hilo banda unalo na hao kuku umeshaanza kufuga ili upewe pesa uongeze. Sasa tofauti na wananchi walivyofahamu wananchi wanaona kwamba labda sawa sawa na serikali inatayarisha *writeup* ukauza ikanunuliwa.

Mimi nina mtaalam wangu ataniandikia mradi nafuga mabada ishirini. Kuku mia nne banda la vyumba vitano nahitaji milioni tano, kama *writeup* imekaa vizuri nipewe nijenge banda. Ninunue mabata, kuku na vyakula nitie, lakini ukiwambia watu wa fedha, wanakwambia sivyo ilivyokusudiwa, utuonyeshe ulichonacho halafu uandike sisi tukupe. Kwa hivyo tutawasaidia wale wale wenye kitu na wanyonge haiwasaidii.

Sasa naomba serikali ikakae upya itizame na hayo mawazo ya wananchi.Kama mtu mwenye biashara ndio apewe mkopo basi hatuwasaidii wanyonge. Mnyonge unaweza kutayarishiwa *writeup* ya kuweza kufanya mradi kama duka, kuku, ng'ombe ipitishwe halafu atafutiwe ng'ombe afuge, waone kama hakwenda mbele kama wenziwe. Lakini tukisema wenye mradi tu wapewe mfuko itakuwa tumeutafsiri vibaya naomba uelezwe tena wananchi waufahamu na wajenge imani kwetu sisi. Kwa sababu sasa hivi wale ambao wamekosa wametoka imani na sisi hatukufahamu kama ni hivi, tungewaelekeza.

Kama nia ya kusaidia wanyonge ipo basi yule anayeandika *writeup* na watalaam achukuliwe afanye ule mradi si lazima awe nao. Kwanza, kwa upande wa mfuko huu na hilo tunaomba serikali ifanye utaratibu mpya ili mtu anayeweza kubuni mradi akaandikiwa na akasimamiwa basi fedha apewe ili ziweze kumsaidia. Lakini kwa kutafuta mwenyewe mradi afanye pesa hana itakuwa halikufikiwa lengo lililokusudiwa. Kwenye mfuko huo ushauri wangu

ni huo na kama serikali itaona unafaa basi tungeufuatilia tukaona yale malengo tuliyokusudiwa yanafikiwa.

Nije mchango wangu wa tatu ukurasa wa ishirini kifungu thalathini sekta ya kilimo, tumezungumza kwamba kilimo ni uti wa mgongo pamoja na yote sekta kiongozi utalii, uvuvi lakini kilimo tangu tunafungua macho ndicho kinachotusaidia. Lakini bado mpaka hivi sasa serikali pamoja na wataalam wote tuliokuwa nao hatujaenda kulima kilimo cha kisiwa tunalima kama watu tuko bara wakati eneo letu dogo. Sasa ningelishauri mambo yafuatayo:-

Kwanza tungekipa kipaumbele kilimo cha kumwagilia, kwa sababu mfano mdogo tu mpunga wa kumwagilia unachukua miezi minne. Kama utalima kwenye shamba moja katika mwaka utalima mara nne lakini sasa hivi tunalima mpunga wa kungojea mvua na kwa mwaka tunalima mara moja eneo dogo tutaagizia chakula siku zote. Sasa nashauri kwamba mabonde yote ambayo yanaweza kufanyiwa *irrigation* yangefanyiwa mtu baada ya kulima mara moja kwa mvua atalima mara nne kwa mwaka mmoja. Kwa hivyo atapata kipato cha kuuza na chakula mwenyewe nadhani hili tunalizungumza muda mrefu.

Pia tupange wapi? Tunalima na wapi? Tunajenga na wapi viwanda ? Kwa sababu sasa hivi imekuwa ni uvamizi tu. Bonde langu la Chuini sasa hivi linamalizika kwa kujengwa na lilikuwa tunalima mpunga. Tunazalisha miwa na mboga mboga na wahusika wanaona bonde la mpunga. Tunajenga majumba na si hilo tu yapo mengi tu. Kuna sehemu nyingi za kilimo wameshajenga watu, sasa tukifanya hivi hata huo mpunga wa kulima mara moja tutakuwa hatuupati.

Serikali ipange wapi tunalima? Wapi tunajenga? Wapi viwanda ili twende uzuri na sisi wakati wataalam tunao? Lakini zaidi umwagiliaji ufuatiliwe na si kwa mpunga tu lakini migomba ukimwagilia inakuja vizuri, matango ukimwagilia yanakuja vizuri na mboga mboga zote. Naomba na hili serikali ikae iweke utaratibu mzuri. Mabonde yote ambayo yanaweza kumwagiliwa basi tumwagilie ili tuweze kuvuna mara nne kwa mwaka, badala ya mara moja itaondosha uagiziaji na mwaanchi, atapata chakula na atapata kuuza.

Mhe. Spika, jengine ni suala la matrekta tunashukuru kwamba yamenunuliwa matrekta 45 na kwa tathmini ya wataalam ni kwamba tumefikia 83%. Lakini tujiulize wangapi wanalima kwa matrekta? Takwimu haipo wala hatuijui? Sasa naomba zikija takwimu kama hizi ziwe wazi, tumenunua matrekta kiasi fulani lakini waliolimiwa ni idadi fulani, idadi fulani wanachangia na idadi fulani serikali inasaidia hii inaweka wazi mtu kuona vipi tunapiga hatua kule tunakokwenda. Sasa na hili pia tungeliliomba katika takwimu zinazotolewa tukaliona linaweza kusaidia katika utekelezaji wa sehemu ya kilimo.

Mhe. Spika, nije sehemu ya nne Ukurasa 40 kifungu 74 (c) hapa inazungumziwa mpango wa muda mrefu wa kujenga njia mpya ya umeme unaotoka bara kuja Unguja, tunashukuru kwamba tatizo lililotokezea limetufunza tujenge laini nyengine. Lakini hapa hapa tulizungumza kwamba laini hii mradi umesainiwa hapa imeelezwa kwenye kamati yetu au bajeti hii Mei, 2010 lakini mradi utakwisha 2012 tukazungumza kwamba ni muda mrefu wakati tuna dhiki, tukaambiwa kwamba serikali itafuatilia hao wenzetu wanaotusaidia wapunguze angalau badala ya miaka miwili iwe japo mwaka mmoja na nusu. Jibu kwenye kitabu sikuliona labda Mhe. Waziri kama utakuwa nalo wakati wa majumuisho naomba tulipate, lakini pia imesema tayari kwenye maeneo wameshafanyiwa watu tathmini na mradi *time* yoyote unaweza kuanza, sasa tathmini hizo ningeomba zikafanyiwa tena uhakiki kwa sababu wanasikitika mtu mwenye kibanda cha *kiosk* na mtu mwenye nyumba ya kawaida *kiosk* ana milioni ishirini, nyumba ya kawaida ana milioni kumi na tano sasa hayo yapo sisi tunaokaa mitaani tunasikia.

Naomba kama walifanya wao mradi tathmini hiyo na sisi tutie mkono wetu kwa sababu wakitoa wao pesa ndogo lawama zije serikalini itabidi tufidie sisi, sasa kabla hazijatoka wende wataalam wahakiki tena ni kweli au mazungumza ya mikahawani tu, mtu ana kiosk cha kuuzia soda na mwengine ana nyumba ya familia sita wanakaa *kiosk* pesa nyingi nyumba pesa kidogo. Sasa na hili kabla mradi haujaanza naomba tungesaidiwa ili kupata kujua ni kweli au watu wanaengezea tu katika mambo hayo, nadhani tukipata jibu na sisi tunaweza kuwaelezea wenzetu.

Mhe. Spika, nije uk. 58 kifungu 112 Takwimu. Nashukuru sana baada ya kuona takwimu zimepewa maelekezo mengi humu lakini nisikitike kwamba takwimu hatuzitumii inavyotakiwa serikali pamoja na jamii na taasisi na nitatoa mifano miwili. Kwenye kitabu nitaomba ninukuu Uk. 50 kifungu 112 kinasema.

" *Ukurasa 58 kifungu 112 kinasema kwamba katika mwaka wa 2009/2010 zimefanywa kazi za utafiti na tafiti ya mwanzo ilikuwa juu ya mapato na matumizi ya kaya, sensa ya kilimo, sensa ya uzalishaji viwandani, utafiti wa hali ya hewa na chakula, utafiti wa afya ya mama na mtoto ziko nyengine".*

Mimi nataka nizungumze mbili tu utafiti ukifanywa na serikali unataka ujue tunakwenda mbele au tumebaki pale pale mfano matumizi ya kaya, pengine imeonekana kaya moja kwa mswahili anazaa watoto saba kwa mwezi anatumia laki tano lakini anazalisha laki moja atakwenda anavyotakiwa, sasa serikali ishaona vile ipendekeze mbinu ya kuweza kufikia yale mapendekezo yaliyotolewa ndani ya ule utafiti. Mfano imeshaonekana watu sita kwa uzazi wa kimasikini ni mkubwa sana tushawishi watu nyota ya kijani wafike watoto wanne tunafikia yale malengo yaliyokusudiwa pale afya atapata na atasoma

vizuri, lakini tukisema kila mtu aje na riziki yake ndio atazaa kumi na sita au kumi na nane sasa itakuwa zile tafiti zinafanywa lakini zimo ndani a mafaili hazifanyiwi zile hatua zinazokusudiwa.

Naiomba serikali tafiti kama zile za kaya wakishaziona na wakishaona tatizo lipo basi watu waelimishwe ili tuondoe hilo tatizo lakini ikiwa tafiti zimo ndani ya mafaili tutakuwa tunatoa pesa tu lakini faida haipatikani, hii tafiti ya kaya imeshapita mwingi hii sasa tutizame je tufanye njia gani tuende huko tunakotaka, tupunguze uzazi au tupunguze mengine. Sasa naomba na hili Mhe. Waziri lifanyiwe kazi tujue.

Lakini nyengine tunaambiwa kuna tafiti ya mama na mtoto tunakubali sasa hivi vifo kidogo vimepungua lakini bado watoto wanafariki, na kinamama pia wanafariki tatizo nini tulisikia labda wanatozwa fedha wakati wa kujifungua inaonekana ni tatizo watu wanazalia majumbani *operation* elfu arubaini haijaondoka, sasa tunatizama tafiti zinavyosema halafu serikali inachukua hatua hapo tufafika pale tunapokusudia kwenye watu mia labda atakufa mmoja halafu itafika mpaka hafi mtu kwa sababu hawatoogopa serikali itakuwa ni ya bura, kuliko kule kwenda na uzi, kiwembe inakuwa unakwenda kushona tena, sasa kuna mambo lazima serikali ipige kufua sisi wanaume sio wazazi lakini pesa tunawapa sie wale wanawake kwenda kule, kwa hivyo kwenye uzazi na sisi tumo hatuwezi kutoka. Sasa naomba tafiti kama hizi zikishakufanywa yaondoshwe haya matatizo yaliyoonekana lakini tafiti ikisha inatiwa kwenye sanduku akitaka mtu inatafutwa.

Mhe. Spika, hata hali ya hewa hakuna wakulima wanaotafuta hali ya hewa sasa hivi au wavuvi inasaidia kuwaambia kwamba leo kumekaa vibaya msiende lakini hakuna mtu anayefuatilia mambo ya utafiti na takwimu, sasa naomba na hili lifanyiwe kazi ili tufike kwenye malengo.

Mhe. Spika, mwisho nije kwenye suala la wenzangu walilozungumza mimi niko kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na nilifikiria sana nilipokwenda kuangalia maeneo huru hasa ya Micheweni, hivi sasa Micheweni kama hatukwenda kugawa tukasema huku kwa maeneo huru huku watu wachimbe tofali basi eneo lote litamalizika. Kwa hivyo tunashauri serikali iende ikaone kwa kuwa wananchi wanaona kitega uchumi watapata ajira na hazipo wameamua kuchimba ile ardhi yenyewe na imeshachimbwa eneo kubwa na hawasikii hata ukiwaambia, wakuu wa wilaya wameshasema, wakuu wa mikoa wameshasema wanasema sisi tutaacha kuchimba kama itakuja ajira maana ndio tunamopata kula, sasa kama hatukwenda kupima matofali chimbeni huku na huku ngojeeni hizo ajira kutamalizika.

Lakini upande wa kwetu Fumba watu wanajenga majumba sasa akija muwekezaji itabidi yule mtu afidiwe aondoke akae muwekezaji itakuwa ni yale yale tutakosa mtoto na maji ya moto, maana kama hukuzaa maji ya moto ya nini tena sasa tunaomba na hili kwa Fumba litizamwe watu wasijenge kumevamiwa sana Mhe. Waziri umeshakwenda, tuwaambie mwisho hapa kule tena msijenge ili yule anayekuja asijekulipa fidia kwa mtu.

Mhe. Spika, baada ya hayo na mimi nisichukue muda mwingi ilikuwa hamu yangu ni mambo matano haya ambayo nimeshayasema na nadhani serikali imeshasikia la kulifanyia kazi naomba lichukuliwe hayo ni mawazo ya wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini, naunga mkono bajeti ya serikali mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Ali Salim: Asante Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru *Allah* kuweza kunipa uwezo saa hizi kusimama baada ya kuruhusiwa nizungumze machache. Nadhani sitozungumza kama waliopita kwa sababu mimi si mtaalam wa uchumi walionitangulia ni wataalam wa uchumi, kwa hivyo yatageuka yale anayoyazungumza Mhe. Haji Faki kila siku kuwa ikishapita zumari, kinanda huwa hakina hazi tena. *(Kicheko).*

Mhe. Spika, hata hivyo kwa sababu ni wajibu wangu kufanya haya ninayoyafanya hivi sasa basi nitazungumza mambo kidogo lakini si kama mtaalam wa uchumi ni kama mtu ninayeishi na watu, kwa sababu unapoishi na watu ndio unajua matatizo yao. Lakini naomba Mhe. Spika, uniruhusu niseme kitu kimoja kidogo kabla sijachangia. Tunaposema kukosa mtoto na maji ya moto maana yake ni kuwa atazaa lakini yule mtoto atapita na tutakosa hata yale maji moto ya kutiwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo pia nianzie pale alipomalizia Mhe. Juma Duni Haji kuhusu soda inapoongezwa bei, yeye kasema anaathirika anayekunywa soda Darajani, mimi nataka niongezee anaathirika mgonjwa kwasababu soda kwetu sisi ni dawa mpaka uumwe ndio uinywe *(Kicheko).*

Mhe. Spika, sasa nataka niingie moja kwa moja katika suala zima la bajeti nataka nianze kutoka linalojulikana kwenda lisilojulikana au kutoka lililopita kwenda lijalo, lililopita ni bajeti ya miundombinu ya kilimo na utalii hilo ndio lililopita lakini linalokuja ni bajeti ya demokrasia na maendeleo. Kwa hivyo nianzie hii ya miundombinu nikisha nije kuunga na hii ya maendeleo ambayo tunaitarajia ije kuanzia mwaka ujao wa fedha, tunapozungumzia bajeti ya miundo mbinu tena mambo mawili kilimo na utalii kuna mambo ambayo huwa yanatutwanga ndani ya kichwa tunatarajia haya tuyaone katika kilimo yawe yamefanyika, haya tuyaone katika utalii kuwa yamefanyika mamo ya miundo mbinu.

Sasa mambo muhimu katika kilimo miundombinu yake ukiacha vifaa vya kisasa ambavyo vitamsaidia mwananchi katika kilimo hiyo ni miundo mbinu ya mwanzo, pembejeo atakazopelekewa mwananchi zikamsaidia katika kilimo ni miundo mbinu mingine. Lakini pia utaalam kwa sababu huwezi kutumia vifaa vya kisasa kama huna utaalam wa kuvitumia kwa hivyo lazima apelekewa na utaalam wa kilimo ili aweze kuchanganya mambo na kutoa vijambo, sasa tukiangalia hayo kwa upande wa kilimo haionekani kama mwananchi kawekewa miundo mbinu ya kutosha ya kilimo, tunaposema kilimo tusifikirie tu mambo ya mimea, tunaposema kilimo pia tuangalie mambo ya mifugo lakini pia tuangalie mambo ya uvuvi yote haya mimi nayaingiza katika kilimo, tujiulize je miundombinu ya mambo yote haya uvuvi, kilimo chenyewe, mifugo kweli miundo mbinu yake imepatikana katika bajeti hii iliyopita hivi sasa kweli wananchi wanazalisha vya kutosha kutokana na miundo mbinu waliyotayarishiwa katika bajeti iliyopita, nafikiri hili ni moja katika suala muhimu la kujiuliza kabla hatujenda mbele katika bajeti nyengine ambayo ina mambo mengine mapya.

Lakini pia tukija katika miundo mbinu ya utalii ni pamoja na barabara, lakini kuna baadhi ya maeneo tayari barabara ziko lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo ni mazuri mno kwa utalii na tayari umeshaanzishwa utalii lakini barabara yake hakuna mtalii ambae angeweza kuipita, nitatoa mfano mzuri kwa Wambaa. Watu siku hizi wananijua nikitoa mfano ninatoa wa Wambaa, barabara hivi sasa haipitiki kabisa kabisa, mvua hizi zilizopita na tulitarajia kwa sababu ni bajeti ya miundombinu ya utalii kule kwenye utalii kungefanywa hii miundo mbinu mwanzo na nakumbuka katika baraza hili tulipoambiwa kuna mradi wa barabara wa ufadhili wa NORWAY wa barabara sita za kusini.

Tulitoa mawazo yetu tukasema barabara hizi sita zote kupewa Mawasiliano wazijenge ni kupoteza muda mwingi bure, haiwezekani Mawasiliano wajenge hizi barabara sita za mradi, wajenge barabara za mfuko wa barabara, waende wakatie viraka barabara zinazohitaji viraka. Mawasiliano hao wana uwezo gani wa kufanya mambo hayo yote na yaende kwa muda mfupi, tukasema kama ni hivyo basi angalau zingegawiwa mbili wakapewa Mawasiliano mbili ikapewa kampuni moja na mbili nyengine wakapewa wengine sasa hivi angalau tungelikuwa barabara tatu tunazo, lakini kwa sababu inajenga mawasiliano peke yake mpaka hivi sasa hata barabara moja haijesha.

Mhe. Spika, hapa tuliambiwa barabara tatu zitaanza kwa umoja na kitabu cha Mhe. Waziri cha Wizara ya Fedha cha bajeti ya Serikali kinasema. " *Miongoni mwa barabara zilizokwishaanza moja katika hizo ni barabara ya Mzingani/Wambaa imo humu".* Sasa namthibitishia tu kuwa bado haijaanza na nyengine pia hazijaanza ya Chambani pia haijaanza, Tundaua haijaanza, Pujini haijaanza barabara iliyoanza ni ya Mtambile/Mwambe na Barabara ya

Mtambile/Kangani tayari imeshaanza kuparwa na ikafika pahali ikawa hakuna hata gari inayoweza kwenda huko Kandani kwenyewe. Kwa hivyo kitabu hiki kimesema barabara hizi zote tayari zimeshaanza kujengwa si kweli Mhe. Spika, Mhe. Waziri hakusema uongo lakini hakuwa na uhakika analolisema.

Mhe. Spika, jambo jengine katika miundo mbinu ya utalii ni suala zima la umeme naomba niipongeze serikali kuleta umeme kutoka Tanga kuja Pemba tuliuona siku ile ulivyokuwa ukienda, pale Mhe. Rais alipokuwa akibonyeza basu! Tuliuona umeme uliokuwa ukitoka Tanga ukienda zake mpaka ukafika Pemba ukamwaga pale katika kiwanja cha Gombani, hili mimi nalipongeza lakini kwa tahadhari kubwa kwa sababu moja haielekei kutokana na matukio kuwa kuna nia njema. Huu wa Unguja, bara walipandishiwa kidogo Unguja wakapandishiwa sanaa hivyo hii ni nia njema kwa hivyo jambo kama hilo linaweza kutoka na kule Pemba, Tanga wakapandishiwa kidogo lakini Pemba wakapandishiwa sana hili linanipa wasi wasi, siku zote mtu akitafunwa na nyoka basi akiona ukuti huwa anataharuki.

Mhe. Spika, hili nalisema kwa tahadhari kubwa lakini pia naiomba serikali bado ifanye juhudi ya kutafuta umeme wetu wenyewe ili miundo mbinu yetu hiyo ya utalii basi iwe ya uhakika kwa sababu umeme tunao tumeukalia lakini bahari yetu ina umeme kweli kweli na wameshakuja taaalam na wamesema habari hizo, kwa nini hatuutoi umeme tukauleta juu hili naomba kidogo nalo lishughulikiwe ili tuweze kwenda vizuri katika miundo mbinu hii. Kwa hivyo bajeti iliyopita inavyoonekana haikuweza kutekeleza ikaweza kukidhi haja tuliyoitarajia iweze kukidhi mara hii tumerudi na bajeti nyengine, sasa katika bajeti ya mara hii naomba Mhe. Spika, nianzie hapa katika mwelekeo wa hali ya uchumi mpango wa maendeleo wa bajeti wa mwaka 2010/2011 kwa sababu hapa ndio kwenye mambo yote ya huko mbele kuwa yatatekelezwa.

Mhe. Spika, nikianzia hapa nataka nianze na kifungu cha 149 na 150 hapa 149 naomba ninukuu kitu kidogo mafanikio haya ambayo yametajwa katika kifungu hicho yanategemea kuendeleza zaidi uwekezaji rasilimali na utekelezaji wa mkakati wa ukuzaji uchumi na mkakati wa usafirishaji utakaosaidia na utekelezaji wa juhudi za mageuzi katika sekta ya kilimo ambayo inatia mkazo zaidi kwa kuongeza thamani ya bidhaa. Haya mambo ya mageuzi katika sekta ya kilimo mimi siyajui maana yake sio mtaalam wa kilimo lakini humu hayamo, mageuzi gani tunayotaka kuyafanya hayamo isiwe tu kama kule nyuma kwamba tunageuza miundo mbinu lakini haikuimarishwa sasa angalau tungejuulishwa haya mageuzi ni yepi yaliyokusudiwa kuletwa katika kipindi cha bajeti hii ijayo katika asilimia sita ya kilimo ya bajeti ya serikali.

Lakini katika kifungu cha 150 tunaambiwa matarajio ya kukua kwa uchumi kwa mwaka 2010/2011 yanatokana na mambo yafuatayo. Katika mambo haya yote yafuatayo mimi nitazungumzia machache tu kwa sababu haya ndio mategemeo yetu, haya ndio yatakayotukuzia uchumi.

Kwanza ninalotaka kuzungumzia ni utekelezaji wa program ya mageuzi ya kilimo Zanzibar ambayo yatashajihisha uzalishaji kuongeza tija na kuhakikisha uhakika wa chakula hii ni kauli ya kisiasa sio kauli ya kiuchumi, kwa sababu kuna kauli ya uchumi na kauli ya siasa hii ni kauli ya kisiasa sio kauli ya uchumi, nadhani tungepewa kauli ya uchumi hapa tukaambiwa kutafanywa hili na hili katika kilimo. Kwa ufupi tu itakapokuja Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ikafafanua sasa hili lililokusudiwa kupangwa hivi litakuwa hivi na hivi na tutaleta hiki kwenye Wizara ya Kilimo, lakini hapa angalau kwa ufupi tukawekewa yale mambo muhimu yatakayofanywa katika utekelezaji wa mageuzi haya ya kilimo

Nikija katika kifungu (g) Washirika wa maendeleo wataendelea kusaidia juhudi za maendeleo Zanzibar. Hivi Mhe. Spika, sisi tumesharidhika na mwendo huu tunaosaidiwa mpaka tukafika pahali ikawa tunategemea kuwa msaada huu tunaopewa utatukwamua katika masuala ya uchumi ili uchumi wetu ukuwe.

Tukiangalia hapo nyuma tulivyofanyiwa, tumepata asilimia 32 za misaada na baadaye pamoja na kuongezewa na mambo mengine ndio tukapata asilimia 46. Sasa ikiwa misaada yetu tuliyopata huko nyuma imefikia asilimia hiyo tunawekaje matarajio kwa kukuza uchumi wetu kwa kutegemea jambo hilo hilo. Au tunataka fimbo ile ile itupige mara mbili. Watu wanavyosema fimbo ile ile mtu haimpigi mara mbili kwa nini sisi tutake fimbo ile ile itupige tena mara mbili.

Mhe. Spika, tuliloahidiwa hatukupewa, halikufika hata nusu, imepanda kidogo tu baada ya robo. Lakini lile lile na mara ya pili linakuja tena, tunasema hawa hawa ndio watakaotusaidia uchumi ukakuwa. Hivi kweli sisi tunafanya mambo haya kwa kuamini kwa umakini kabisa au tunafanya haya kwa sababu tuwe tunasababu tu ya kueleza ndani ya Baraza, kweli hili litatusaidia.

Kifungu (h) kuendelea utekelezaji mageuzi ya msingi. Haya Mhe. Spika, kwangu ni kitendawili naomba nije nieleweshwe, mageusi ya msingi ni yepi. Maana itakuwa kuna mageuzi ya msingi na kuna mageuzi ya ghorofa. Sasa haya ya msingi sijayajua, nikiyajua ya msingi na ya juu zaidi nitayajua, lakini kwanza niyajue haya ya msingi yaliyokusudiwa hapa ni yepi.

Katika kifungu cha (e) kuendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kijamii na kisiasa. Katika hili Mhe. Spika, naomba niseme njia ya kulifanya hili ipo.

Lakini njia hii itakuwa ipo kama tutashirikiana sote humu ndani ya Baraza, sote tukawa kitu kimoja, tukawa na kauli moja, hili linawezekana. Kwa sababu hili ni kuimarisha yale makubaliano yaliyotokea tukaletewa hapa, tukaijadili hoja binafsi, tukaletewa Mswada tukaupitisha, sasa hivi tunangoja tarehe 31 kwenda uwanjani kwenda kusema tunataka tuwe na umoja au hatutaki tuwe na umoja. Sasa kama sote sisi tuliyokuwemo humu tutashirikiana kwa umoja wetu tukasema tuwaambie wananchi wetu kuwa tunahitaji kuwa na umoja. Hili litatekelezeka, vyenginevyo wakitokea wengine wakenda kinyume na hili nalo litakuwa halitekelezeki. Kwa hivyo itakuwa yale matumaini tuliyopewa kuwa kutokana na mambo haya uchumi wetu utakuwa basi itakuwa kinyume chake, uchumi wetu utafuia na utadumaa.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 152 katika ukurasa wa 81 kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri. Kifungu hiki kinasema naomba ninukuu : "Maendeleo yanapaswa kulenga katika mafanikio ya wananchi walio wengi na kuimarisha uwezo wao" Tukisema tunatoa misamaha kwa wanaojenga nyumba za kijani za kulelea miche, hivi hawa ndio walio wengi. Kwa sababu kama hawa ndio walio wengi tutakuwa tumesibu, tumechoma ndipo. Lakini ikiwa hawa sio wengi, basi bado hatujawatafuta walio wengi tukawafanyia jambo la kuendeleza wao.

Mhe. Spika, tunaambiwa kwamba kuna uwezeshaji. Katika uwezeshaji walio wengi bado hawajawezeshwa ni wachache mno waliowezeshwa. Kwa hivyo hili nalo mpaka sasa lina matatizo sijui litatatuliwa vipi mpaka tufikie pahali tulete haya maendeleo katika kuhakikisha kuwa tunalenga katika mafanikio ya wananchi walio wengi.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba kunukuu "lengo la msingi la serikali ni kuona wananchi wanaishi maisha marefu yaliyo bora ambayo wananchi ni chaguo lao wenyewe"

Mhe. Spika, kwa kushindia kipande cha muhogo na chai kavu ukalalia muhogo wa nazi na mboga ya kisamvu hujajenga mtu mwenye afya njema hata siku moja. Hivyo ndivyo vyakula tunavyokula huko vijijini. Na hatuli hayo kwa kutaka, tunakula kutokana na uwezo. Je, lengo hili litatekelezeka Mhe. Spika. Ikiwa hali ya wananchi wetu ndio hiyo, hatuna tulilolifanya kuwainua wananchi wanakaweza kupata milo mitatu ya uhakika ya kitoweo kutoelea chakula, sio chakula kutoelea kitoweo. Utakapokula chakula kutoelea kitoweo utakachopata kingi sana ni uwanga. Mwananchi anavyotakiwa ale kitoweo atoelee chakula. Iwe chakula ni kidogo kuliko kitoweo, utakipataje kitoweo kingi. Kitoweo miongoni mwa vitoweo ni vitu vya baharini, mifugo, mboga mboga za majani, lakini hata hizo mboga za majani zinastahiki zipate na virutubisho vyengine kutoka kwenye nyama.

Hili ni jambo muhimu sana kulizingatia serikali katika bajeti yake. Wananchi wawezeshwe kuvua ili vipatikane vitoweo vya kutosha. Waheshimiwa waliotangulia hapa wamesema sana kuhusu suala la uvuvi kuwa hata kuwemo katika bajeti halimo, hivi vitoweo vitapatikana vipi.

Lakini si hilo tu, wananchi wetu hivi sasa wanavyovua uvuvi mkubwa ni wa madema. Uvuvi wa madema sasa hivi umepitwa na wakati, kwenda kuliweka dema ukamwambia samaki ukitaka ingia saa unayotaka ukitaka usiingie, huo sio uvuvi tena sasa hivi. Au uvuvi wa kuchukua mchipi ukenda ukaurusha ukamwambia huwooo ukiutaka kula hutaki basi. Sio uvuvi tena hivi sasa.

Sasa hivi tunapozungumzia uvuvi tumesema maeneo mengi tumeyaweka hifadhi ndio maeneo ambayo wavuvi wetu walikuwa wakienda wakigaragara humo wakipata chochote angalau wakipata mafuta ya taa. Lakini leo maeneo mengi tumeshayawekea hifadhi. Maana yake nini sasa, maana yake ni kwamba wavuvi tumewazuia mle wasivue. Sasa tufanye nini? Sasa hivi tuwawezeshe wavuvi wakavue huko kunapotakiwa kuvuliwa. Na huko si rahisi tu mvuvi kwenda akavua . Ikiwa ni mitego ya humu tu, humu karibu mnaniona shilingi milioni 20 ndio uweze kuutimiza mtego. Je, huo mtego wa kwenda kuvua huko na mimi niko huku utahitaji kiasi gani, (*Vicheko*).

Mhe. Spika, Bajeti hii haijaeleza chochote kuhusu hilo. Kwa hivyo tunaomba inapoandaliwa bajeti mambo kama yazingatiwe. Mimi ndio maana nikasema japo kuwa si mchumi lakini nakaa na watu kwa hivyo nitazungumza jinsi ya nnayoyaona na niliyoambiwa na watu ninaokaa nao. Kwa sababu mimi nina wavuvi wengi sana katika jimbo langu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie kidogo katika ukuzaji wa uchumi. Wengi walizungumzia suala zima la mafuta kuwa humu halikutajwa. Lakini na mimi nataka niongezee kitu kingine kipya ambacho kuwa hakijasemwa.

Mhe. Spika, mchemba wachemka chini baharini, nishaletewa habari na wavuvi wa jimbo langu walikuwepo Wambaa kuna sehemu Wambaa mafuta yanatoka wenyewe, ukenda maji yamejaa yanaelea juu, ukenda maji yametoka utayaona hasa yanatoka yanachirizika yanakwenda zake hayo.

Mhe. Spika, ikiwa jambo hili hata kuingizwa humu halikuingizwa tunatarajia nini siye kukua katika uchumi. Labda Mhe. Waziri atwambie kuwa labda hili hatua zilizobaki tena ni hatua za kufanywa siri siri. Lakini hatua za mwanzo naona tulifanyiwa dhahiri hapa na tukashirikishwa na sisi tukashiriki na tukafika pahali sasa hivi tuna mambo tunayasubiri lakini hatujayaona.

Mhe. Spika, kwa kweli nasikitika, mimi miguu yangu ni mibovu tu siwezi kufika huko pwani wenyewe yalipo hayo mafuta, wamenambia wanichukue wanipeleke lakini nimewambia jambo siku moja nitakaporudi waniingize japo kwenye gari la ng'ombe wanipeleke. Hiyo ndiyo hali yenyewe ilivyo. Jambo hili kwa kweli kutokuwemo ndani ya bajeti kwa kweli wametuvunja moyo sisi waheshimiwa tuliyokuwemo humu ndani ya Baraza lakini pia na wananchi wetu wakilipata suala hili kwa sababu kila siku wanatuulizia habari hizi, wakipata habari hii kuwa ndani ya bajeti hii halikutajwa. Aah! Watavunjika moyo sana tena sana.

Mhe. Spika, nikitoka hapo kabla kidogo niingie kama wenzangu katika suala zima la kero ni kero na kero inakera na ikikera anayekerwa anaghadhibika na anaweza akasema chochote kile kwa sababu kakerwa. Sasa tumeambiwa hapa kuwa kuna kero ambazo tayari zimepatiwa suluhisho. Moja katika hilo ni ugawaji wa mikopo ya bajeti sasa hivi sisi tunapata asilimia 4.5 hapa nina maswali mawili.

Swali la kwanza kwa nini?

Ni vigezo gani vilivyotumika tuambiwe tujue, isiwe huko mmeshazungumza nyie mnajua vigezo gani vilivyotumika lakini sisi ndani ya Baraza hatujui ni vigezo gani vilivyotumika. Kwa hivyo tuambiwe ndani ya Baraza hili ni vigezo vilivyotumika mpaka makafikia uamuzi wa kuondoa kero kwa kuipa Zanzibar asilimia 4.5 ni mambo gani muliyoyaangalia.

Swali la pili mnapataje taarifa ya mikopo yote ya Bajeti inayoipata Tanzania ili mkafanya hesabu mkajua haki ya Zanzibar ni kiasi gani, mnaarifiwa, kila mwaka mapema kuwa safari hii mikopo yetu ni kiasi fulani halafu mkafanya hesabu mkapewa. Kwa sababu hili lililofanywa mara hii inaonesha wazi kuwa, kama mnaambiwa basi mdanganywa. Kwa sababu aliyozungumza kwenye Bajeti *share* yetu ilikuwa iwe kubwa sana Mhe. Spika. Zaidi ya mara mbili ya hii tuliyopewa. Ina maana kama wao ndio waliokwambieni basi wanatudanganya. Kwa hivyo itafutwe njia ambayo hatutokuwa tukidanganywa tena, tutajua kima sahihi ili hiyo 4.5 kwa misingi yoyote mliyokubaliana lakini angalau itimie. Sasa hivi haitimii.

Mhe. Spika, kwa kweli suala zima la hiyo mifuko ya kumsaidia mwananchi mimi hasa huu wa TASAF, nadhani kuna mambo tunakosea. Kwa sababu nina mifano ya fedha ya TASAF kwa mawazo yangu ni sawa sawa na kwamba zilizochukuliwa na kutupwa baharini. Kwa mfano hii barabara ya Wambaa, fedha za TASAF zilitengeneza na ikatiwa kifusi, imeshatengenezwa tena mara tatu kwa kifusi. Sasa ile ya mwanzo iliyotiwa imekuwa kama imetupwa ikaja mvua ikachukua mambo yakesha. Mimi nafikiri hii miradi ya TASAF

ingechaguliwa ambayo itakayoweza kudumu kwa muda mrefu ili kuweza kuwasaidia wananchi. Usiwe mradi tu kwa sababu wameutaka wananchi hata kama wataalamu wanaona huu hautadumu muda mrefu ikawa lazima ukubaliwe tu hivyo hivyo. Wananchi kuna mambo ni lazima waelimishwe. Wananchi wanaweza wakachagua kitu wao wanaona kitawaletea manufaa kwao lakini kama hakina manufaa endelevu basi waelimishwe na wapewe mbadala wa mambo kama matatu au manne hivi wachague kuliko kuwaachia mradi ambao una hakika kuwa huu hautimizi hata mwaka mmoja itakuwa pesa zile zimepotea bure.

Mhe. Spika, hili la mifuko naomba lingezungumzwa vizuri, lingaangaliwa vizuri katika utekelezaji wake. Lakini pia katika hili la miradi nina kitu kimoja kidogo tu ambacho nataka nimalizie. Inavyoonekana hii miradi mingi inayofanywa kwa wananchi wanaofaidika zaidi si wananchi ni maofisa wanaosimamia miradi hiyo. Kwa mfano kuna kitabu katika kila mradi kilichotengenezwa kwa kutumia kompyuta yaani kimechapishwa kikawa *printed*, karatasi zake kiasi kama hizi mara mbili ndio wingi wa karatasi zake. Wenye mradi wanauziwa kitabu kile kuanzia laki moja mpaka laki mbili. Wakati ukenda kuchukua kitabu kilichochapishwa hasa, wachilia mbali cha kompyuta kilicho na volume kama hii mara 10 hakifiki hata elfu 50. Nashangaa ni gharama zipi walizopata waliotayarisha kitabu kile mpaka kifikie laki moja na hamsini au zaidi.

Suala jengine kuna *component* ya mafunzo mle yamepangwa mafunzo kumi yatatolewa. Anakuja afisa anafanya mafunzo siku mbili tu, lakini anachukua fedha za mafunzo ya siku kumi zote. Nani anayefaidika, anafaidika mwananchi au anafaidika afisa anayesimamia mradi. Mifano ninayo hai kabisa anayeyataka aje nitampeleka mpaka kwenye mradi aangalie vitabu na kila kitu. Kwa hivyo tunaposema tunataka tuwawezeshe wananchi basi tuwaangalie wananchi zaidi kuliko kujiangalia sisi wenyewe.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia. Ahsante.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii iliyokuwepo hapa mezani sasa hivi.

Mhe. Spika, kabla ya yote nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikutoa shukurani hizi ninazotaka kuzitoa. Kwanza kwa ruhusa yako nakuomba Mhe. Spika, uniruhusu nishukuru hawa nitakaowashukuru. Nilikuwa nnakilio cha watu waliopata maafa ya upepo ndani ya jimbo langu, nikalalamika hapa mwezi wa April kwa bahati suala lile limetekelezwa na serikali hii.

Mhe. Spika, kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Afisi ya Waziri Kiongozi, Afisi inayoshughulikia mambo ya maafa na Afisi ya Mkuu wa Mkoa, suala hili wamelitekeleza kwa kiwango chote na wananchi wangu wamefanikiwa na hivi sasa nyundo zinacheza kwa kuwezeka mabati. Isipokuwa kuna wachache wasiopungua 10 na zaidi sijui kama kompyuta ilirusha au kulikuwa na matatizo fulani hao natarajia pindipo mambo yakitulia na hao pia watafikiriwa.

Mhe. Spika, sasa nakuja katika bajeti. Nawashukuru wapanga bajeti hii ambayo tunayoichangia sasa hivi, kwa kweli wameipanga kwa utulivu, inaeleweka na inafahamika, nawapongeza wote kwa kazi hii.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 42 kifungu cha 78 kinachohusiana na kilimo. Tatizo la kilimo hapa nchini tunalo, tatizo kubwa kuhusu kilimo tunachotegemea sana hapa ni mpunga, migomba, mahindi na kadhalika. Lakini utakuta sasa hivi pale penye kilimo cha maeneo haya yote sasa hivi pameshavamiwa kwa makaazi ya kuishi binaadam. Kwa hivyo utakuta eneo la kilimo tulilokuwa nalo hivi sasa ni fupi sana, hakuna wakulima wanaolima kama heka tano au kumi ambapo ikawezekana kupata chakula cha kutumia yeye na chengine akauza nje. Ukulima wetu ndio huo huo mdogo mdogo heka tano, tatu wa kumsaidia mtu binafsi.

Mhe. Spika, ninachoona Waziri wa Wizara hii alenge zaidi na kutizama zaidi katika maeneo ya uwanda kwa kuwa tunayo maeneo makubwa ya uwanda na baadhi ya vilimo vingi vinakuja hata kwa kutilia maji, angalau katika matumizi tunayotumia katika majumba, wiki ipatikane mara mbili au mara moja angalau mtu apike kile anachokizalisha mwenyewe hapa ikiwemo mihogo, viazi, ili kuepukana na michele ya kutoka nje.

Mhe. Spika, katika ukulima huu tunao ukulima mkubwa ambao tunautegemea kusafirisha kama vile karafuu. Hili nalo ningeliomba tukalitilia mkazo kwa kuwa maeneo yapo wakahamasishwa wananchi wetu wote ili kwa kila palipo mkarafuu ukapandwa mikarafuu mengine, mikarafuu hata ikikatwa kuni ikipandwa tena inakuja zake.

Ningemuomba Mhe. Waziri hili akaliangalia ili tukapata uchumi wa kutusaidia katika mambo yetu mbali mbali ya kimaisha katika nchi yetu.

Jengine kwa kuwa MANCEP inahusika na Wizara ya Kilimo kwa hivyo hii ningeomba Mhe. Waziri akaisimamia sana, ina nyenzo nzuri za kuweza kuwapatia ajira wananchi wetu, wakianzisha masuala ya uvuvi wa bahari kuu hapa kwa kweli tunaweza tukafanikiwa tukapata viwanda vya kusindika samaki na tukapata meli za kuvua huko ili vijana wetu wakapata ajira ya kutosha.

Ningemuomba Mhe. Waziri muhusika na mambo ya makero ya Muungano hili suala la Bahari Kuu kwa kuwa ni moja wapo tukilitegemea litatusaidia kutupatia ajira na kukuza uchumi kwa hivyo alifanyie mbinu zake zote ili likaondolewa ndani ya mambo ya Muungano, faida tutakayoipata katika sekta hii haitomfaa Juma peke yake itamfaa hata Joseph. Ningeomba kitengo hiki kikafikiriwa sana ili wakafaidika wananchi wetu kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nije katika mambo ya biashara kuu ya vyakula. Sasa hivi imekuwa tunapata vyakula vingi kutoka nje na vinapitia kwenye bandari yetu. Tatizo lililokuwepo bei zinapanda kiholela kwa hivyo hatujui tatizo lipo wapi kama tatizo ni katika mabandari yetu ningeomba hili lifikiriwe ili kupunguziwa gharama zaidi za ulipaji ili likawa jingi katika nchi yetu na tukafaidika kupata bei nafuu. Biashara kama hizi zinazohusika na vyakula kidogo tungepunguziwa hapa ingeonesha njia nzuri ya kukuza uchumi wetu ili wananchi wetu wakafaidika kupata mahitaji kwa bei nafuu.

Nitoe mfano mmoja kidogo. Kama nyumbani utakuwa na panya wengi wanakuletea tabu wanakula vitu ambavyo vivyo walivyopangiwa, ukitafuta mtego ukiweka chambo kidogo tu mle ikiwa pweza au ikiwa ngisi, watarundikana panya wale, watajiingiza mle kwa kufata mtego ule. Kwa hivyo na hili suala la biashara kama tutaweka mtego wa kuweka unafuu kwa wafanyabiashara zitamiminika biashara za kutosha. Kwa maana hiyo hizi zilizokuwa zinapanda bei zitapungua.

Mhe. Waziri ningeomba hapo paangaliwe ili kupata wafanyabiashara wengi baadaye tutawapata katika biashara zao katika kuuza kwao kunako leseni, au katika mitaji yao mengine tunaweza tukafaidika zaidi kimapato kwa njia hiyo.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya nchi huwa zinafaidika kwa mipango ya biashara mbali mbali, ambapo watu huingiza na kusafirisha bidhaa. Suala hili nimezungumza kwa kipindi kirefu kuweka biashara huria. Kwa hivyo, pindi suala hili likiendelezwa nafikiri itakuwa ni chanzo kimojawapo cha kusaidia mapato serikali yetu.

Mhe. Spika, niende haraka haraka ukurasa wa 44 kifungu 81 kinachohusiana na elimu. Katika kuwapatia wananchi elimu bora na yenye manufaa tujitahidi zaidi kwenye elimu ya kati na ya juu.

Sasa hivi baadhi ya vijana wetu wanaosoma elimu ya kati na ya juu baada ya siku ya matokeo wengi wao huwa hawafaulu vizuri, ni wachache tu wanaofaulu. Lakini sasa ukishawaacha pale kuwa hawafaulu basi mimi huchanganyikiwa. Kwa sababu sio wengi wenye uwezo wa kutafuta elimu tena.

Kwa hivyo, pale utaona tunakosa vijana wengi ambao walitakiwa waendelee zaidi ili kupata mategemeo ya baadae katika kuleta maendeleo nchini mwetu.

Mhe. Spika, zamani elimu za kati au za msingi ilikuwa wanaofeli kama *marks* zao nzuri huwa wanarejea tena darasa lile lile. Kwa hivyo, tulikuwa tunapata kuwachuja na wengi walikuwa wanafanikiwa kuendelea zaidi. Lakini baada ya kuondoka mfumo ule utakuta wengi wanazurura ovyo bila ya mpangilio wowote. Ningemuomba Mhe. Waziri na hapa wakapaangalia ili vijana wetu tukawaendeleza kwa mafanikio ya baadae ya serikali yetu.

Katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali naipongeza sana kwa juhudi yake kubwa inayochukua kwa majengo mbali mbali ya vyuo vikuu na sekondari, wanavyojitahidi kujenga ili tupate kufanikisha wanafunzi wetu wapate sehemu za kusomea. Mimi nafikiri karibu nitajengewa jengo la gorofa, basi nalipongeza sana hilo ili niondoshe kero kwa wanafunzi wangu wanaosoma katika jimbo langu, waepukane na masafa marefu ya kwenda kusoma mbali. Kwa hivyo, juhudi hii ya Wizara ya Elimu nawashukuru sana.

Lakini kuna tatizo la elimu kuwasomesha wanafunzi. Wajitahidi kutafuta au waongeze zaidi wataalamu ili katika kufanya mitihani yao wafaulu vizuri mwisho wa mwaka.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 46 kifungu cha 87 kinachohusiana na masuala ya afya. Mara nyingi kampeni ya chanjo huna haja kubwa ya kuangalia wanaopewa chanjo hizo kuwa zina madhara au vipi. Kwa sababu watu wetu wana siku maalum ya kupewa chanjo mbali mbali. Lakini imebainika kwa baadhi ya watoto wanaopewa chanjo huwa wanapata madhara kutokana na chanjo zile.

Kuna baadhi ya watoto ambao tunawajua wamepata chanjo lakini baada ya muda wamedhurika. Wakati mwengine wanapolazwa hospitali huwa wanatibiwa maradhi mbali mbali yanayotokana na masuala ya chanjo na mafaili yanakuwepo. Lakini utakuta hawafuatiliwi au kuangaliwa na kupata madhara baadae, ndipo pale utapoona wengine wanapata ulemavu uliokuwa haukutarajiwa.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri katika mpango huu wa kutoa chanjo kwa baadhi ya wale wanaolazwa kwa matatizo ya chanjo, kama vile homa za mapafu au uti wa mgongo, basi akawa anachungulia sana mafaili yale ili kuwafuatilia wale wanaodhurika kwa madhara kama hayo.

Nije ukurasa wa 47 kifungu cha 88, homa ya malaria. Mhe. Spika, nashukuru sana kwa juhudi iliyochukua serikali hii katika kupigana na maradhi ya malaria.

Serikali imejitahidi vya kutosha, wengi wetu tulikuwa tunasumbuliwa sana na maradhi hayo. Mtu alikuwa hana nafasi ya kufanya kazi, akiwa baba mzima basi mtoto mgonjwa, huna raha hata ya kwenda kazini. Lakini sasa kwa kiwango kikubwa wananchi wetu wameepukana na masuala hayo ya maradhi ya malaria.

Kwa hivyo, katika juhudi hio naipongeza sana wizara kwa mkakati wao huo waliochukua wa kufanikisha kwa kiwango kikubwa kuondoa maradhi hayo hapa nchini.

Tatizo lililojitokeza sasa hivi kumekuwa na mbu na kunguni wengi. Mhe. Spika, si kutwa kumuona mwakilishi wako kaja hapa na suti nzuri lakini anatembelewa na kunguni kwenye suti hiyo. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, kitengo kilichopambana na maradhi ya malaria kikaangalia na matatizo ya wadudu hawa waliojitokeza. Kuna mbu hatuwajui maradhi yao nini na kunguni vile vile. Sasa katika ufukizaji wa dawa watizame na dawa za kuondoa tatizo hili ambalo sisi wananchi hatujui wataleta madhara gani?

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 48 kifungu cha 90 kuhusiana na masuala ya maji. Kwa kweli niwapongeze watu wa Mamlaka ya Maji kwa juhudi yao kubwa wanayochukua. Kwa kuwa kamati yangu ndio iliyokuwa imepangiwa wizara yake, tulikuwa tukitembelea sana, basi nimeziona juhudi walizokuwa wakizifanya. Kwa kweli hali zimekuwa nzuri, maji vijijini yameenea vya kutosha, kila pahali sasa katika vijiji vyetu bomba za maji zipo na mitandao mipya.

Mhe. Spika, tangu tulipokuwa na Kampuni ya KONOIKE sasa hivi tuna ACRAA. Kwa hivyo, nawapongeza watu wa Mamlaka ya Maji kwa juhudi hiyo waliyochukua.

Lakini pia kuna tatizo dogo tu ambalo linataka kufanyiwa ufumbuzi. Kwa kuwa maji tumeshakuwa nayo tunayapata, tatizo la kukatika katika umeme katika vianzio vya maji lidhibitiwe. Kwa hivyo, hilo nitamuomba Mhe. Waziri walifanyie kazi ili tatizo hilo liondoke na wananchi wafaidike na maji safi ya bomba.

Nikiendelea katika wizara hiyo hiyo kuhusiana na masuala ya umeme. Naipongeza sana wizara hii kwa juhudi kubwa inayochukua kwa kushirikiana na Serikali iliyoko madarakani kuwapatia umeme wananchi wa Visiwa vya Pemba na Unguja, ili kuwapunguzia gharama ya kutumia umeme kwa bei kubwa. Kwa juhudi hii waliyochukua nawapongeza.

Vile vile niwapongeze kwa juhudi waliyochukua ya kuweka majenereta zaidi ya 32 hapo Mtoni ili kuwa na hakiba pindi pakitokea tatizo la umeme.

Lakini Mhe. Spika, tatizo liliopo, tuna wenzetu hawa wanaitwa *EWURA*. Kwa kweli Mhe. Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa, kunaletwa *bill* iliyopita kiwango tofauti na kadirio la bei iliyopo au iliyokuwa kwa wenzetu. Utakuta *unit* moja Bara shilingi 27 elfu na Unguja ilikuwa kama imezidi basi shilingi 28 elfu. Lakini sasa hivi kuna bajeti ya *unit* moja kutumia shilingi 168. Kwa kweli tutawapa mzigo mkubwa sana wananchi wetu.

Suala hili katika kutembelea katika kamati yangu tumelikuta na hivyo linaleta bughudha sana. Kama itakuwa deni hili italipa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi utakuta kuna mambo mengi ya mafao juu ya mahitaji ya wananchi tutayakosa. Kwa hivyo, deni la kusingiziwa kama hivi linaleta bughudha. Ningemuomba Mhe. Waziri anayehusika na suala hili wakalifanyia ufumbuzi mapema ili bei zetu zikaoana na sisi tukauza umeme angalau kwa faida kidogo na wananchi wetu wakafaidika na bei nafuu ya umeme huo.

Mhe. Spika, nimeamua kulisema hapa hili kwa makusudi kwa sababu limeleta kero kubwa sana. Sasa katika masuala ya kuondoa makero ya Muungano na hili moja wapo lipo la kuwekwa bei kubwa za kiholela. Kwa hivyo, ningeomba suala hili likaangaliwa sana na kupatiwa ufumbuzi. Si hivyo, tutakuwa na wasi wasi kwa kuwa ndio tumeunga basi ndio tuwekewe bei kubwa kama hiyo? Kwa kweli hili litaleta usumbufu. Ndio pale ninaposema tutafute miundombinu mingine angalau kujiwekea hakiba kuepukana na masuala haya ya kupanda kwa umeme kiholela.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda unamalizika niende haraka haraka na sasa nitazungumzia kuhusu suala la ujenzi wa barabara. Kwanza nawapongeza *UUB* wanajitahidi sana kwa Unguja na Pemba. Kwa ziara tuliyoifanya ya kutembelea mabarabara tumeona hali ni nzuri sana kwa upande wa barabara zetu.

Lakini nitachokiomba Mhe. Waziri kuna baadhi ya vifaa vya kutengenezea barabara tulipotembea tumevikuta vimeharibika. Kwa hivyo, ningeomba katika bajeti yao kama ipo basi wakawa wanapewa haraka sana ili kutafuta vipuri na vipate kufanyiwa kazi kwa haraka katika barabara zetu.

La mwisho nitalizungumza kama wenzangu walivyozungumza. Kwa kuwa muda wa vikao vyetu vya Baraza kwa kipindi hiki cha miaka mitano unamalizika, lakini tulikuwa na masuala yetu ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, hilo nasema pindi wananchi wakiturejesha tena tutalitetea kwa nguvu zetu zote na anayehusika na suala hili tutamuomba awajibike, lakini hili

lifanikiwe. Kwa kuwa pameshaanza kutolewa wataalamu kwenda kusoma basi liendelee moja kwa moja. Isije ikawa likiondoka awamu hii awamu ijayo likawa linalazwa kwa miaka mingi tu. Kwa hivyo, tunasema wazi kwa uongozi huu pindi tukirudi tena tutalitetea suala hili kwa kushirikiana na viongozi wote waliopo hapa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana na ninaiunga mkono hotuba hii kwa kushirikiana na wananchi wangu wa Jimbo la Amani kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 15/06/2010 saa 3:00 asubuhi)